# KISWAHILI

## Mwongozo wa Mwalimu

## Kidato cha 5

## Mchepuo wa Lugha

©2024 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# Dibaji

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha nne katika ngazi ya juu ya elimu ya sekondari.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa .

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mkufunzi litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;
- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

# Shukrani


Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikimilisha kitabu hiki.



**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

# Yaliyomo


Dibaji ..... iii

Shukrani ..... v

Mpangilio wa masomo ya Kiswahili ..... 1

Mapendekezo kuhusu huduma kwa wanafunzi wenye matatizo maalumu katika mafunzo yao ..... 20

Shughuli za ufundishaji ..... 22

Muhula wa kwanza ..... 26

**Sura ya 1: Nadharia ya fasihi simulizi ya Kiswahili na tanzu zake ..... 26**

Somo la 1: Fasihi ya Kiswahili ni nini? ..... 32

Somo la 2: udhamini wa kazi za sanaa za fasihi simulizi ..... 42

Somo la 3: Tanzu za fasihi simulizi ya kiswahili na vipera vyake ..... 52

Somo la 4: Mifano ya nyimbo za kiswahili katika fasihi simulizi..... 62

Somo la 5: Mifano ya Methali za Kiswahili ..... 70

Somo la 6: Mifano ya nahau na misemo ya Kiswahili ..... 77

Somo la 7: Mifano ya Vitendawili vya Kiswahili ..... 87

Somo la 8: Ushairi wa Kiswahili katika fasihi simulizi ..... 96

Somo la 9: Aina za sentensi za Kiswahili ..... 103

**Sura ya 2: Fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili ..... 114**

Somo la 10: Uhakiki katika fasihi simulizi na vipengele vyake ..... 120

Somo la 11: Kuhakiki hadithi za Kiswahili ..... 126

Somo la 12: Kuhakiki methali za Kiswahili ..... 134

Somo la 13: Kuhakiki vitendawili vya Kiswahili ..... 140

**Muhula wa pili ..... 146**

Somo la 14: Uhakiki wa nahau na misemo ya Kiswahili ..... 146

Somo la 15: Uhakiki wa nyimbo za Kiswahili ..... 151

Somo la 16: Kuhakiki mashairi simulizi ya Kiswahili ..... 159

Somo la 17: Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi ..... 164

Somo la 18: Utoaji wa uwasilishaji kuhusu kazi za fasihi simulizi ..... 170

Somo la 19: Muundo wa sentensi za Kiswahili ..... 176

**Sura ya 3: Utungaji wa barua rasmi, simu na matangazo** ........ **186**
Somo la 20: Barua rasmi au ya kikazi na utungaji wake ........ 190
Somo la 21: Utungaji wa simu ........ 195
Somo la 22: Utungaji wa matangazo ........ 199

**Muhula wa tatu** ........ **203**
Somo la 23: Kupambanua sentensi za Kiswahili ........ 203

**Sura ya 4: Ufahamu na ufupisho** ........ **210**
Somo la 24: Ufahamu wa habari ........ 216
Somo la 25: Ufupisho wa habari ........ 221
Somo la 26: Muhtasari wa matumizi ya nyakati kuu za Kiswahili ........ 225

**Marejeo** ........ **229**

## *MPANGILIO WA MASOMO YA KISWAHILI*

***Ndugu mwalimu,***
***Fuata mpangilio wa masomo uliotolewa hapa chini ili kuweza kutoa maudhui ya msingi yaliyokusudiwa kufundishwa katika sura zilizochaguliwa na kumsaidia mwanafunzi kuwa na uwezo unaotakiwa mwishoni mwa kidato cha tano, mchepuo wa lugha. Uwezo huo ni huu ufuatao:***

- ***Kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali;***
- ***Kufanya utungaji na ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kwa ufasaha;***
- ***Kufanya ufafanuzi wa kina wa kila utanzu uliopo katika fasihi ya Kiswahili;***
- ***Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi;***
- ***Kuainisha na kubainisha tanzu za fasihi ya Kiswahili na kueleza dhima ya fasihi katika jamii;***
- ***Kufanya mawasiliano rasmi kwa ufasaha akizingatia malengo na nyenzo ya mawasiliano inayotumika;***
- ***Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habaria mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii za kimasimulizi na kimaandishi.***

***Kumbuka kuwa Kitabu cha Mwanafunzi kinachohusiana na Mwongozo wa Mwalimu huu kimeandikwa kwa mtindo wa mtaala Uegemeao katika uwezo ambapo mbinu za kufundishia na kujifunzia zinamshirikisha mwanafunzi kimpango na kimatendo. Ni kusema kwamba mtindo huu unatoa mwongozo wa maingiliano kati ya mwanafunzi na mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji huku ukibainisha stadi za kivitendo na ujuzi ambao mwanafunzi ataupata wakati atakapokuwa anajifunza na baada ya kufika mwisho wa kila sura au mada ya ujifunzaji.***

# A. MPANGILIO WA MASOMO KWA MUHULA WA KWANZA

| Mada kuu | mada ndongo | Vipindi | Sura | Shabaha | Njia / Mbinu | Vifaa | Uwezo wa kuendelezwa | Maadili na mwenendo | Idadi ya kazi | Masuala mtambuka yatakayo-shughulikiwa | Tathmini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Uwanja wa fasihi kama sanaa | 1.Nadharia ya fasihi simulizi ya Kiswahili na tanzu zake | 65 | 1.Maana ya fasihi ya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelezea fasihi ya Kiswahili; | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 29 | -Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (Kuishi kwa amani na kuendeleza jamii)<br>-Usawa wa jinsia;<br>-Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari;<br>-Elimu isiyo na ubaguzi | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | 2.Udhamini wa kazi za sanaa za fasihi simulizi | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelezea udhamini wa kazi za kifasihi | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, matini na majarida yanayoelezea udhamini, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua udhamini wa kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili katika kuiendeleza jamii au nchi | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 28 | -Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo<br>-Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua, kufafanua kwa kina na kuzielezea tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na makundi yake makuu yaani semi, masimulizi, ushairi na mazungumzo. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 33 | -Mafunzo kuhusu uzalishajimali<br>-Mila na desturi, na kuzalisha kwa kiwango<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 4.Mifano ya nyimbo za Kiswahili katika fasihi simulizi | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua nyimbo na kujadili mchango wake katika jamii. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea nyimbo za Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua nyimbo za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 32 | -Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza (Mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaani zeruzeru au albino)<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI na madhara yake<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo ya kudumu<br>-Usawa wa jinsi | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5.Mifano ya methali za Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua methali, kuzitumia kwa kuzihusisha na maisha ya kila siku na kujadili mchango wake katika jamii. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea methali za Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua methali za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 26 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo kuhusu kuboresha uzazi (kutii mpango wa serikali wa kuboresha uzazi) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 6.Mifano ya nahau na misemo ya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua nahau na misemo, kuitumia kwa kuihusisha na maisha ya kila siku na kujadili mchango wake katika jamii na lugha. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea nahau na misemo ya Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua nahau na misemo ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 31 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Amani na maendeleo | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7.Mifano ya vitendawili vya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua nahau na misemo, kuitumia kwa kuihusisha na maisha ya kila siku na kujadili mchango wake katika jamii na lugha. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea nahau na misemo ya Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua nahau na misemo ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 31 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Amani na maendeleo | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 7.Mifano ya vitendawili vya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua vitendawili na kujadili mchango wake katika jamii. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea vitendawili vya Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua vitendawili vya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuvitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 31 | -Elimu isiyo na ubaguzi<br>-Amani na maendeleo | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8.Ushairi wa Kiswahili katika fasihi simulizi | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua mashairi na kujadili mchango wake katika jamii. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea mashairi simulizi ya Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | Kufafanua mashairi ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuyatumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | 29 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Usawa wa jinsia<br>-Kutunza mazingira | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 9.Aina za sentensi za Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kubainisha aina za sentensi za Kiswahili | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya sarufi ya Kiswahili, matini na majarida yanayoelezea aina za sentensi za Kiswahili, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuzingatia aina za sentensi za Kiswahili | -Kufurahia kujua kuainisha sentensi za Kiswahili | 32 | -Kutunza mazingira<br>-Uzalishajimali | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani<br>-Upimaji wa jumla au upimaji wa kujifunza: Unawanyiwa darasani au nje ya shule kwa muundo wa mtihani wa taifa |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelewa na kuelezea uhakiki katika fasihi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 24 | -Uzalishajimali,<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu,<br>- Mafunzo kuhusu mpango wa kuboresha uzazi<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa hadithi simulizi za Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika hadithi simulizi za Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 26 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI (magonjwa mengi ya zinaa kama vile UKIMWI)<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza mali yako ili uweze kupata faida) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. Uhakiki wa methali za Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa methali za Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika methali za Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 23 | -Amani na maendeleo,<br>-Usawa wa jinsia,<br>-Uzalishajimali<br>-Mafunzo kuhusu maendeleo ya kudumu | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 4. Uhakiki wa vitendawili vya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa vitendawili vya Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 22 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Amani na maendeleo ya kudumu | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

## B. MPANGILIO WA MASOMO KWA MUHULA WA PILI

| Vipindi | Sura | Shabaha | Njia / Mbinu | Vifaa | Uwezo wa kuendelezwa | Maadili na mwenendo | Idadi ya kazi | Masuala mtambuka yatakayo-shughulikiwa | Tathmini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 5.Uhakiki wa nahau na misemo ya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa nahau na misemo ya Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika nahau na misemo ya Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 21 | -Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (kuboresha maisha na mazingira ya binadamu)<br>-Elimu isiyo na ubaguzi | -Tathmini<br>-Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6.Uhakiki wa nyimbo za Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa nyimbo za Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika nyimbo za Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 21 | -Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (Umoja na maridhiano) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| 7.Uhakiki wa mashairi simulizi ya Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa mashairi ya Kiswahili.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika mashairi simulizi ya Kiswahili. | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | 22 | -Mafunzo kuhusu kuboresha uzazi<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza mali na kutegemea benki ili kuboresha maisha ya mtu) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8.Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelezea hadharani maoni yao kuhusu utanzu wa fasihi simulizi ambao wameusoma au kuusikiliza darasani kwa kueleza walichofurahia, walichochukia, walichijifunza na kadhalika | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti kuhusu utoaji wa maoni binafsi, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili. | -Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mtumwingine bila ugomvi wowote.<br>-Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika tanzu inayoshughulikiwa. | 17 | -Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (kuwahudumia maskini hohehahe kwa kuwapa ng'ombe)<br>-Elimu isiyo na ubaguzi (elimu kwa wote na wanawake kuwa warithi) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9.Utoaji wa uwasilishaji kuhusu kazi za fasihi simulizi | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuwasilisha mada inayohusiana na uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi;<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kulinganisha tanzu moja na nyingine kwa kueleza kufanana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya fasihi, magazeti kuhusu utoaji wa mhadhara, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili. | -Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mtumwingine bila ugomvi wowote.<br>-Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika tanzu inayoshughulikiwa. | 17 | -Mafunzo kuhusu kuzalisha kwa kiwango (bidhaa za kweli yaani zisizo za bandia)<br>-Amani na maendeleo<br>-Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10.Muundo wa sentensi za Kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kukumbuka mambo muhimu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Vitabu vya sarufi ya Kiswahili, magazeti kuhusu muundo wa sentensi za Kiswahili, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki na kifutio | -Kuzingatia muundo wa sentensi za Kiswahili | -Kufurahia kujua kuchambua sentensi ya Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake. | 27 | -Mafunzo kuhusu maendeleo ya haraka ya uchumi<br>-Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (sigara huharibu afya ya mtu) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani<br><br>-Upimaji wa jumla au upimaji wa kujifunza: Unawanyiwa darasani au nje ya shule kwa muundo wa mtihani wa taifa |
| | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 72 | 1.Barua rasmi au ya kikazi na utungaji wake | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kueleza tofauti iliyopo baina ya barua ya kirafiki na barua rasmi.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutunga barua ya kikazi kutokana na kisa kinachojitokeza.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kukumbuka sehemu muhimu za barua rasmi.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutoa mfano wa barua za kikazi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa barua, magazeti, mtandao wa intaneti, vitabu, ubao, chaki, kifutio. | -Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu. | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | 18 | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (umoja na maridhiano baina ya Wanyarwanda) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. Simu na utungaji wake | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua mtindo wa simu.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutunga simu ya maneno kutokana na kisa kinachojitokeza.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelewa sehemu muhimu za simu ya maneno.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutoa mfano wa simu ya maneno. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa simu ya maneno, magazeti, mtandao wa intaneti, vitabu, simu ya mkononi, ubao, chaki, kifutio. | -Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu. | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | 18 | -Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani<br><br>-Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.Matangazona utangaji wake. | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kutambua mtindo wa tangazo.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutunga tangazo kutokana na kisa kinachojitokeza.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelewa sehemu muhimu za tangazo.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutoa mfano wa tangazo. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa matangazo, magazeti, mtandao wa intaneti, vitabu, ubao, chaki, kifutio | -Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu. | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | 18 | -Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza pesa na kuwasiliana na benki ili kukuza mtaji)<br>-Mafunzo kuhusu amani (mkataba wa amani)<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (kuepukana na kuvuta sigara) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | | | | | | | | |

## C. MPANGILIO WA MASOMO KWA MUHULA WA TATU

| Vipindi | Sura | Shabaha | Njia / Mbinu | Vifaa | Uwezo wa kuendelezwa | Maadili na mwenendo | Idadi ya kazi | Masuala mtambuka yatakayo-shughulikiwa | Tathmini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.ucha nganuzi wa sentensi za kiswahili | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye mitindo mbalimbali ya uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili, magazeti, mtandao wa intaneti, vitabu, ubao, chaki, kifutio. | -Kuzingatia uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili | -Kufurahia kujua kuchanganua sentensi za Kiswahili | 23 | -Mafunzo kuhusu amani -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani<br><br>-Upimaji wa jumla au upimaji wa kujifunza: Unawanyiwa darasani au nje ya shule kwa muundo wa mtihani wa taifa |
| | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 72 | 1. Ufahamu wa habari na mbinu zinazofuatiliwa | -Wanafunzi wawe na uwezo wa kuelezea mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo kujibu kwa ufasaha maswali yanayoulizwa kuhusu kifungu cha habari husika. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye habari mbalimbali, taarifa, kanda na vinasa sauti, ubao, chaki, kifutio. | -Kumwezesha mwanafunzi kusoma vifungu vya habari na kuvitafsiri | -Ukuzaji wa tafakari tunduizi.<br>-Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine.<br>-Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani. | 19 | -Mila na desturi na kuzalisha kwa kiwango<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani |
| | 2. Ufupisho wa habari na mbinu zinazofuatiliwa | -Wanafunzi wawe na uwezo kutaja sifa za ufupisho mzuri.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kujadili kanuni za ufupisho wa habari fulani.<br>-Wanafunzi wawe na uwezo wa kutoa maana inayopatikana katika aya za kifungu cha habari bila kuyapotosha | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Kumwezesha mwanafunzi kusoma vifungu vya habari, kuvitafsiri na kuvitolea ufupisho | -Ukuzaji wa tafakari tunduizi.<br>-Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine.<br>-Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani. | 18 | -Usawa wa Jinsia<br>-Elimu isiyo na ubaguzi | v |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.Muhtsari wa matumizi ya nyakati kuu za kiswahili. | -Wanafunzi waweze kukumbuka na kuzingatiamabadiliko yanayojitokeza katika matumizi ya nyakati za Kiswaahili katika hali yakinishi na hali kanushi. | Kazi katika jozi, kazi katika makundi, kazi ya mwanafunzi peke yake, michezo, mawasiliano, utafiti, ubunifu na ugunduzi | -Matini zenye habari mbalimbali kuhusu matumizi ya nyakati za Kiswahili, taarifa, kanda na vinasa sauti, ubao, chaki, kifutio. | -Kumwezesha mwanafunzi kuzingatia matumizi ya nyakati kuu za Kiswahili | -Kufurahia kujua kutumia ipaswavyo nyakati kuu za Kiswahili | 10 | -Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kurutubisha shamba ili kupata mavuno mengi)<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (kutetea haki za watoto na kupiga marufuku ubakaji wa watoto) | -Tathmini endelezi au tathmini ya ujifunzaji: Inayofanyiwa darasani<br><br>-Upimaji wa jumla au upimaji wa kujifunza: Unanyiwa darasani au nje ya shule kwa muundo wa mtihani wa taifa |
| | | | | | | | | |

Ili mpangilio huu wa masomo ufikie lengo lake, ni lazima uzingatie jinsi muda ulivyopangwa katika kitabu hiki cha mwongozo. Kumbuka kuwa mwalimu si mhubiri bali anawasaidia wanafunzi katika shughuli zao za kujifunza ili waweze kuzipata stadi zotakazowaongoza katika kozi zao.

## MAPENDEKEZO KUHUSU HUDUMA KWA WANAFUNZI WENYE MATATIZO MAALUMU KATIKA MAFUNZO YAO

Unapofundisha, kumbuka kuwa baadhi ya wanafunzi wanaweza kuelewa somo kwa urahisi lakini, kwa wengine, ikawa vigumu kuelewa kutokana na matatizo yao binafsi hususan matatizo ya kiafya. Haya yafuatayo ni makundi ya wanafunzi hao wenye matatizo mbalimbali:

Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu:

**1. Wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu**

- Ulemavu wa viungo vya mwili;
- Ulemavu wa kiakili;
- Matatizo ya kuona;
- Matatizo ya kusikia;
- Matatizo ya kukua kwa sehemu za mwili;
- Matatizo mbalimbali;
- Matatizo ya kuongea na kuwasiliana.

**2. Wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza**

- Uwezo mahususi wa kiujumla katika kujifunza;
- Werevu wenye kipaji cha hali ya juu.z

**3. Wanafunzi wenye matatizo ya kijamii, kihisia na kimwenendo**

- Matatizo ya kihisia;

- Matatizo ya kimwenendo;
- Matatizo ya kijamii / Udhaifu.

**4. Wanafunzi wenye matatizo yahusuyo mitaala**

- Matatizo katika kutunza na kutumia rasilimali za kielimu (wakiwemo wanafunzi wanaotumia mkono wa kushoto kwa kuandika);
- Matatizo ya kuelewa au kutumia lugha ya kufundishia (wakiwemo wanafunzi wachache wawezao kutumia lugha hiyo).

**5. Wanafunzi wenye matatizo ya kiafya (magonjwa mbalimbali)**

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mwalimu uwasaidie ipasavyo. Msaada wako utakuwa wa:

- Kuwaambia wale wenye tatizo la kutoona au kutosikia vizuri wakae kwenye dawati zilizoko sehemu za mbele karibu na mwalimu;
- Kupanga kazi maalum zilizoandikwa kwenye karatasi kwa wanafunzi wenye matatizo ya kusikia;
- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kuongea na kuwasiliana na wengine, kupewa muda wa kuongea,...;
- Kuunda makundi ya wanafunzi kutokana na ujuzi na uwezo wao katika kujifunza;
- Kupanga kazi au mazoezi kutokana na makundi ya wanafunzi wenye matatizo maalum ya kielimu;
- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kimwenendo na kuwachunga ipasavyo;
- Kuwasiliana na wazazi wa wanafunzi wenye matatizo maalumu ili kusaidiana katika kupata suluhisho kwa matatizo yao;
- Kuzingatia matatizo ya kila mwanafunzi, kumtega sikio na kuelewa mahitaji yake;
- Kushirikiana na viongozi wa shule na wazazi katika kuweka mikakati thabiti ili lugha ya kufundishia isije ikawa kizuizi kwa masomo yao;

- Kutowasimanga na kutowakashifu wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama vile wale wanaotoka katika familia fukara, wale wenye matatizo ya kielimu, wale wanaoandika kwa kutumia mkono wa kushoto, wale wasiosema vizuri na kadhalika;
- Kuwa mwenye wingi wa huruma na kujua kwamba ulemavu wao au matatizo yao yanajitokeza kwa ghafla na hayatokani na utashi wao au matendo yao;

## SHUGHULI ZA UFUNDISHAJI

Katika kuandaa somo lako, unapaswa kwanza kusoma shughuli zifuatazo zilizotumiwa katika Mwongozo wa Mwalimu huu, kuchagua zile zilizotumiwa katika somo husika katika Kitabu cha Mwanafunzi na kufuata maagizo ambayo yametolewa kwa kila shughuli. Shughuli hizo ni hizi zifuatazo:

### 1. Kutafakari picha

- Fuata maagizo yaliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi kama vile kuwaweka wanafunzi katika jozi au makundi mengine, kumpa mwanafunzi peke yake nafasi ya kujibu na kadhalika;
- Tilia mkazo mwenendo mwema na maadili katika jozi au makundi hayo;
- Waambie wanafunzi waitafakari picha iliyotumiwa;
- Wape wanafunzi dakika za kutosha za kuitafakari picha husika;
- Waulize wanafunzi wanachokiona kwenye picha iliyotumiwa;
- Waache wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha iliyotumiwa;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

### 2. Kusikiliza

- Waambie wanafunzi wasikilize kwa makini maoni ya wenzao kuhusu picha;
- Baada ya kutoa maoni yao, tambulisha somo husika la leo (kichwa cha somo);

- Waambie wanafunzi wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

**3. Kusoma**

- Waambie wanafunzi wasome kifungu cha habari kilichotolewa zaidi ya mara moja;
- Ongoza wanafunzi katika kusoma kifungu cha habari kilichotolewa;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

**4. Msamiati**

- Waongoze wanafunzi katika matumizi ya Kamusi ya Kiswahili Sanifu;
- Waongoze wanafunzi katika kufanya kazi zilizopangwa kuhusu msamiati lakini wazifanye kazi zote peke yao;
- Sahihisha hadharani kazi zote zilizofanywa na wanafunzi. (Linganisha majibu yao na yale ambayo yametolewa hapa chini katika sehemu iliyoitwa “Kusahihisha kazi mbalimbali”);
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

**5. Maswali ya ufahamu**

- Waongoze wanafunzi katika kujibu maswali lakini wayajibu peke yao;
- Sahihisha hadharani kazi zote zilizofanywa na wanafunzi. (Linganisha majibu yao na yale ambayo yametolewa hapa chini katika sehemu iliyoitwa “Kusahihisha kazi mbalimbali”);
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

6. **Kuzungumza**

- Baada ya kukisoma kifungu cha habari, wanafunzi wahusishe yaliyomo na ujumbe unaotolewa na picha ile;
- Mwambie mwanafunzi mmoja asimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzake yale ambayo ameyasoma;
- Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi yaliyopangwa kuhusu kuzungumza;
- Sahihisha hadharani kazi zote zilizofanywa na wanafunzi. (Linganisha majibu yao na yale ambayo yametolewa hapa chini katika sehemu iliyoitwa “Kusahihisha kazi mbalimbali”);
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

7. **Sarufi na matumizi ya lugha**

- Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi yaliyopangwa kuhusu sarufi na matumizi ya lugha;
- Waongoze wanafunzi katika kusoma maelezo yaliyotolewa kuhusu sarufi na matumizi ya lugha;
- Waongoze wanafunzi katika kulinganisha majibu yao na yale ambayo yametolewa hapa chini katika sehemu iliyoitwa “Kusahihisha kazi mbalimbali”);
- Sahihisha hadharani kazi zote zilizofanywa na wanafunzi ili wasahihishe makosa ambayo wamefanya;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

8. **Kuandika, kuchambua na kutafsiri**

- Waongoze wanafunzi katika kufanya kazi za kuandika, kuchambua au kutafsiri lakini wazifanye kazi zote peke yao;
- Sahihisha hadharani kazi zote zilizofanywa na wanafunzi. (Linganisha majibu yao na yale ambayo yametolewa hapa chini katika sehemu iliyoitwa “Kusahihisha kazi mbalimbali”);
- Pendekeza kazi ya utungaji (kuhusu mada iliyotolewa) ifanyiwe mara nyingi nyumbani;

- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

**9. Cheka kidogo**

- Waambie wanafunzi wasome kichekesho kilichotolewa;
- Waambie watafute vicheko vingine katika Kiswahili.

**10. Michezo**

- Waambie wanafunzi wasome mchezo uliotolewa na kutoa majibu;
- Ongoza wanafunzi katika kutoa majibu lakini wafanye kazi hiyo peke yao;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

**11. Utafiti**

- Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi lakini wazifanye kazi zote peke yao.
- Sahihisha hadharani mazoezi yote ili wanafunzi waweze kujua ni makosa gani ambayo wameyafanya;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa;
- Pendekeza kazi ya utafiti ifanyiwe mara nyingi nyumbani au mahali pengine maalumu.

**12. Tathmini kuhusu sura**

- Hii ni kazi ya kupima maarifa, ufahamu na stadi ambazo mwanafunzi amepata kutokana na yale aliyojifunza katika sura husika;
- Sahihisha hadharani mazoezi yote ili wanafunzi waweze kujua ni makosa gani ambayo wameyafanya;
- Kumbuka kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

# MUHULA WA KWANZA

# SURA YA 1:
## NADHARIA YA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI NA TANZU ZAKE

Sura hii inajumuisha vipengele nane vinavyohusiana na tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na kipengele cha mwisho kinachohusu aina za sentensi za Kiswahili. Kipengele cha kwanza kinahusu maana ya fasihi ya Kiswahili. Kipengele cha pili kinashughulikia udhamini wa kazi za sanaa za fasihi simulizi. Vipengele vinavyofuata mpaka kipengele cha nane vinaainisha na kubainisha tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kueleza dhima yake katika jamii.

Kila kipengele kinaundwa na masomo mbalimbali ambayo yanapaswa kuandaliwa vizuri ili kufundishwa vema. Huu ufuatao ni mfano wa maandalio ya somo:

### MAANDALIO YA SOMO

Katika kazi yako, unashauriwa kuandaa somo lako ili lengo la ufundishaji na ujifunzaji lifikiwe. Jambo hili litafanyika kwa kila somo. Katika Mwongozo huu wa Mwalimu, umetolewa mfano mmoja wa maandalio ya somo na wewe mwalimu utaandaa masomo mengine kwa kuiga mfano huu na kuuhusisha na yaliyomo katika masomo hayo yaliyopangwa kwa sura hii. Mfano wa maandalio ya masomo ni huu ufuatao:

| MAANDALIO YA SOMO | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Muhula wa | | | | Jina la mwalimu: | | | |
| Muhula wa | Tarehe | Somo | Kidato cha | Sura ya | Somo la | Muda | Idadi ya wanafunzi |
| | 18/01/2016 | Kiswahili | Tano | Kwanza | 1 kwa 9 | Dakika 80 | 30 |
| Makundi ya wanafunzi wenye matatizo ya kielimu na idadi yao:<br>1. Wanafunzi wenye matatizo ya kusikia: 2<br>2. Wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu: 4 | | | | | | | |
| Mada kuu: | Uwanja wa fasihi kama sanaa | | | | | | |
| Mada ndogo: | Nadharia ya fasihi simulizi ya Kiswahili na tanzu zake | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika mada: | Mwishoni mwa sura hii, mwanafunzi ataweza:<br>• Kufafanua tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | | | | | | |
| Kichwa cha somo | Maana ya fasihi ya Kiswahili | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika somo | Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi ataweza:<br>• Kuelewa na kuweza kuelezea fasihi ya Kiswahili | | | | | | |
| Mahali pa kufundishia | Darasani | | | | | | |

| | |
|---|---|
| Malengo ya kujifunza (Ni lazima yazingatie mahitaji ya wanafunzi) | Maarifa na ufahamu:<br>- Kueleza fasihi ya Kiswahili na udhamini wa kazi za kifasihi ;<br>- Kutambua na kuzieleza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili (semi, masimulizi, ushairi, mazungumzo);<br>- Kujadili mchango wa fasihi ya Kiswahili na jamii;<br>- Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili.<br>Stadi:<br>- Kufafanua kwa kina tanzu na vipera vya fasihi simulizi ya Kiswahili.<br>- Kuzipangilia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili katika makundi yake;<br>- Kutumia methali na nahau za Kiswahili kwa kuzihusisha na maisha ya kila siku;<br>- Kusimulia hadithi au shairi darasani;<br>- Kuchambua sentensi za Kiswahili kutokana na aina zake.<br><br>Maadili na mwenendo:<br>- Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. |
| Vifaa vitakavyotumiwa | Vitabu vya fasihi, tanzu za fasihi zilizorikodiwa, mchoro wa sanaa na matawi yake, matini na majarida yanayoelezea mwanzo na maendeleo ya fasihi, mtandao wa intaneti, ubao, chaki, kalamu na kifutio |
| Vitabu vitakavyotumiwa | Kitabu cha Mwanafunzi<br>Mwongozo wa Mwalimu<br>Vitabu vingine vinavyohusu fasihi ya Kiswahili |

| Muda na hatua | Mbinu za kufundishia na kujifunzia<br><br>Kwa kupitia kazi za kutafakari picha, kusikiliza, kusoma, kuzungumza, kujadili na kuandika katika makundi au jozi au kwa mwanafunzi peke yake au michezo, wanafunzi wataweza kuelewa vizuri fasihi ya Kiswahili, kusoma kazi mbalimbali za fasihi na kuwaambia wengine yale ambayo ameyasoma. | | Maarifa pamoja na Masuala mtambuka |
|---|---|---|---|
| | Wajibu wa mwalimu | Wajibu wa mwanafunzi | |
| Utangulizi<br><br>[Dakika 8=10%] | -Fuata maagizo yaliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi kama vile kuwaweka wanafunzi katika jozi au makundi mengine, kumpa mwanafunzi peke yake nafasi ya kujibu na kadhalika;v<br>-Waache wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha iliyotumiwa;<br>-Wape wanafunzi dakika za kutosha za kuitafakari picha husika;<br>-Waulize wanafunzi wanachokiona kwenye picha iliyotumiwa.<br>-Waongoze katika kutoa maoni yao;<br>-Baada ya kutoa maoni yao, tambulisha somo husika la leo ambalo ni "Mazingira ya hospitali, vifaa na wafanyakazi". | -Wafuate maagizo yaliyotolewa katika Kitabu chao kama vile kujigawa katika jozi au makundi mengine, kila mwanafunzi kujibu maswali peke yake na kadhalika;<br>-Waitafakari picha kwa makini;<br>-Watoe maoni yao kwa sauti kuhusu picha iliyotumiwa. | Maarifa:<br>- Kueleza fasihi ya Kiswahili; Kutambua na kuzieleza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili (semi, masimulizi, ushairi, mazungumzo); Kujadili mchango wa fasihi ya Kiswahili na jamii; Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili<br><br>Stadi:<br>- Kufafanua kwa kina tanzu na vipera vya fasihi simulizi ya Kiswahili; Kuzipangilia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili katika makundi yake; Kutumia methali na nahau za Kiswahili kwa kuzihusisha na maisha ya kila siku; Kusimulia hadithi au shairi darasani; Kuchambua sentensi za Kiswahili kutokana na aina zake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Upeo<br><br>[Dakika 60=75%] | -Waambie wanafunzi wengine wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Baada ya kukisoma kifungu cha habari, wanafunzi wahusishe yaliyomo na ujumbe unaotolewa na picha ile;<br>-Mwambie mwanafunzi mmoja asimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzake yale ambayo ameyasoma.<br>-Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi yaliyopangwa na kutoa majibu yao;<br>-Jadiliana na wanafunzi kuhusu majibu yao au matokeo ya kazi wanazozifanya. | -Wasome kifungu cha habari kwa sauti;<br>-Wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Waige matamshi sahihi ya maneno mbalimbali na kiimbo kinachofaa;<br>-Wahusishe yaliyomo katika kifungu cha habari na ujumbe wa picha iliyotolewa;<br>-Wasimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzao yale ambayo wameyasoma;<br>-Wafanye kazi mbalimbali zilizopangwa;<br>-Wajadiliane na wenzao kuhusu majibu ambayo wameyapata au matokeo ya kazi ambazo wamefanya na kuyalinganisha majibu yote yaliyotolewa. | Maadili na mwenendo mwema:<br>- Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii;<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii.<br><br>Masuala mtambuka yanayoshughulikiwa:<br><br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (Kuishi kwa amani na kuendeleza jamii)<br>-Usawa wa jinsia;<br>-Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari;<br>-Elimu isiyo na ubaguzi |
| Mwisho<br><br>[Dakika 12=15%] | -Waongoze wanafunzi katika kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Waachie wanafunzi kazi ya nyumbani | - Kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Washiriki katika zoezi ambalo limetolewa;<br>-Waandike katika daftari zao kazi ya nyumbani ambayo imetolewa na mwalimu. | |

| | |
|---|---|
| Tathmini ya mwalimu | Kutokana na maoni yake kuhusu jinsi wanafunzi walivyoshiriki katika somo lake, mwalimu achunguze jambo la kutilia mkazo hususan pale ambapo wanafunzi wamekutana na matatizo mbalimbali |

Licha ya mfano huo wa maandalio ya masomo, kila somo lina mwongozo wake. Isome miongozo hiyo ili kujua yanayopendekezwa katika kila somo.

# SOMO LA 1:

## FASIHI YA KISWAHILI NI NINI?

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kwanza. Mambo mengine yametolewa katika sehemu za hapo juu.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuelezea fasihi ya Kiswahili;<br>- kujadili mchango wa fasihi katika Kiswahili na jamii. |
| **Vipindi:** | 7 |
| **Shughuli:** | - Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; kucheka, -Utafiti |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
|---|---|---|
| Kufafanua tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | - Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii | - Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (Kuishi kwa amani na kuendeleza jamii)<br>- Usawa wa jinsia;<br>- Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari;<br>- Elimu isiyo na ubaguzi |
| | | |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Tunamwona mwalimu darasani pamoja na wanafunzi wake. Anafundisha mambo yanayohusu nadharia ya fasihi ya Kiswahili.

Kazi ya 2:

Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi inayomwongoza mtafiti au mtaalamu. Nadharia husaidia katika kulielezea vema jambo fulani. Jambo moja linaweza kuelezwa kwa namna tofauti kwa kuongozwa na nadharia tofauti.

Kazi ya 3:

**Madokezo:**
Katika kifungu cha habari, fasili ya nadharia za fasihi ya Kiswahili imetolewa. Na picha inahusu mambo ya fasihi hasa nadharia ya fasihi ya Kiswahili.

### A. Maswali ya Ufahamu

Kazi ya 4:

1. Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi inayomwongoza mtafiti au mtaalamu na ambayo husaidia katika kulielezea vema jambo fulani kwa mtazamo imara zaidi kuliko mtazamo mwingine.
2. Hapana. Sihiri si chanzo cha fasihi bali ni sehemu ya mila na desturi za jamii nyingi duniani.
3. Fasihi katika jamii inaweza:
   - Kuburudisha, kufurahisha na kuchangamsha jamii;
   - Kuelimisha jamii;
   - Kuionya jamii na kuipa mwelekeo;
   - Kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii;
   - Kuunganisha jamii na vizazi;
   - Kukuza na kuendeleza kipawa cha lugha;
   - Kukuza uwezo wa kufikiri.

4. Hapana. “Fasihi simulizi ya Kiswahili ilikuwepo kabla ya majilio ya wageni sehemu za pwani ya Bahari ya Hindi”. Mahali hapo panajulikana kama makazi ya Waswahili. Hili linatokana na kuwa ukuwepo wa kila fasihi unakwenda sambamba na ukuwepo au uundaji wa jamii husika ya watu.
5. Hata “siku za leo, tunaweza kuwapata watu wanaotunga kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili”. Wapo watu mbalimbali wanaoendelea kubuni kazi zao za kifasihi kwa njia ya masimulizi. Ndiyo sababu tunaweza kuipata fasihi simulizi ya kale na fasihi simulizi ya kisasa.
6. Eleza kidogo nadharia za ubadilikaji taratibu, msambao na nadharia ya kisosholojia.

   Ubadilikaji taratibu: Nadharia hii iliasisiwa na Charles Darwin (ndiye mwasisi wake) ambaye alikuwa mwana baiolojia karne ya 19. Katika utafiti wake kuhusu viumbe hai walioishi miaka mamilioni iliyopita, Darwin aligundua kuwa iliwezekana tu viumbe hai kuendelea kuishi kwa sababu ya kumudu mapambano dhidi ya uhaba wa vyakula. Hivyo, Darwin alilitaja jambo hili kama “Uhai kwa wanaofaa”. Aligundua pia kuwa viumbe hai waliendelea kuishi kwa sababu ya maumbo yao na mazingira yaliyosababisha wao kuwepo.

   Wanamabadiliko wanaamini kuwa viumbe hai wote tulitokea kwenye asili moja; hivyo tuna uwezo wa akili sawa na kimaendeleo tutakuwa sawa. Pia wanaamini kuwa kuna misingi sawa kuhusu kanuni zinazoongoza asili na maendeleo ya utamaduni wa mwanadamu. Waliona kwamba misingi mikuu ya dhana ya ubadilikaji taratibu ni “viumbe hai” kwa sababu viumbe hai wote wanakuwa katika mchakato wa mabadiliko mbalimbali hadi kufikia kwenye maumbo yao ya sasa.
   Na fasihi simulizi ilipitia michakato mingi ya mabadiliko mpaka kufikia katika umbo lake la sasa. Kwa hiyo, kazi za fasihi simulizi tulizo nazo leo zina asili moja isipokuwa zilikuwa zikibadilika kutokana na mabadiliko ya wakati. Kwa maoni yao, chimbuko la fasihi simulizi ni jamii yenyewe na kutokea kwa kufanana kwa kazi za fasihi simulizi kutoka jamii moja hadi nyingine kunasababishwa na hatua sawa za mabadiliko kiakili na kijamii kwani ni jamii moja iliyozagaa ulimwenguni kote na akili zao ni sawa. Hivyo, kutokana na maoni ya wanamabadiliko hawa,

fasihi simulizi ya kiafrika hubadilika kutoka kipindi kimoja hadikingine kutokana na mabadiliko ya kijamii.

-Msambao: Waasisi wa nadharia hii niJacob na Wilhem Grimm. Baadaye mawazo yao yaliendelezwa na Maxmuller na Mmarekani Stere Thomson. Licha ya tofauti ndogondogo, wataalamu wa nadharia hii wanaamini kwamba chimbuko la fasihi simulizi ni moja lakini kutokana na maingiliano ya kijamii, fasihi simulizi ilisambaa hasa kutoka jamii zilizostaarabika (Ulaya) kuja katika jamii zisizostaarabika (Afrika). Baadhi yao walisema kuwa hadithi simulizi zilisambazwa na makundi ya wahamiaji kutoka India na kufika huko Magharibi kwa njia ya msambao.

Kwa wanamsambao, utamaduni unaweza kusambaa kutoka katika jamii imara na maarufu tena yenye nguvu kuelekea katika jamii iliyo dhaifu. Hivyo basi, kutokana na mawazo ya wanamsambao fasihi simulizi ya kiafrika ilisambaa kutoka sehemu moja iliyostaarabika yaani Ulaya kwenda sehemu nyingine ambayo haijastaarabika yaani Afrika.

-Nadharia ya kisosholojia: Nadharia hii ina mihimili mitatu yaani umahususi, mkazo katika utendaji na dhima ya fasihi simulizi katika jamii. Umahususi unahusu kujikita zaidi katika jamii peke yake badala ya kujikita katika taaluma ya sanaa jadi kwa ujumla. Katika mhimili wa utendaji, wanasosholojia walisisitizia kuchunguza utendaji wa kazi mbalimbali za fasihi simulizi. Ni kusema kuwa fanani wa kazi ya fasihi simulizi ana ujuzi na ustadi wa kiutendaji katika sanaa husika.

Kwa wanasosholojia, ili kujua fasihi simulizi ya kiafrika ni vizuri kuangalia jamii na utendaji wa kazi husika. Katika msisitizo juu ya dhima ya fasihi simulizi katika jamii, wanasosholojia wanaamini kuwa ukamilifu wa fasihi simulizi uko hai na hauwezi kufa na kwamba unabadilika kulingana na maendeleo ya jamii husika.

Hivyo, kutokana na maoni ya wanasosholojia,ili kuelewa historia ya fasihi simulizi mtu anapaswa kuangalia jamii husika, utendaji na dhima ya fasihi katika jamii husika kwani mihimili hii ndiyo chanzo au historia ya fasihi simulizi

ya jamii husika. Kutokana na maoni hayo, asili ya fasihi simulizi ya kiafrika ni ndani ya jamii za kiafrika zenyewe na si mahali pengine.

-Nadharia ya utaifa: Waasisi wake ni kama vile S. Adeboye, Babalola, daniel P. Kunene na J.P. Clark. Nadharia hii ilizuka katika vuguvugu la kudai uhuru barani Afrika. Wanautaifa wanasema kuwa wananadharia hao wote wa kiutandawazi hawakuelewa vizuri lugha za kiafrika. Wao waliathiriwa kwa kiwango kikubwa na dhana za kikoloni na upendeleo wa kibepari kuwa Afrika ni bara la giza na washenzi wasio na ustaarabu wowote na wanaostahili kustaarabishwa na wazungu kupitia mlango wa ukoloni.

Wanautaifa wanaamini kuwa chimbuko la fasihi simulizi ya kiafrika inapatikana ndani ya jamii ya kiafrika na ili kuchunguza fasihi ya jamii husika, sharti wataalamu na wanazuoni wa jamii hiyo wahusishwe.

Nadharia hulutishi: Nadharia hii iliasisiwa na wanazuoni wa kiafrika kama vile M.M. Mlokozi, johnson na Ngugi wa Thiong'o. Mtazamo wao ni kwamba fasihi ya kigeni na ya kijadi ziliathiriana na kuingiliana. Ni kusema kuwa wageni walichangia katika kukuza taaluma ya fasihi simulizi ya kiafrika. Hivyo basi, historia ya fasihi simulizi ya kiafrika inaweza kujadiliwa kwa kuhusisha au kuchanganya mawazo ya wataalamu wote wa kigeni na wa kijadi.

7. "Fasihi kwa Kiswahili" ni ile inayoundwa na kazi zote za kifasihi zisizo za Waswahili lakini zilizotungwa au zilizotafsiriwa katika Kiswahili. Hili linatokana na kuwa ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima:

-izungumzie utamaduni wa Waswahili;
-na itungwe katika Kiswahili.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 5:

Kila mwanafunzi asikilize jinsi wanafunzi wenzake wanavyosoma kifungu cha habari na kuheshimu alama za uakifishaji.

**C. Kusoma**

Kazi ya 6:

1. Fasihi, kama dhana, ilielezwa na wataalamu wengi kwa kuegemea nadharia na mitazamo mbalimbali.
2. Nadharia ya kiutandawazi) imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni ubadilikaji taratibu, msambao na nadharia ya kisosholojia).
3. Inaundwa na kazi za sanaa zinazowasilisha ujumbe fulani kwa hadhira inayokusudiwa.
4. Fasihi inaweza kuburudisha, kufurahisha na kuchangamsha jamii.
5. Waswahili walikuwa na eneo lao, jadi zao, vyakula vyao tofauti na vile vinavyopendelewa na Wakongo.
6. Kazi za sanaa za fasihi ya Kinyarwanda au ya Kirundi au ya Kiingereza zikiandikwa kwa Kiswahili huitwa kazi za fasihi kwa Kiswahili.

Kazi ya 7:

Simama mbele ya darasa na kukamilisha sentensi zifuatazo mwanzoni, katikati au mwishoni kama zilivyotumiwa katika habari:

1. Wajamaika walioko Uingereza kwa miaka na karne nyingi hawajakubalika kuwa ni Waingereza.
2. Fasihi ya Kiswahili inaundwa na nyanja kuu mbili yaani fasihi simulizi ambayo ni ya kale na fasihi andishi ambayo ni changa.
3. Nadharia husaidia katika kulielezea vema jambo fulani kwa mtazamo imara zaidi kuliko mtazamo mwingine.

Kazi ya 8:

Ni hadithi simulizi ya hurafa.

**D. Msamiati**

Kazi ya 9:

Chanya: -enye kuleta matumaini
Utandawazi: Upanuakaji kwa kina kirefu wa mahusiano miongoni mwa jamii mbalimbali ili dunia iwe kijiji kidogo.
Kuhuluti (sha): Kuweka vitu mahali pamoja; kuchanganya
Hadhi: Cheo cha mtu
Ufisadi: Maovu; uharibifu
Taadhima: Heshima; utukufu; unyenyekevu
Jadi: Asili ya mtu anakotoka; ukoo au kizazi cha mtu
Kedi: Mambo yasiyopendeza; mambo ya kinyumenyume; hila

Kazi ya 10:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 11:

1. Nadharia;
2. Mtazamo;
3. Ubishi;
4. Kipawa.

Kazi ya 12:

1. Nadharia ya kiutandawazi ni mojawapo kati ya nadharia zinazohusu kueleza chanzo, ukuaji na ueneaji wa fasihi simulizi.
2. Serikali ya Rwanda imeanza kuhamasisha hadhira husika kuhusu amani na maendeleo ya kudumu.

3. Ufasaha wa lugha huwasaidia viongozi mbalimbali kuaminiwa na raia kuhusu mikakati iliyochukiliwa na serikali zao.
4. Ufukara unaendelea kupigwa marufuku nchini Rwanda kutokana na sera thabiti za serikali.

Kazi ya 13:

1. Fasihi ni kongwe ndani ya kila jamii ya watu.
2. Kazi zote za fasihi ya Kirundi zilizotafsiriwa katika Kiswahili si za fasihi ya Kiswahili.
3. Uamuzi wa serikali yetu wa kutilia mkazo lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari unatokana na umuhimu

Kazi ya 14:

| **1. Binadamu** | **2. Lugha** | **3. Mengine** |
|---|---|---|
| Mwanafunzi<br>Mwanafasihi<br>Mnyonge | Kirundi<br>Kimashomvi<br>Kiingereza<br>Kimanyema | Ndoto<br>Kiroboto<br>Ulimwengu |

Kazi ya 15:

| **Sanaa** | **Wenzo (au kitu kinachorahisisha kazi)** |
|---|---|
| 1. Fasihi | Lugha |
| 2. Uchoraji | Rangi |
| 3. Uimbaji | Lahani |
| 4. Ufumaji / udarizi | Nyuzi |
| 5. Ufinyanzi | Udongo |
| 6. Uchongaji | Miti/mawe |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 16:

Kila mwanafunzi apewe fursa ya kusimama mbele ya darasa na kuwaambia wenzake aliyoyasoma.

Kazi ya 17:

-amali na desturi;
-uzazi wa mpango au kuboresha uzazi;
-tatizo la kisiasa;
-dini ya kijadi;
-maadili bora na kadhalika.

Kazi ya 18:

Fasihi inajitokeza kama:
-chombo cha kukuza lugha;
-chombo cha kuburudisha, kufurahisha na kuchangamsha jamii;
-chombo cha kuelimisha jamii;
-chombo cha kuonya jamii na kuipa mwelekeo;
-chombo cha kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii;
-chombo cha kuunganisha jamii na vizazi;
-chombo cha kukuza uwezo wa kufikiri.

Kazi ya 19:

Kuna uhusiano kati ya fasihi simulizi ya Kiswahili na maandishi yaonekanayo kwenye picha hii kwa sababu fasihi simulizi ya Kiswahili ni uwanja mmoja kati ya nyanja kuu mbili zinazoiunda fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Uwanja mwingine ni fasihi andishi.

**F. Utafiti**

Kazi ya 20:

Licha ya biriani na kuku wa kupaka, vyakula vingine vilivyokuwa vikipendelewa na jamii ya Waswahili na wakazi wengine wa mwambao katika enzi za kikoloni ni kama vile:
-Mseto;
-Samaki wa kupaka;
-Haluwa;

-Mkate wa sinia;
-Vitumbua;
-Mahamri.

**G. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 21:

Kila mwanafunzi atatoa kichekesho chake.

**H. Kuandika**

Kazi ya 22:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 23:

-Ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima izungumzie utamaduni wa Waswahili.
-Ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima itungwe katika Kiswahili.
-Mtu anaposikiliza au kusoma kazi ya fasihi anapata ujuzi wa lugha unaotokana na vipengele imara mbalimbali vya fasihi.

Kazi ya 24:

Fasihi hutumia lugha kufikisha ujumbe wake kwa:
- Jamii;
- Wasikilizaji;
- Wasomaji;
- Hadhira;
- Binadamu,...

Kazi ya 25:

[Ndugu mpenzi,
Sijasikia mkono ukipewa shukrani na mguu kwa kuutoa mwiba. Lakini ni ujinga

wa mguu kufikiria unastahili kutolewa mwiba, maana kuna miili isiyo na mikono. Na miguu hiyo ichomwapo na miiba hutaabika sana. Hivyo, sioni kustahili kwangu bali ni rehema na neema za Mola kuwa na ndugu. Nami nimepata na kujifunza zaidi upendo wako.
Mungu akubaliki! ].

Kazi ya 26:

Matini hii si ya kifasihi kwani:
-haitumii lugha mahususi, yenye mvuto na mguso wa kusisimua kama ile ya kifasihi;
-haitawaliwi na kaida na masharti ya kisanaa, ni kusema kuwa maneno hayakupangwa kisanaa,...

## SOMO LA 2:
## UDHAMINI WA KAZI ZA SANAA ZA FASIHI SIMULIZI

### A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la pili.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuelezea udhamini wa kazi za kifasihi</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">7</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">- Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| Kufafanua udhamini wa kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili katika kuiendeleza jamii au nchi | - Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | - Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu<br>- Mafunzo kuhusu amani na maendeleo<br>- Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

-Kuna watu wawili: Mdhamini na mtafiti;
-Mdhamini anamwagiza mtafiti kufanya kazi kulingana na itikadi yake;-
-Mtafiti anafikiri kuwa atakapofanya utafiti wake namna hiyo, atakuwa kama karagosi wa mdhamini wake. Lakini kitu cha lazima kwake ni kumpa pesa.

Kazi ya 2:

Wanazungumzia kuhusu udhamini atakaoupata mtafiti kutoka kwa tajiri (au bosi) mdhamini.

Kazi ya 3:

Maana ya karagosi: Kwa kawaida, karagosi ni mtoto wa bandia anayening'inizwa kwenye uzi ambao ukivutwa mtoto huyo hucheza ili kuchekesha watazamaji. Lakini hapa, kikaragosi ni mtu anayetumiwa na bosi wake au tajiri kwa faida ya bosi au tajiri huyo.
Ubaya wa kuwa karagosi wa mdhamini: Matokeo ya utafiti huathiriwa sana na fikra na malengo ya mdhamini, hakuna kuweko kwa uhuru wa mtafiti katika kazi yake, ujuzi wa mtafiti hupuuzishwa,...

Kazi ya 4:

Kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu athari za udhamini katika fasihi simulizi. Na picha hii inatuonyesha watu wawili ambao ni mdhamini na mtafiti. Mtafiti yuko kazini na mdhamini anamkumbusha kufanya kazi kulingana na itikadi yake. Kwa hiyo, picha hiyo ina uhusiano na yaliyomo katika kifungu cha habari.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 5:

1. Udhamini humwezesha mtafiti kuwa na uuwezo wa kifedha ili kuendeleza kazi yake ipaswavyo. Ijulikane kuwa ili utafiti uendelezwe vizuri na kufikia lengo lake, ni lazima kuwa na uwezo wa kifedha. Pesa hizo ndizo zinazomsaidia mtafiti katika kufika mahali fulani, kununua vifaa muhimu atakavyotumia katika kazi yake na kadhalika.

2. Utafiti katika fasihi simulizi unalenga mambo yafuatayo :

   -Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa.
   -Kuongeza hazina ya maarifa katika uwanja unaohusika;
   -Kupima hali, fikra, mitazamo, na matarajio ya jamii ya watafitiwa;
   -Kuchangia katika kujenga na kuendeleza fani za fasihi simulizi na fani nyinginezo.

3. Ni kweli kwamba «kazi ya utafiti hudai ushirikiano wa watu mbalimbali». Watu hao ni kama vile :

   **Mtafitiwa:** Ni upande wa mtu au watu wanaochunguzwa. Ndiye anayemiliki data zinazotakiwa na walio katika mazingira maalum ya kijamii na kijiografia. Mazingira haya ndiyo mandhari ya fasihi simulizi husika. Wajibu wake ni kutoa taarifa, kujenga uhusiano na mtafiti na kuchagua taarifa za kumpa mtafiti;

   **Mtafiti:** Ndiye mtaalamu ambaye, pamoja na wasaidizi wake, anashughulikia ukusanyaji wa data na habari zozote zinazotakiwa katika uwanja huo.

Baada ya kuzipata data hizo, mtafiti huzilinganisha, huzichambua, hizifasili, huzitathmini, na kuzijumuisha. Kazi hizi zinamsaidia ili kupata matokeo kamili ya utafiti wake;

**Mdhamini:** Ndiye anayetoa fedha za kugharamia utafiti. Pesa hizo ndizo zinazomsaidia mtafiti katika kufikia shabaha yake. Mdhamini ndiye anayeweka malengo ya kiujumla ya utafiti na kupokea matokeo yake.

4. Upande wa watafitiwa unalazimishwa kutoa taarifa, kujenga uhusiano na mtafiti na kuchagua taarifa za kumpa mtafiti ili kitendo cha utafiti kiweze kufaulu.

5. "Uhuru na hiari mtafiti aliyo nayo ni ile tu anayopewa na mdhamini wake". Ingekuwa vizuri mtafiti awe na uhuru katika kazi yake lakini kazi yake hutegemea msaada wa mdhamini wake. Mdhamini ndiye anayeainisha nyanja za kufanyia utafiti, aula za utafiti na watafiti wenyewe. Ndiye anayetoa fedha na nyenzo za utafiti na kupokea matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, mtafiti analazimishwa kuwa karagosi wa mdhamini.

6. Matokeo ya utafiti katika fasihi simulizi huathiriwa na udhamini kwa sababu :

-Kwa kawaida, mambo yanayochunguzwa ni yale tu yanayotakiwa, yanayohitajiwa au yanayokubaliwa na mdhamini;

-Mapana ya utafiti kidata, kijiografia na kimaudhui huamuliwa na mdhamini na hutegemea mahitaji yake na kiasi cha pesa anachotoa. Ni kusema kuwa, akiwa na uwezo mkubwa wa kifedha au mahitaji ya kushughulikia jambo fulani, anaweza kupanua kabisa uwanja wa utafiti kwa mtafiti wake.

-Mara nyingi, fasiri na ufafanuzi rasmi wa data hubidi ulingane na mtazamo

wa kiitikadi wa mdhamini. Ni sharti mambo yalingane na imani yake.

-Mara nyingi, matokeo ya utafiti ni mali ya mdhamini. Ni kusema kuwa hutumiwa naye ili kuendeleza masilahi na malengo yake.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 6:

Kila mwanafunzi apewe fursa ya kusikiliza mwenzake na matamshi bora yatiliwe maanani.

**C. Kusoma**

Kazi ya 7:

Mwanafunzi asome kifungu cha habari kwa kufuata malamshi bora na alama za uakifishaji.

Kazi ya 8:

Katika kutegemea udhamini wa bosi au tajiri na kufanya kazi kulingana na itikadi yake, mtafiti hulazimishwa kufunga macho na kunyamaza kuhusu mambo mbalimbali yatokanayo na uvumbuzi wake. Ni kusema kuwa hulazimishwa kuwa kipofu na bubu kuhusu mambo hayo.

Kazi ya 9:

1. Baada ya kuzipata data hizo, mtafiti huzilinganisha, huzichambua, huzifasili, huzitathmini, na kuzijumuisha.
2. Ingekuwa lazima atumie fursa yoyote kwa kutetea ukweli wa kisayansi dhidi ya uongo wa baadhi ya wadhamini.
3. Ni kusema kuwa, mtafiti atajikuta akifanya utafiti ili kuendeleza na kutekeleza malengo na masilahi ya wengine.
4. Uchambuzi ndio unaowawezesha wanafasihi kuhakikisha kuwa kazi fulani ni ya kifasihi au la.

Kazi ya 10:

Kusoma kwa kuzingatia malamshi bora ndilo lengo la kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa lengo hili limefikiwa.

## D. Msamiati

Kazi ya 11:

**Data:** Taarifa au takwimu inayotumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani au mambo mbalimbali yaliyokusanywa katika kazi ya utafiti

**Aula:** Bora zaidi

Wenzo (nyenzo): Kitu kinachorahisisha kazi

**Itikadi:** Imani katika jambo la kidini na jinsi ya mapokezi yake; mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au za kiuchumi

**Jasiri:** Shujaa; hodari (Mfano: Mtu jasiri)

Kazi ya 12:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 13:

1. Mapana ya utafiti kidata, **kijiografia na kimaudhui** huamuliwa na mdhamini na hutegemea mahitaji yake na kiasi cha pesa anachotoa.
2. Mara nyingi, matokeo ya utafiti ni **mali** ya mdhamini.
3. Mtafiti analazimishwa kuwa **karagosi** wa mdhamini.

Kazi ya 14:

1. U**dha**mini;
2. **Da**ta;
3. **Su**ala;
4. Ku**gha**ramia;
5. Ma**si**lahi

Kazi ya 15:

| Watu wanaochangia katika kuendeleza utafiti | Mengine |
|---|---|
| Mdhamini<br>Mtafiti<br>Mtafitiwa | Data<br>Matokeo<br>Bakteria<br>Masilahi<br>Kijasumu<br>Mkariri<br>Maendeleo<br>Muflisi<br>Mkongwe |

Kazi ya 16:

1. Utunzi wa kazi za fasihi simulizi kuhusu malezi bora hufuata kanuni hizo.
2. Mtafiti anapaswa kuwa ***jasiri*** katika kazi yake ili asije akaathiriwa na mdhamini wake.

Kazi ya 17:

Tunamwona mwanafunzi ambaye amehitimu masomo yake ya chuo kikuu na kupewa shahada. Udhamini unawezaje kukufikisha kwenye kiwango kama hiki ikiwa huna fedha za kulipa ili kuendeleza masomo yako. Mtu asiye na uwezo wa kifedha hawezi kuendeleza masomo yake. Akipata udhamini kwa mtu au chuo fulani, ndipo anaweza kulipa fedha za shule na hata kusoma chuo kikuu na kupata shahada.

Kazi ya 18:

1. "Udhamini si udhahili": Udhamini ni msaada wa kifedha anaopewa mtafiti na mtu fulani mwenye uwezo ili kukidhi mahitaji fulani yanayohusu kazi hiyo ngumu ya ukusanyaji wa data. Udhahili nao ni ile hatua ya mtu kufanya maombi katika chuo kikuu husika na kutaka kusoma shahada fulani. "Udhamini si udhahili"

ni kusema kuwa mtu anaweza kukubaliwa msaada na mdhamini fulani na kutopewa udhahili kutokana na masharti ya chuo.

2. “Udhamini ni fadhila“: Ni kusema kuwa mdhahili kunatokana na hiari ya mtu. Kukubali kuwa mdhamini wako ni kama shukrani kwako.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 19:

Kila mwanafunzi atoe muhtasari wa yale ambayo ameyasoma.

Kazi ya 20:

| | |
|---|---|
| Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa | kama vile mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu |
| Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa | kama vile mafunzo kuhusu amani na maendeleo |
| | kama vile mafunzo kuhusu mauaji ya kuangamiza |

Kazi ya 21:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jambo | lolote | la | kisayansi | linadai | utafiti |
| Jambo | lolote | la | kidini | linadai | imani |

Kazi ya 22:

Wanafunzi wana uhuru wa kutoa maoni tofauti.

**F. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 23:

Kila mwanafunzi ana kichekesho chake.

**G. Utafiti**

Kazi ya 24:

**.Mambo yanayotawala ukusanyaji wa data katika utafiti ni:**

-Uwanja wa taaluma unaohusika

-Lengo/madhumuni ya utafiti

-Uwezo na nyenzo alizo nazo mtafiti

-Muda alio nao mtafiti

**.vya msingi katika utafiti:**

Vifaa hutegemea aina ya utafiti, lakini aghalabu baadhi ya vifaa hivi, kama si vyote, ni:

-Shajara ya uwandani

-Kalamu na karatasi za kuandikia kumbukumbu

-Tepurekoda au kinasasauti na vifaa vyake

-Video/kamrekoda na vifaa vyake

-Kamera na vifaa vyake

-Kompyuta na vikorokoro vyake

-Vidadisi (hojaji) na dodoso

-Vifaa vya kupimia/kuhesabia

-Darubini, vionambali, na kadhalika.

**Njia za utafiti**

-Mahojiano – faida na hasara zake;

-Kushuhudia – faida na hasara zake;

-Kushiriki – faida na hasara zake;

-Kutumia vidadisi/majedwali, n.k. – faida na hasara zake.

Njia hizi hutokana na aina za utafiti ambazo ni:

-Utafiti wa maktabani/ wa nyaraka

-Utafiti wa uwandani

-Utafiti wa maabarani/studioni

## H. Kuandika

Kazi ya 25:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

Kazi ya 26:

| |
|---|
| Mara nyingi, fasiri na ufafanuzi rasmi wa data hubidi ulingane na mtazamo wa kiitikadi wa mdhamini. |
| Katika utafiti wowote wa fasihi simulizi, zipo pande tofauti. Ni lazima pande hizo zisaidiane ili utafiti ulifikie lengo lake. |
| Mtafiti ndiye mtaalamu ambaye, pamoja na wasaidizi wake, anashughulikia ukusanyaji wa data na habari zozote zinazotakiwa katika uwanja huo. |

Kazi ya 27:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Wajibu | wa | mtafitiwa | ni | Kutoa taarifa. |
| Wajibu | wa | mtafitiwa | ni | kujenga uhusiano na mtafiti. |
| Wajibu | wa | mtafitiwa | ni | kuchagua taarifa za kumpa mtafiti. |

Kazi ya 28:

Kila kikundi kitoe mawazo yake.

# SOMO LA 3:

## TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI NA VIPERA VYAKE

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la tatu.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua, kufafanua kwa kina na kuzielezea tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na makundi yake makuu yaani semi, masimulizi, ushairi na mazungumzo</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">7</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti; -Michezo</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
<tr><td>Kufafanua tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake</td><td>- Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii.</td><td>- Mafunzo kuhusu uzalishajimali<br>- Mila na desturi, na kuzalisha kwa kiwango<br>- Mazingira na maendeleo ya kudumu</td></tr>
</table>

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Picha inayoonyesha funiko la kitabu ambapo paliandikwa “Methali na Nahau” na methali ya Kiswahili “Usiache mbachao kwa msala upitao”. Picha nyingine inaonyesha wasichana wanaopiga densi.

Kazi ya 2:

"Usiache mbachao kwa msala upitao." Maana yake ni usishtushwe na mambo mapya yenye mng'ao (au yanayomeremeta) wa muda mfupi bali chagua yale unayoyazoea yanayoweza kudumu.

Kazi ya 3:

Picha ya kwanza inahusu "methali" lakini picha ya pili inahusu utanzu wa "nyimbo".

Kazi ya 4:

Picha ya kwanza inahusu "methali" lakini picha ya pili inahusu utanzu wa "nyimbo". Tanzu hizo zote zimezungumziwa katika kifungu cha habari. Tena ni tanzu za fasihi simulizi.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 5:

1. Zitaje sifa bainifu tano za fasihi simulizi ya Kiswahili.

-Husambazwa kikalima;

-Huwa na hadhira mahususi iliyo hai;

-Huwasilishwa kwa wakati na mahali maalumu kama vile jioni baada ya kazi, katika sherehe na kadhalika;

-Huwa na mwanzo na mwisho maalumu wa kiada. Muundo wake ni rahisi kufuatika;

-Ni mali ya jamii kwani mtunzi hajulikani;

-Hubadilika kulingana na wakati hasa inapowasilishwa kupitia ufaraguzi;

-Huwa na wahusika wengi tofauti yaani wahusika wa aina mbalimbali. Msimulizi ndiye mhusika wa kati;

-Huwa na tanzu nyingi zenye vipera vingi;

-Hutungwa kila wakati na baadhi yake huzuka papo hapo;

-Hutumia sauti, mdomo na ishara za mwili. Kwa hiyo, si lazima fanani au hadhira wajue kusoma. Kiungo muhimu katika mapokezi ni masikio;

-Huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii;

-Huwa na uzuri unaotegemea ubingwa wa fanani;
-Ni kongwe kwani ilianza tu lugha ilipoanza.

2. "Jambo linalobabaisha leo ni upungufu wa idadi ya watu wanaoendelea kujivunia ubunifu wa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili". Chanzo cha jambo ni:

- Uvumbuzi wa maandishi: Katika enzi za kale, fasihi simulizi ndiyo iliyokuwa sanaa ya pekee ya lugha. Kupitia fasihi hii, vizazi viliweza kurithi kazi mbalimbali za vizazi vingine. Walakini, wanajamii walizipoteza kazi nyingi kutokana na njia hiyo ya masimulizi. Uvumbuzi wa maandishi ndio uliorahisisha kuhifadhi mila na tamaduni zao. Vilevile, kazi mbalimbali za fasihi simulizi zilihifadhiwa.
- Mfumo mpya wa elimu na maendeleo: Awali, watoto walikuwa wakijumuika kwenye moto nyakati za jioni ili kusimuliwa hadithi au vitendawili. Siku hizi,

wanajumuika kwenye kumbi na madarasa yanayoangaziwa kwa kutumia umeme. Wao wametekwa na vifaa vipya kama vile redio, runinga, vitabu na kadhalika. Mfumo huu mpya wa elimu hutilia pia mkazo masomo mengine huku fasihi simulizi ikipuuzwa. Elimu ya vitabu ndiyo inayoshughulikiwa mno kuliko ile ya mapokeo.
- Mwingiliano na mgusano wa jamii mbalimbali: Kule kuingiliana kwa jamii mbalimbali ulimwenguni kulipunguza uhalisia wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Vinyume vya mwingiliano huo ni kama vile kutoweza kujieleza kwa lugha moja, kutoweza kujigamba mbele ya hadhira na kadhalika. Kumeibuka jamii ya Waswahili yenye utamaduni mseto na lugha iliyopunguziwa nguvu zake.

3. Mfumo wa elimu mpya na maendeleo huchangia katika kupunguka kwa idadi ya kazi za fasihi simulizi kwa namna hii:

Awali, watoto walikuwa wakijumuika kwenye moto nyakati za jioni ili kusimuliwa hadithi au vitendawili. Siku hizi, wanajumuika kwenye kumbi na madarasa yanayoangaziwa kwa kutumia umeme. Wao wametekwa na vifaa vipya kama vile redio, runinga,

vitabu na kadhalika. Mfumo huu mpya wa elimu hutilia pia mkazo masomo mengine huku fasihi simulizi ikipuuzwa. Elimu ya vitabu ndiyo inayoshughulikiwa mno kuliko ile ya mapokeo.

4. Ili kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili ziendelee kutungwa, tunalazimisha:
   - Ni lazima wanajamii wasisitizie utafiti wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi hiyo;
   - Ni vizuri jamii husika iunde mikakati thabiti ya kufundisha fasihi hiyo shuleni;
   - Ni lazima jamii husika ihimize uhifadhi wa kazi za sanaa za fasihi hiyo;
   - Ni lazima lugha ya Kiswahili itumiwe kwa ufasaha ili kupambana na lugha za kikoloni. Kwa hiyo, wanajamii wanatakiwa kutopuuza fasihi simulizi ya Kiswahili.

5. Taja na kueleza vipera vya utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili unaoingia katika kundi la masimulizi.
   - Utanzu unaoingia katika kundi la masimulizi ni hadithi. Vipera vya utanzu huu ni ngano, hekaya na hurafa.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 6:

Kila mwanafunzi apewe fursa ya kusoma kwa usahihi akifuata alama za uakifishaji.

**C. Kusoma**

Kazi ya 7:

Mwalimu atoe fursa ya kusoma kwa ufasaha matini husika huku wanafunzi wakieleza ujumbe muhimu unaozungumziwa.

Kazi ya 8:

Sungura anazungumza na ajuza.

Kazi ya 9:

| |
|---|
| 1. Kigezo muhimu cha kuainisha fasihi ni namna msanii anavyoupitisha ujumbe wake yaani masimulizi ya mdomo au maandishi. |
| 2. Fasihi simulizi ya Kiswahili huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii. |
| 3. Ni lazima lugha ya Kiswahili itumiwe kwa ufasaha ili kupambana na lugha za kikoloni. |
| 4. Ili mazungumzo yaitwe kazi ya fasihi, ni lazima yawe na usanii wa aina fulani. |

**D. Msamiati**

Kazi ya 10:

**Kigezo:** Mtu, kitu au jambo la kuigwa

**Kalima:** Tamko; kauli

**Kiada:** Kwa utaratibu wake; vizuri; vema

**Ufaraguzi:** Hali kutenda jambo bila kutarajiwa kufanywa

**Fanani:** Msanii katika fasihi simulizi hasa anayesimulia hadithi, methali, vitendawili,... au anayecheza ngoma.

Kazi ya 11:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 12:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 13:

1. Ufaraguzi;
2. Uvumbuzi au Uchambuzi;

3. Mintarafu;
4. Hadhira

Kazi ya 14:

1. Ni lazima serikali yetu iunde mikakati thabiti ya kufundisha fasihi simulizi shuleni.
2. Uvumbuzi wa maandishi ni mojawapo kati ya mambo yanayosababisha uhaba wa kazi za fasihi simulizi..
3. Serikali ya Rwanda imepiga hatua kubwa katika kuendeleza elimu isiyo na ubaguzi.

Kazi ya 15:

| Maneno | Fasihi simulizi ya Kiswahili | Fasihi Andishi ya Kiswahili |
|---|---|---|
| Maombolezo<br>Tamthilia<br>Ngano<br>Hekaya<br>Riwaya<br>Hurafa<br>Tanzia | Maombolezo<br>Ngano<br>Hekaya<br>Hurafa | Tamthilia<br>Riwaya<br>Tanzia |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 16:

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutoa muhtasari wa kifungu cha habari kilichosomwa.

Kazi ya 17:

Kila mwanafunzi apewe fursa ya kusimulia hadithi yake mbele ya darasa.

Kazi ya 18:

Vidokezo:

-Hii ni televisheni au runinga. Runinga huhabarisha watu;

-Huelimisha watu;

-Huburudisha watu,...

Kazi ya 19:

| | |
|---|---|
| Uhaba wa kazi za fasihi simulizi ulisababishwa na | uvumbuzi wa maandishi |
| Uhaba wa kazi za fasihi simulizi ulisababishwa na | mfumo mpya wa elimu na maendeleo |
| Uhaba wa kazi za fasihi simulizi ulisababishwa na | mwingiliano na mgusano wa jamii mbalimbali |

Kazi ya 20:

Habari hii si ya kifasihi kwani utungaji wake haufuati kanuni za kisanaa zinazohusu kazi za kifasihi.

Kazi ya 21:

| | |
|---|---|
| 1. Katika Kinyarwanda, fasihi simulizi ni | ubuvanganzo nyemvugo. |
| 2. Sungura | ni mhusika aliyependelewa sana na Wanyarwanda na Waswahili katika hadithi zao na ambaye huwakilisha tabia ya werevu na ujanja |
| 3. Hadithi simulizi za Waswahili huwa na mwisho ufuatao: | Huu ndilo mwisho wa hadithi. |

**G. Utafiti**

Kazi ya 22:

Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kusoma matokeo ya utafiti.

Kazi ya 23:

Kusomea wengine maelezo husika.

**H. Mchezo**

Kazi ya 24:

Maneno hayo ni:

-Kizazi;

-Ishara;

-Kiswahili;

-Awali;

-Zinaweza.

**I. Kuandika**

Kazi ya 25:

Mawazo makuu:

1. Kupogoka kwa uchumi ni kuharibika kwake.
2. Kupogoka kwa uchumi huleta matatizo mengi katika nchi yakiwemo:

   -Kupanda kwa bei za bidhaa;

   -Fedha ya nchi kushuka thamani na raia kuikimbilia fedha yenye nguvu;

   -Viwanda kufanya kazi kwa shida kwa kukosa vipuli na malighafi;

   -Mashamba kukosa pembejeo na zana za kilimo. Jambo hili husababisha uzalishaji hafifu wa mazao ya chakula na biashara;

   -Hali ya usafiri na mawasiliano kuwa mbaya kutokana na ukosefu wa vipuli na mafuta ya vyombo vya usafirishaji. Jambo hili husababisha mlundikano wa bidhaa viwandani;

   -Huduma mbalimbali (kama vile huduma ya afya, elimu,...) kukosa vifaa muhimu;

-Maadili ya jamii kuweza kuingiliwa na rushwa na magendo na imani miongoni mwa watu kutoweka;

-Utendaji wa kazi kwa ujumla kuzorota na maendeleo ya nchi kudidimia kabisa.

Kazi ya 26:

| Neno | Umoja |
| --- | --- |
| Majambazi | Jambazi |
| Wezi | Mwizi |
| Ghala | Ghala |

Kazi ya 27:

| |
| --- |
| 1. Matamko hayo mafupi ya Kiswahili yanapatikana katika tanzu kama vile vitendawili, mafumbo, methali. |
| 2. Vyombo hivi visipofanya kazi maana yake ni kwamba mali inayozalishwa viwandani na mashambani haiwezi kusafirishwa. |
| 3. Hali ya kupogoka kwa uchumi huathiri moja kwa moja maadili ya jamii. |

Kazi ya 28:

1. Hii runinga mpya itatumiwa katika kuwahamasisha wafanyakazi kuhusu kuzalisha mali kwa kiwango.
2. Mwanangu, hivi ndivyo vinyume vya kutumia madawa ya kulevya.
3. Mwanafunzi wa kidato cha tano analazimishwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

Kazi ya 29:

| | | | |
| --- | --- | --- | --- |
| Kundi la | kwanza | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | masimulizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kundi la | pili | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | semi |
| Kundi la | tatu | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | ushairi |
| Kundi la | nne | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | mazungumzo |

Kazi ya 30:

-Habari "Kupogoka kwa uchumi" si ya kifasihi;

-Habari "Jongoo na chura" ni hadithi simulizi ya hurafa.

Kazi ya 31:

Ni:

-Kazi ya fasihi: Kazi ya fasihi simulizi;

-Utanzu: Hadithi;

-Kipera: Hurafa.

Kazi ya 32:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

# SOMO LA 4:

## MIFANO YA NYIMBO ZA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la nne.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua nyimbo na kujadili mchango wake katika jamii |
| **Vipindi:** | 8 |
| **Shughuli:** | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti; -Kucheka |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
|---|---|---|
| Kufafanua nyimbo za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | -Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza (Mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaani zeruzeru au albino)<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI na madhara yake<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo ya kudumu<br>- Usawa wa jinsi |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Wanamziki wanaimba wimbo uitwao “kasha langu”

Kazi ya 2:

Picha hii inahusu utanzu wa “nyimbo”.

Kazi ya 3:

Picha inaonyesha waimbaji na habari inazungumzia kuhusu nyimbo yaani kazi za sanaa ya uimbaji.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 4:

**1.Sifa za nyimbo:**

-Kutumia kiimbo au sauti maalumu na mdundo unaosisimua.

-Kuweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi. Wakati mwingine, huweza kuimbwa kwa kupokezana.

-Kuweza kuambatana na utumiaji wa ala za mziki. Mwimbaji ana uhuru wake wa kutumia zana za muziki anazotaka au kutumia sauti yake tu.

-Kutumia lugha teule, lugha ya mkato. Lugha hii ndiyo inayovuta msikilizaji ili aweze kupenda kazi hizo za sanaa ya lugha.

-Kutungwa katika mishororo na beti na kurudiarudia au kukariri maneno ili kusisitizia ujumbe. Nyimbo nyingi huwa na kiitikio.

**2. “Afrika ni Afrika iimbayo”.**

Waafrika huimba katika shughuli mbalimbali, nyakati mbalimbali na mahali mbalimbali.

**3. Ni lazima Wanyarwanda wahamasishwe kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa sababu maradhi hiyo inaendelea kuyaangamiza maisha ya mamia na mamia ya watu.**

**4.Umuhimu wa mfumo wa kisiasa wa vyama vingi:**

Katika mfumo wa vyama vingi, kila chama:

- -Kina uhuru wa kutoa maoni yake kuhusu mambo yanayotendeka katika uongozi wa nchi;
- -Kina uhuru wa kinagombea nafasi mbalimbali bungeni, serikalini,... dhidi ya vyama vingine;
- -Kina uhuru wa kujieleza, kutetea matendo yake ya nyuma na kuonyesha jinsi gani kinavyotaka kuboresha mambo tofauti na vyama vingine;
- -Kinachangia kwenye harakati ya kujenga nia ya jamii inamofanya kazi kama inashinda au kushindwa kwenye uchaguzi.

5.Umuhimu wa tumbuizo katika jamii ya Waswahili: Huimbwa kwa kufurahisha au kutoa burudani kwa watu tu. Zinaweza kuwa na onyo fulani au la.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 5:

Kusikiliza na kuzingatia mawazo muhimu ndilo lengo la kazii. Mwalimu ahakikishe kuwa lengo hii limefikiwa.

**C. Kusoma**

Kazi ya 6:

Kusoma ni stadi muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanasoma vizuri matini matini husika.

Kazi ya 7:

Huu ni wimbo wa watoto wanaojibizana.

Kazi ya 8:

Kusoma kwa sauti majina ya zana za muziki kutawasaidia wanafunzi kuzielewa na kutilia maanani matamshi bora.

Kazi ya 9:

1. Jamii mbalimbali za kiafrika hupenda sana nyimbo ambazo ni chanzo cha ushairi.
2. Mtu anaposikia wimbo anafurahi moyoni na kujisikia katika hali ya kutokuweko na usumbufu.
3. Nyimbo za harusi huimbiwa bwana na bibi harusi kwa kuwapa heko kwa kufunga ndoa na mawaidha ya kutunza familia.

Kazi ya 10:

- Wimbo wa kwanza ni wa kumbembeleza mtoto;
- Wimbo wa pili ni wa kazi (kuvuta kitu kizito);
- Wimbo wa tatu ni wa kazi (kilimo).

Kazi ya 11:

| Neno au kundi la maneno | Maelezo |
|---|---|
| Nyimbo za maombolezo | huimbwa wakati wa huzuni au simanzi, msiba, njaa,... ili kuwapa matumaini waombolezaji |
| Taarabu | ni muziki wa mahadhi unaotumia ala za mchanganyiko wa kiarabu, kihindi na kizungu |
| Wimbo | huundwa na maneno yanayochaguliwa na kupangwa vizuri na kutamkwa kwa sauti ya muziki |

**D. Msamiati**

Kazi ya 12:

**Kiitikio:** Sehemu ya wimbo ambayo mwimbaji huitikiwa; kipokeo; mkarara

**Kustarehe:** Kukaa au kuishi bila ya kuwa na shida au usumbufu; kuwa na raha

**Zeruzeru:** Mtu mwenye ulemavu wa ngozi ambaye nywele na ngozi yake imekosa rangi yake kamili na badala yake kuwa nyeupe sana na ambaye macho yake hayawezi kuvumilia mwangaza mwingi

**Kuliwaza:** Kubembeleza ili kutoa mtu majonzi; kupoza

**Nana:** Tamko litumikalo kumwitia mwanamke kabla au badala ya kutaja jina lake

**Labeka:** Tamko la kuitikia; abee; naam

Kazi ya 13:

Kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.

Kazi ya 14:

Hiki ni kipera cha "wimbo wa kazi"

Kazi ya 15:

- "Kupanda mmea" ni kuweka mbegu au mche katika ardhi ili ukue.
- "Kupandikiza mmea" ni kung'oa mmea na kuupanda mahali pengineau kupachika kichipukizi cha mmea ndani ya mmea mwingine ili kupata mmea chotara.

Kazi ya 16:

Kila kikundi kitajieleza kuhusu jambo hili.

Kazi ya 17:

| **Maneno** | **Sherehe** | **Kazi** |
|---|---|---|
| Kilimo<br>Uashi<br>Mavuno<br>Uvuvi<br>Harusi<br>Maulidi<br>Unyago<br>Jando | Harusi<br>Maulidi<br>Unyago<br>Jando | Kilimo<br>Uashi<br>Mavuno<br>Uvuvi |

Kazi ya 18:

1. Kasida / tumbuizo ni mojawapo kati ya nyimbo hizo.
2. Wakati wa majonzi, nyimbo hutumiwa kwa kumbembeleza / kumliwaza na kumfanya asimame wima.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 19:

Muhtasari wa yale ambayo ameyasoma uzingatiwe.

Kazi ya 20:

Kuimbia wengine kwa sauti nyororo kuzingatiwe.

Kazi ya 21:

Kuchunguza maoni ya wanafunzi kuzingatiwe ili wasiende nje ya mada.

Kazi ya 22:

| Ni mwiko | Kitendo |
|---|---|
| Ni mwiko | kufagia usiku kwani kunakimbiza baraka |
| | kuonyesha mwezi mchanga kwa kidole kwani kunaleta kukatika kidole |
| | kukutana na paka mweusi usiku kwani ni nuksi |
| | kumbusu mtoto usingizini kwani kunamfanya awe na majivuno ukubwani mwake |
| | kula gizani kwani ni kula na shetani |

Kazi ya 23:

| |
|---|
| 1. Kuelimisha, kufunza, kuonya na kuelekeza wanajamii kuhusu mambo mbalimbali yanayowagusa kama vile zamani za ufukara na ujinga |
| 2. Nyimbo huwa na umuhimu wa kukuza ustadi na sanaa katika jamii |

Kazi ya 24:

| | |
|---|---|
| 1. Nyimbo za kashifa huimbwa kwa kuwakashifu | watu wasio na staha/heshima/ nidhamu, wachawi, watoto vikojozi na wengineo. |
| 2. Nyimbo za kashifa huimbwa kwa kuwakashifu | watu wasio na adabu, walozi/ makahini, watoto vikojozi na wengineo. |

**F. Utafiti**

Kazi ya 25:

Wanafunzi watafute nyimbo mbalimbali.
Mfano:
Nalia chozi la damu,
nimeisha fahamu, usilie,
nyamaza kwani ukilia nami nitalia (Huu ni wimbo wa mapenzi)

**G. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 26:

Kuwaambia wenzake kichekesho.

**H. Kuandika**

Kazi ya 27:
Kila mwanafunzi atunge sentensi zake
Mfano: Makahaba huwa na tabia zao.

Kazi ya 28:

1. Kasida;
2. Kiarabu;
3. Taarabu;
4. Hodiya.

Kazi ya 29:

| |
|---|
| 1. Lugha ya mnato huingizwa ili kuvutia hadhira |
| 2. Lugha hii ndiyo inayovuta msikilizaji ili aweze kupenda kazi hizo za sanaa ya lugha. |
| 3. Wakati mwingine, huweza kuimbwa kwa kupokezana. |

Kazi ya 30:

1.Ni nyimbo za kuwasifu viongozi wa kisiasa, kuunga mkono mfumo wa utawala fulani na kuonyesha uzalendo kwa kusifia taifa au nchi.
2.Nyimbo hutia moyo watu wakati wa kufanya kazi ngumu kama vile kilimo, kuvuta kitu kizito, uvuvi, ujengaji nyumba na kadhalika.
3.Mama au mlezi au mtu mwingine humwimbia mtoto mchanga nyimbo hizi kwa makusudi ya kumwongoa na kumlaza.

Kazi ya 31:

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutunga wimbo huo.

# SOMO LA 5:

# MIFANO YA METHALI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la tano.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua methali, kuzitumia kwa kuzihusisha na maisha ya kila siku na kujadili mchango wake katika jamii |
| **Vipindi:** | 7 |
| **Shughuli:** | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti; -Kucheka; -Michezo |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
|---|---|---|
| Kufafanua nyimbo za fasihi simulizi ya Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo kuhusu kuboresha uzazi (kutii mpango wa serikali wa kuboresha uzazi) |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kuna:

-Kanga (pameandikwa methali “Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika”);

-Mzee mmoja ambaye anawafundisha watoto methali.

Kazi ya 2:

Picha zinahusu utanzu wa “methali.”

Kazi ya 3:

Picha zinahusu “methali”, jambo ambalo linazungumziwa katika habari.

**A. Maswali ya Ufahamu**

Kazi ya 4:

1. Asili ya utamu wa methali ni lugha nyepesi inayopenya moja kwa moja katika mioyo ya wasikilizaji.
2. Dhima ya methali katika jamii ni:

   - Kuelimisha wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayoikabili jamii yao.
   - Kuonya wanajamii yaani kuipa jamii maadili bora.
   - Kukosoa jamii na kurekebisha mwenendo wake.
   - Kuhamasisha wanajamii na kuwatia moyo.

3. “Kazi ya kutafsiri methali huwa ngumu”.

   Watu hufikiri kuwa ni kazi inayofanywa neno kwa neno yaani “tafsiri sisisi”. Ukweli ni kwamba ni jambo la kumakinikia. Kwa mfano, mtu akisema “mtaka cha uvunguni, sharti ainame”. Kauli hii hutumiwa kwa kumhamasisha mtu afanye kazi ili apate faida. Kwa kuitafsiri neno kwa neno katika Kinyarwanda [ushaka ikiri munsi y’ameza, agomba kunama], inapoteza utamu wake. Ni lazima kutafuta methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ili utamu wake ubakie. Methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ni “ushaka inka aryama nka zo”.

4. “Wanafasihi wengi wanajua methali zote za Kiswahili”. Kauli hii haina ukweli kwa sababu hakuna mtu anayeweza kujidai kuwa anajua yote kuhusu methali.

5. Methali zote zilizotumiwa katika hadithi “Linalowezekana leo lisingoje kesho”.

- Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako
- Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu’
- Linalowezekana leo lisingoje kesho
- Wakati una mabawa
- Wakati titi la nyati hukamuliwa kwa mashaka
- Haraka haraka haina Baraka
- Ngoja ngoja huumiza matumbo
- Mchumia juani hulia kuvulini
- Maneno mengi hayavunji mfupa
- Kesho kesho nitafanya
- Mwoga hukimbilia wanawe
- Kitamu hutokea kwa mwenye nguvu

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 5:

Kusoma na kuandika mawazo makuu ndilo lengo la kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa lengo hili limefikiwa.

**C. Kusoma**

Kazi ya 6:

Kusoma mara nyingi kifungu hiki kutawasaidia wanafunzi kukielewa. Wanafunzi wapewe fursa hii.

Kazi ya 7:

Kwenye picha hii, kumeandikwa “methali” moja ambayo ni “Kamba hukatika pabovu”. Na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu methali.

Kazi ya 8:

| |
|---|
| 1. Waliendelea kulima huku jua kali likichoma miili yao |
| 2. Kazi ya kutafsiri methali si rahisi kama inavyodhaniwa na watu ambao hawajapevuka katika mambo ya lugha |
| 3. Usiwategemee wengine katika kukidhi mahitaji yako |
| 4. Unapojikita sana katika anasa za dunia na kuwa na tabia ya kupenda kuzini, hii ni tamaa |

## D. Msamiati

Kazi ya 9:

Kunata: Kushika mahali kwa nguvu kama vile inavyoshika gundi
Kupenya: Kupitia kwenye tundu ndogo, ufa au mwanya finyu na kuingia ndani
Anasa: Mambo au hali ya raha nyingi
Kuganga: Kufanyia mgonjwa matibabu; kutengeneza kilichovunjika au kuharibika
Maktaba: Mkusanyo wa vitabu vingi; nyumba ambamo watu huenda kujisomea au kuazima vitabu

Kazi ya 10:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

Kazi ya 11:

| Kauli | Kikundi cha methali | Kikundi cha nyimbo |
|---|---|---|
| - Baada ya dhiki faraja;<br>- Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo;<br>- Mama nipe radhi;<br>- Chanda chema huvishwa pete;<br>- Sega langu la asali;<br>- Lala salama;<br>- Jogoo la shamba haliwiki mjini. | - Baada ya dhiki faraja;<br>- Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo;<br>- Chanda chema huvishwa pete;<br>- Jogoo la shamba haliwiki mjini. | - Mama nipe radhi;<br>- Sega langu la asali;<br>- Lala salama; |

Kazi ya 12:

1.Walikumbana na majanga ya magonjwa ya zinaa.
2.Kidole kimoja hakivunji chawa.
3.Kusubiri muda mrefu kunasumbua mtu.
4.Ilikuwa saa tano baada ya jua kuchomoza.

Kazi ya 13:

1. Methali ni semi kama nahau. (semi; vitendawili)
2. Hizo unazoona ni rafu za vitabu. (kababu; rafu)
3. Mume wake amempa bunda la noti. (bunda; bandia)
4. Amenunua mkungu wa ndizi. (Mkundu; mkungu)

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 14:

Kutoa muhtasari ndilo lengo la kazi hii. Wanafunzi wapewe fursa hiyo.

Kazi ya 15:

| **Hali** | **Methali** |
|---|---|
| 1. Tabia ya kuombaomba vitu humfanya mwombaji kuwa mnyonge au duni | Ombaomba huleta unyonge |
| 2. Mkubwa wao akiondoka, walio chini yake hujiona kuwa huru na hufanya mambo wapendavyo | Paka akiondoka, panya hutawala |
| 3. Usiporekebisha kosa dogo tangu mwanzo, hatimaye utapata hasara kubwa | Usipoziba ufa, utajenga ukuta |

Kazi ya 16:

Kila mwanafunzi atoe maoni yake.

Kazi ya 17:

1. Chema chajiuza kibaya chajitembeza / Akeza karigura
2. Bandubandu humaliza gogo / Buhoro buhoro ni rwo rugendo
3. La kuvunda halina ubani / Akabaye icwende ntikoga
4. Umleavyo mtoto ndivyo akuavyo / Igiti kigororwa kikiri gito

5. Paka akiondoka, panya hutawala / Ahabyutse ingwe haryama umukara

Kazi ya 18:

1. UKIMWI, homa, mafua, upele na kifaduro ni maradhi.
2. Kilemba, suruali, kanzu na fulana ni mavazi.
3. Kiroboto, chawa, nyigu, nyuki na panzi ni wadudu.

**F. Utafiti**

Kazi ya 19:

Kutafuta methali mbalimbali ndiko kunakodhamiriwa na mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya methali zao mbele ya darasa.

**G. Mchezo**

Kazi ya 20:

C/4: L, E, G, O
E/7: B, U

**H. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 21:

Kutafuta kichekesho kwa kila mwanafunzi kuzingatiwe.

**I. Kuandika**

Kazi ya 22:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

Kazi ya 23:

1. Dalili ya mvua ni mawingu.
2. Mchumia juani hulia kivulini.
3. Shukrani za punda ni mateke.
4. Ganda la muwa la jana, chungu kaona kivuno.

Kazi ya 24:

1. Methali hutumiwa kila wakati katika mazungumzo ya kawaida ya wanajamii na hunata akilini kwa urahisi kuliko kauli nyingine.
2. KAGABO alimhimiza mkewe kazi wamalize ngwe waliyokuwa wameanza na kusema, “Linalowezekana leo lisingoje kesho!”
3. Tunapotenga kitu kwa manufaa ya baadaye (akiba) na kuanza kukimega kidogo kidogo, mwisho tutashtuka tumekimaliza.
4. Mtu ambaye hakuweza kurekebisha mwenendo wake na tabia yake mbaya unaweza kumwonya kwa kupitia methali kama vile “asiyesikia la mkuu huvunjika guu”.

Kazi ya 25:

| |
|---|
| 1. Wengi walimsifu na kusema kwamba wakati sisi tunatafuta methali, zake zinabubujika kama maji. |
| 2. Tusibabaishwe na mabaya yaliyofanyika kwani hayana umuhimu kwetu. |
| 3. Ingawa mtu anaweza kuwa na ulemavu au upungufu fulani wa kimaumbile, ni kiumbe kama sisi. |

Kazi ya 26:

<table>
<tr><td>Methali ni semi muhimu kwa binadamu kwani ni njia ya mkato ya</td><td>kuelimisha wanajamii</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Methali ni semi muhimu kwa binadamu kwani ni njia ya mkato ya</td><td>kuonya jamii</td></tr>
<tr><td>kukosoa jamii na kurekebisha mwenendo wake</td></tr>
<tr><td>kuhamasisha wanajamii na kuwatia moyo</td></tr>
</table>

# SOMO LA 6:

# MIFANO YA NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la sita.

| | | |
|---|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua nahau na misemo, kuitumia kwa kuihusisha na maisha ya kila siku na kujadili mchango wake katika jamii na lugha | |
| **Vipindi:** | 7 | |
| **Shughuli:** | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti; -Michezo | |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi | |
| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
| Kufafanua nahau na misemo ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Amani na maendeleo |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Picha inaonyesha kitabu ambacho ni “Kamusi ya misemo na Nahau.”

Kazi ya 2:

Wanafasihi husema kuwa “nahau” ni semi zinazodai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali “misemo” ni semi zisizokuwa na au zisizohitaji vitenzi. Maana kamili ya “misemo” haihitaji kitenzi ili kueleweka ingawa inaweza kutumiwa pamoja na vitenzi.

Kazi ya 3:

Picha inaonyesha kitabu ambacho ni “Kamusi ya misemo na Nahau”. Na habari yetu inazungumza kuhusu nahau na misemo.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 4:

1. Kichwa cha habari ni “Tamaa mbele, mauti nyuma”. Hii ni methali. Maana yake ni kuwa “tamaa huangamiza”. Mtu akitamani sana kitu fulani, ni lazima ajihadhari kwani mwisho wake unaweza kuwa kifo. Mfano ni ule wa ajali iliyotokea na watu wengi wakatamani sana kuyateka mafuta ya bwerere. Walakini, mambo hayakuwa mema kwa sababu mtu mmoja kati yao alipowasha sigara, moto mkali ulizuka na wengi wao wakateketea kabisa. Ni kusema kuwa tamaa yao ya kuyachota mafuta ya mahonyo iliwaletea kifo”.
2. Wanafasihi husema kuwa “nahau” ni semi zinazodai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali “misemo” ni semi zisizokuwa na au zisizohitaji vitenzi. Maana kamili ya “misemo” hayahitaji kitenzi ili kueleweka ingawa inaweza kutumiwa pamoja na vitenzi. Kwa mfano, “kupigwa kalamu”, “kumwaga unga”, “kugonga mwamba” ni nahau lakini “lila na fila”, “mdomo na pua”, hii ni misemo. Walakini, kutokana na tofauti hiyo ndogo, wanafasihi wengi hupendelea kutumia maneno hayo mawili pamoja yaani “nahau na misemo”.

a. Nahau na misemo ni semi zinazopunguza ukali wa maneno.

Siku za leo, mataifa yote yanapigana na janga la ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI ambalo linaendelea kuangamiza watu wengi sana. UKIMWI si kama tetekuwanga au kifaduro kwani haina dawa. Kwa hiyo, ni lazima wale

wenye kiini au virusi vya ugonjwa huo watunzwe vizuri kama vile:

- kupatiwa dawa zinazowasaidia katika maisha yao na ambazo wanahitaji;
- kutofanyiwa ubaguzi wowote na kutotengwa na watu wengine;
- kutotumia kauli zinazoweza kuwafanya wadharauliwe na kadhalika.

Kuhusu kauli hizi, badala ya kusema kuwa “fulani aliweza kuvumilia” ingawa yuko katika hali mbaya ya kiafya kutokana na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI, unaweza kusema kuwa “fulani anajikaza kisabuni”. Kama “amekufa”, unaweza kutumia tamko la “kuaga dunia”. Hii ni nahau na inaeleweka kuwa inapunguza ukali wa maneno ya kwanza.

3. Nahau na misemo:

- Anga ikavaa joho jeusi: Giza ikatawala
- Usiku ukashika hatamu: Usiku ukaongoza
- Baadhi yao walisikika wakitia chumvi: Kuongeza maelezo yenye kusifu jambo kupita kiasi
- Kakangu ya kujipatia jiko: Kuoa
- Wasiwasi wa mwasi ukanivaa: ukanitawala
- Lakini nilipiga moyo konde: Kuwa jasiri
- Wengi wao walikula mwande: Kukosa ulichotumainia
- Lakini nikagonga mwamba: Kutofanikiwa
- Kwa kweli, lila na fila havitangamani: Mema na mabaya
- Niliponea katika tundu la sindano: Kuponea kwa bahati
- Maneno tamaa, pupa na papara niliyazika katika kaburi la sahau: Kutupilia mbali jambo ili kulisahau kabisa

4. Methali zote zilizotumika katika matini “Tamaa mbele mauti nyuma”:

- Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo: kama kuna dalili za jambo Fulani, ni kusema kwamba bila shaka litatendeka
- Fumbo hufumbiwa mjinga mwerevu akatambua: Unapomwambia kitu mtu mpumbavu hawezi kutambua haraka unalolizungumzia. Lakini mwerevu anatambua upesi.

- Aliye kando haangukiwi na mti: Asiyehusika na jambo, madhara yake hayawezi kumfikia.
- Tamaa mbele, mauti nyuma: Vinyume vya hamu kubwa ya kupata kitu ni kifo. Usitamani sana kitu ili usije ukafikiwa na janga kubwa.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 5:

Kutega sikio na kuandika mawazo makuu ndiyo malengo ya kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa yamefikiwa.

**C. Kusoma**

Kazi ya 6:

Kusoma mara nyingine kwa kufuata alama za uakifishaji ndilo lengo la kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa limefikiwa.

Kazi ya 7:

Jambazi ameiba fuko la mtu na kupiga mbio. Mtu huyo anamfuata kwa kukimbia.

Kazi ya 8:

Kamilisha sentensi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika habari:

1. Kwa wayowayo na jakamoyo nilikwenda nyatunyatu na kutupa jicho.
2. Nahau na misemo ni semi fupi zinazotumia maneno ya kawaida lakini maana yake huwa fiche.
3. Nilighairi kubaki nyuma kama koti la mzee na kuamua kuwa wa mbele kama mfuko wa shati.
4. Kama ajali, tuligutushwa na kishindo kikuu kilichotisha kama Izraili.

Kazi ya 9:

1. Kabla hajapuliza fundo la kwanza, mlipuko wa ajabu ulisikika.
2. UKIMWI si kama tetekuwanga au kifaduro kwani haina dawa.
3. Muda mrefu haukupita kabla ya meza kujaa mapochopocho kochokocho na harufu nzuri kusikika kote sebuleni.

4. Mara maneno tepetepe na mipayuko kama ya wehu ikatamalaki na kuhinikiza hewani.

**D. Msamiati**

Kazi ya 10:

**Darubini:** Chombo chenye lensi kinachofanya vitu vilivyo mbali vionekane karibu na vidogo vionekane vikubwa.
**Majungu:** Vyungu vikubwa (Chungu ni chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kwa kupikia).
**Kuzagaa:** Kuwa kila mahali; kuenea kila mahali.
**Kushamiri:** Kuenea kwa jambo au habari; kuzagaa; kutapakaa.
**Umbu:** Jina wanaloitana ndugu wazawa wa kike na wa kiume.
**Kochokocho:** Kwa wingi; tele.
**Kugwengwenya:** Kubandua kwa meno kama vile nyama kwenye mfupa; kuguguna.
**Kutuama:** Kushuka kutoka mahali fulani na kwenda kulala chini.
**Libasi:** Mavazi au nguo.
**Jakamoyo:** Masumbufu ya rohoni; kero la moyo.
**Ushamba:** Tabia za kijinga zinazofikiriwa kuwa ni za mtu anayeishi mbali na miji yaani katika vitongoji vya mbali.
**Bwege:** Mtu mjinga au mpumbavu.
**Bwerere:** Kitu cha bure au cha mahonyo.
**Dafrau:** Mgongano wa nguvu baina ya vitu viwili au zaidi (Kupigwa dafrau=Kugongwa na).

Kazi ya 11:

Kila jozi itunge sentensi zake.

Kazi ya 12:

1. Kupiga mbizi
2. Kupiga mwayo
3. Kupiga mluzi
4. Kupiga darubini

Kazi ya 13:

1. Kuchungulia kaburi: Kuwa mgonjwa kukaribia kufa; kunusurika kifo.
2. Kutia utambi: Kuchochea ugomvi.
3. Kutoa lulu: Kusema maneno mazuri ya maana na ya hekima.
4. Kumwaga unga: Kufukuzwa kazi.

Kazi ya 14:

| Kitenzi | Nahau |
|---|---|
| 1. Kupiga | 1. Kupiga mbio: Kukimbia haraka<br>2. Kupiga pasi: Kunyosha nguo kwa kutumia pasi ya mkaa au ya umeme<br>3. Kupiga chafya: Kuchemua<br>4. Kupiga hodi: Kubisha hodi<br>5. Kupiga jeki: Kumpa mtu msaada<br>6. Kupiga mafungu: Kugawanya<br>7. Kupiga maji: Kunywa ulevi<br>8. Kupiga mwayo: Kuonyesha ishara ya kusinzia au kutoshiba kwa kufunua mdomo<br>9. Kupiga mbiu: Kutangaza habari<br>10. Kupiga mbizi: Kuzama chini ya maji mtini<br>11. Kupiga mstari: Kuchora mstari chini ya maandishi<br>12. Kupiga moyo konde: Kuwa jasiri; kukata shauri gumu |
| 2. Kuchapa | 1. Kuchapa kazi: Kufanya kazi kwa bidii<br>2. Kuchapa maji: Kunywa pombe nyingi<br>3. Kuchapa miguu: Kwenda kwa miguu |
| | |

Kazi ya 15:

Joho jeusi tititi

Tulijipweteka pwete

Nikitetemeka tetete

Papo hapo

Mweusi tititi

Ulizuka zu

Waliteketea teketeke

Kazi ya 16:

1. Hadija alimwomba dadake viatu lakini dadake alimwambia, “sikupi ng’o!”.
2. Mvua ilimnyeshea na kurowa chapachapa / chepechepe / chapa.

3. Alishika buku lile na kulichana shwaa.
4. Alipofika nyumbani alitulia tuli.
5. Fulani alifunga kamba na kulikaza ngi.

### Kazi ya 17:

- Anga ikavaa joho jeusi tititi kama kizimwili;
- Kishindo kikuu kilichotisha kama Izraili;
- Nikitetemeka tetete kama kifaranga aliyenyeshewa na mvua ya gharika;
- Mipayuko kama ya wehu ikatamalaki;
- Nilighairi kubaki nyuma kama koti la mzee;
- Kuamua kuwa wa mbele kama mfuko wa shati;
- Jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti;
- Mweusi tititi kama lami aliwasha sigara;
- Moto mkubwa ulizuka zu kama mizuka;
- Kuangushana kama magari barasteni;

### Kazi ya 18:

Kila mwanafunzi aingize katika sentensi yake “kama kinywa cha samaki.”

### Kazi ya 19:

1. Mganga anayeshughulikia mambo ka kuboresha uzazi ni mrefu kama twiga / jini / mlingoti.
2. Kiranja wa darasa letu ni mfupi kama kinu.
3. Dadake aliyeambukizwa UKIMWI amekonda na kuwa kama sindano / mbu.
4. Yeye anasema kama kasuku.
5. Kiongozi anayeshughulikia mambo ya uzalishaji mali ana akili kama mchwa.

Kazi ya 20:

| Kauli | Nahau | Methali |
|---|---|---|
| - Cheche huzaa moto<br>- Alimpiga pambaja mwandani<br>- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi<br>- Usimpe nyama ya ulimi<br>- Kaza kamba ndugu!<br>- Yote yang'aayo si dhahabu | - Alimpiga pambaja mwandani<br>- Usimpe nyama ya ulimi<br>- Kaza kamba ndugu! | - Cheche huzaa moto<br>- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi<br>- Yote yang'aayo si dhahabu |

## E. Kuzungumza

Kazi ya 21:

Kutoa muhtasari ndilo lengo la kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa lengo hili limefikiwa.

Kazi ya 22:

| Tungo ya kukamilisha | Neno la kukamilisha |
|---|---|
| 1. Badala ya kutumia neno "kuoa", yeye alisema kuwa "alijipatia ..................." | Alijipatia jiko |
| 2. Kumezea .............. kitu ni kukitamani sana | Kumezea mate |
| 3. Anapoishi si mbali; ni pua na ............... | Pua na mdomo |

Kazi ya 23:

| Nahau | Maana |
|---|---|
| 1. Amewachukua wazee wake | Amewatunza vizuri wazazi wake |
| 2. Amekuwa popo | Ni kigeugeu |
| 3. Ana ulimi wa upanga | Ana maneno makali |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kufyata mkia | Kuacha kutenda jambo kufuatana na woga |
| 5. | Amepaka mafuta kwa mgongo wa chupa | Amedanganya |
| 6. | Usiwe kupe | Fanya kazi |
| 7. | Kujipalia mkaa | Kujitia matatani |
| 8. | Usiwe na mrija | Usiwanyonye wenzako |

Kazi ya 24:

1. Ndugu yake alimkaribisha shingo upande.
2. Mdogo wangu ni kiguu na njia yaani mtu asiyetulia mahali pamoja.
3. Kwa uzi na sindano, waliweza kuboresha uzazi katika familia yao.

Kazi ya 25:

| |
|---|
| 1. Tukiwa katika pilikapilika za kuyateka mafuta ya mahonyo / bure, jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti na mweusi tititi kama lami aliwasha sigara |
| 2. "Kaka yake amemwaga unga": Inamaanisha kwamba "Kaka yake amepigwa kalamu" |
| 3. Nami nilifanya kwa kila namna lakini nikagonga mwamba |

**F. Utafiti**

Kazi ya 26:

Kila kikundi lina nahau zake / Mfano: Kuba Gashuhe: Kuwa na mkono wa birika (Yaani kuwa na tabia ya kunyima watu vitu mbalimbali)

**G. Mchezo**

Kazi ya 27:

Kila mwanafunzi aulize swali lake.

## H. Kuandika

Kazi ya 28:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake.

Kazi ya 29:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kukurukakara | za | kujinusuru | zilianza |
| Vikiri | vya | kujiokoa | vilianza |
| Hekaheka | za | kujiponya | zilianza |

Kazi ya 30:

| **Kitu** | **Nahau** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | Kupata kitanda | Kulazwa hospitali |
| 2. | Kutia chumvi | Kuongeza maelezo yenye kusifu jambo kupita kiasi |
| 3. | Kuchapa maji | Kunywa pombe nyingi |

Kazi ya 31:

Kila kikundi kitunge sentensi zake.

Mfano: Kalisa, mtu mwenye mkono wa birika, aliporudi nyumbani alikuwa amevaa miwani. ...

# SOMO LA 7:

# MIFANO YA VITENDAWILI VYA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la saba.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua vitendawili na kujadili mchango wake katika jamii</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">7</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti; -Michezo; -Kutafsiri</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
<tr><td>Kufafanua vitendawili vya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuvitumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake</td><td>- Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>- Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii.</td><td>- Elimu isiyo na ubaguzi<br>- Amani na maendeleo</td></tr>
</table>

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kinachoonekana kwenye picha:

-Bikizee anayekaa pamoja na watoto watatu. Wanatega na kutegua vitendawili.

Kazi ya 2:

Picha inaonyesha Bikizee anayekaa pamoja na watoto wengi na kutega na kutegua vitendawili. Kifungu cha habari nacho kinazungumzia kuhusu vitendawili.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka. Kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu mazingira yake na kujaribu kupata jibu. Katika shughuli hii, mteguaji huwaza sana kuhusu mazingira hayo na kulinganisha majibu mbalimbali yanayoweza kutolewa. Hii ni namna moja ya kukuza uwezo wake wa kukumbuka na kufikiria.
2. "Vitendawili hutegwa kwa njia ya uchangamfu na ushindani". Vitendawili huzingatia mfumo wa kutega (yaani kuuliza swali) na kutegua (au kujibu swali). Mtegaji na mteguaji hutii utaratibu ufuatao:

Mtegaji : Kitendawili!
Mteguaji : Tega!
Mtegaji : (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").
Mfano : Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
Mteguaji : (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").
Jibu : Nyota

Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu. Hapa, inaonekana wazi kwamba vitendawili hutegwa kwa njia ya kufurahisha yaani uchangamfu na njia ya kupima ujuzi na uwezo wa kufikiri wa mtu yaani ushindani.
3. Kuna tofauti kati ya vitendawili na mafumbo kuhusu namna michezo hiyo inavyochezwa.

Kitendawili ni tungo fupi ambayo huwa na swali wazi yaani swali linaloulizwa kwa kutumia lugha ya mafumbo. Mafumbo hayo ndiyo yanayoufanya utanzu huu uwe wa sanaa ya hali ya juu.

Majibu hutolewa kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Kujibu kunahitaji ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni za mazingira ya jamii husika. Mtu hujibu kiufundi kwa kuzingatia utaratibu wa kuvutia.
Mtegaji na mteguaji hutii utaratibu ufuatao:

**Mtegaji** : Kitendawili!
**Mteguaji** : Tega!
**Mtegaji** : (Anatoa kitendawili chake yaani “kutega kitendawili”).
**Mfano** : Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
**Mteguaji** : (Anatoa jibu yaani “kutegua kitendawili”).
**Jibu** : Nyota

Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

Kuna kipengele kingine cha fasihi simulizi kinachofanana kwa kiasi na vitendawili lakini chenye utaratibu wake wa kipekee. Kipengele hicho ni “mafumbo”. Mafumbo ni kauli zinazoeleza jambo kwa njia fiche yaani isiyo wazi. Msimulizi anatoa fumbo lake na kazi ya wasikilizaji ni kulifumbua.

Katika mchezo huu wa ushindani wa mafumbo, msimulizi anasema “Fumbo mfumbie mjinga”. Msikilizaji anajibu “Mwerevu hiling’amua” na kufumbua jambo linalozungumziwa. Mifano ya mafumbo na ufumbuzi wake:

Mimi na ndugu yangu tulinunua fahali mmoja kutoka sokoni. Baada ya mwaka mmoja alijifungua ndama wawili. Je, kila mtu alipata wangapi? / [Ufumbuzi: Fahali hajifungui].

4.Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.
5.Dhima ya vitendawili katika jamii:

**Vitendawili:**
-Huburudisha watu;
-Huunganisha jamii;
-Huhamasisha watu kuhusu mazingira yao;
-Hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka;
-Hukuza na kuhifadhi amali na tamaduni za jamii;
-Vilitumika kwa muda mrefu kupitisha wakati na kuwafanya watoto wasilale mapema kabla ya chakula kuwa tayari.

6.“Vitendawili ni kipengele cha masimulizi”. Hapana. Vitendawili ni kipengele cha semi.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kutega sikio na kuandika mawazo makuu ndiyo malengo ya kazi hii. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaeleza mawazo makuu ambayo yamezungumziwa.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma matini mara nyingine na kuheshimu alama za uakifishaji kutamsaidia mwanafunzi kuielewa. Mwalimu atoe fursa hiyo kwa wanafunzi wote.

Kazi ya 6:

Picha inaonyesha ndege ambao wametua mtini. Jibu la kitendawili hiki “Anajenga ingawa hana mikono” ni “ndege”.

Kazi ya 7:

1. Siku za leo, vipo vitendawili vingi vilivyotungwa na watu wa vizazi vilivyotangulia.
2. Kitendawili ni tungo fupi ambayo huwa na swali wazi yaani swali linaloulizwa kwa kutumia lugha ya mafumbo.
3. Kujibu kunahitaji ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni za mazingira ya jamii husika.

Kazi ya 8:

Wanafunzi wapewe fursa ya kusoma kwa ufasaha sentensi husika.

**D. Msamiati**

Kazi ya 9:

**Kizibao:** Vazi kama koti fupi lisilo na mikono

**Dema:** Mtego wa samaki uliofumwa kwa matete au vijiti

**Chane:** Shada moja la mkungu wa ndizi (kundi dogo la ndizi zinazojifungia kwenye fundo moja)

**Popoo:** Tunda gumu lenye umbo la duara lililofunikwa na makumbi kama vile nazi, ambalo hukatwa vipande vyembamba na kutafunwa pamoja na tambuu

Kazi ya 10:

Kila kikundi kitunge sentensi zake / Mfano: Kizibao ni nguo ya wanawake inayofunika mwili wote.

Kazi ya 11:

Kila kikundi kitunge sentensi zake.

Kazi ya 12:

1. Kaka kapiga mbizi kaibuka akiwa na mvi / Mwiko unaposonga ugali
2. Nyumba yangu haina mlango / Yai
3. Nililima shamba langu kubwa sana lakini nilipovuna, mavuno yalitosha kiganja cha mkono tu / Kichwa na nywele unapozinyoa

Kazi ya 13:


1. Nimesimika moja nikaezeka /



2. Saa yangu kila siku hutembea, ikisimama haitengenezeki tena /



3. Mifugo ya babu imetafuna ukuta /



Kazi ya 14:

1.Popoo;
2.Kisogo;
3.Kitendawili.

Kazi ya 15:

1.Wanyarwanda wengi wana mwamko wa kutumia mashine iitwayo kompyuta na intaneti.
2.Kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu mazingira yake na kujaribu kupata jibu.
3.Katika siku zilizopita, vitendawili vilitumiwa kama njia ya kuwafanya watoto wangojee na kuvumilia mpaka chakula kiwe tayari.

Kazi ya 16:

| **Kauli** | **Methali** | **Kitendawili** |
|---|---|---|
| 1. Huzitoa zikarudi | | X |
| 2. Dunia hadaa na walimwengu shujaa | X | |
| 3. Ninacho lakini sikitumii | | X |

| | | |
|---|---|---|
| 4. Mkufu wangu mrefu unatembea | X | |

Kazi ya 17:

Vidokezi:

- Huburudisha watu.
- Huunganisha jamii.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 18:

Mwalimu atoe fursa ya kutoa muhtasari huo kwa wanafunzi.

Kazi ya 19:

| Kitendo | Jina |
|---|---|
| 1. Kutega kitendawili | Mtegaji |
| 2. Kutegua kitendawili | Mteguaji |

Kazi ya 20:

1. Askari mlangoni / Kufuri
2. Mhuni wa ulimwengu / Nyuki
3. Mfalme katoa jicho jekundu / Jua linapochomoza
4. Nanywa supu nyama naitupa / Muwa
5. Mzungu anachungulia dirishani / Kamasi

Kazi ya 21:

1. Pana visu vingi lakini mpini mmoja tu / Chane ya ndizi
2. Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani / Chawa.
3. Mkufu wangu mrefu unatembea / Siafu.
4. Hazikauki umande / Pua za mbwa.

Kazi ya 22:

| | |
|---|---|
| 1. Kuna kipengele kingine cha fasihi simulizi kinachofanana kwa kiasi na vitendawili lakini chenye | muundo wake usio wa kawaida |
| 2. Hali hii hudhihirisha kuwa tamaduni za vizazi vya zamani zilitufikia kupitia vitendawili kwa sababu utanzu huu | huwaunganisha pamoja wattu wengi |
| 3. Kwa kawaida, jioni ni wakati mzuri wa kupumzika kwa watu mbalimbali baada ya | shughuli mbalimbali za mchana |

**F. Mchezo**

Kazi ya 23:

Kila mwanafunzi ana swali lake.

Kazi ya 24:

Upande wa kushoto-kulia:
A/1: Ushoroba;
D/1: Kababu;
F/1: Masika;
H/2: Injili.

Upande wa juu-chini:
1/A: Uhakimu;
2/A: Samawari;
5/A: Rumbi;
7/C: Goigoi;
8/A: Ajuza.

## G. Utafiti

Kazi ya 25:

Kila kundi lina vitendawili vyake.

## H. Tafsiri

Kazi ya 26

1. Nshinze umwe ndasakara / Igihumyo (icyobo) // Nimesimika moja nikaezeka (Uyoga)
2. Mugongo mugari mpekera abana / Uburiri // Mama nieleke (Kitanda)
3. Gitimba araguye n'ingabo ze / Igitoki n'amakoma // Mshikeni mzee anaanguka na ndevu zake (Mgomba na mkungu unapokatwa na kuanguka)
4. Karakurizaga karakurutaga wa duri we! / Akanyarirajisho // Anakuliza anakuzidi umri Mkubwa we! (Mdudu jichoni)

## I. Kuandika

Kazi ya 27:

1.Nimesimika moja nikaezeka / Uyoga

2.Mama nieleke / Kitanda

3.Mwanangu hulia msituni / Shoka

Kazi ya 28

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 29:

| | | |
|---|---|---|
| Vitendawili | huburudisha | watu |
| | huunganisha | jamii |
| | huhamasisha | watu |

Kazi ya 30:

Kila jozi ina aya yake

- Huhamasisha watu kuhusu mazingira yao.

- Hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka.
- Hukuza na kuhifadhi amali na tamaduni za jamii.

Kazi ya 31:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Walipofika karibu na mto, iliwabidi wote kuvuka kwenda ng'ambo | kutokana na mazingira mapya ya jamii husika |
| 2. Vilevile, vipo vitendawili vya kisasa vinavyoundwa | apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu |
| 3. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha | lakini hawakuwa na mtumbwi wala daraja la kuvukia |

# SOMO LA 8: USHAIRI WA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI

# A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

## Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la nane.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua mashairi na kujadili mchango wake katika jamii</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">8</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Kucheka; Mdahalo</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| Kufafanua mashairi ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kuyatumia kama sanaa ya kuiendeleza jamii au nchi yake | -Kuheshimu na kuhifadhi mila na desturi za jamii.<br>-Kuitathmini fasihi na kuonyesha hamu ya kuwa msanii. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI<br>-Usawa wa jinsia<br>-Kutunza mazingira |

**B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI**

Kazi ya 1:

Tunaona:

-Maandishi “Mashairi ya watoto”;

Mume anakaa pamoja na watoto na mke wake wanaongea kuhusu mashairi.

Kazi ya 2:

Picha inahusu “mashairi” na habari yenyewe inazungumzia kuhusu “mashairi.”

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo. Mtungo huo unaeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha. Hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa shairi unaohusika. Muundo maalumu ndio unaoletea shairi utamu unaotakiwa.

   Ushairi ni kazi au namna ya kutunga mashairi na kipengele chenyewe kinachoundwa na mashairi.

2. Mashairi ya Kiswahili ya mwanzoni (kabla ya karne ya pili BK) hayakuwa na utaratibu wa vina, mizani na beti kama ilivyo katika mashairi ya kisasa. Mashairi ya siku hizo yalifanana sana na nyimbo kwani ndizo zilizokuwa chimbuko lake.

3. Kutokana na kazi alizokuwa akifanya, binadamu alianza kutunga maneno na sauti za muziki zilizokuwa zikifuata mapigo ya kazi. Wimbo wa kazi ukawa ndio utanzu wa fasihi wa mwanzo. Polepole, ushairi wa Kiswahili ulianzishwa kwa kuiga mapigo ya nyimbo.
4. Mabadiliko mengi ya kimaudhui yalifanyika wakati wa majilio ya Waarabu sehemu za pwani ya Afrika ya Mashariki.
5. Mashairi ya Waarabu yalikuwa na beti, mizani, vina na maudhui ya kidini.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kila mwanafunzi atege sikio mwenzake kisha aandike mawazo makuu ambayo ameazingatia.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma mara nyingine kifungu cha habari kutamsaidia kukielewa akielekezwa na mwalimu.

Kazi ya 6:

Bwana huyu anajigamba. Majigambo ni mojawapo kati ya mashairi ya Kiswahili. Habari yetu nayo inazungumzia kuhusu mashairi.

Kazi ya 7

1. Kwa kawaida, mashairi hutungwa kwa lugha nzito, lugha ya ishara na mafumbo inayoeleweka na wanajamii wanaohusika.
2. Wanafasihi wengi wanaamini kuwa ushairi huo ni zao la jamii ya Waswahili lililokuwepo tangu karne ya pili Baada ya Kristo (BK).
3. Mtu hujisifu kutokana na matendo yake ili wengine wamwogope na wamheshimu kwa ujasiri wake.

Kazi ya 8:

Kusoma kwa sauti na ufasaha sentensi husika kutawasaidia kuelewa umuhimu wa mashairi katika jamii.

Kazi ya 9:

- Kusoma ubeti;
- Katika ubeti huu, burudani tunayoipata ni kichekesho juu ya kupumbazwa kwa mtoto wa tajiri kwani shairi hili ni la watoto na linalenga kuburudisha, kufurahisha na kuchekesha hadhira.

Kazi ya 10:

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa ufasaha ubeti husika na kuzingatia burudani wanayoipata.

**D. Msamiati**

Kazi ya 11:

Muwala: Uwiano wa vipengele vya kisanaa na maudhui katika ushairi
Ustaarabu: Hali ya kustaarabika au kuwa na vitendo, tabia na mwenendo unaolingana na maadili ya jamii inayohusika
Sime: Kisu kikubwa chenye makali pande zote mbili

Kazi ya 12:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake / Mfano: Muwala ni uwiano wa vipengele vya kisanaa na maudhui katika ushairi.

Kazi ya 13:

1. Mashairi waadhi / nyaadhi hutoa maonyo kuhusu nasaha njema.
2. Walinzi wa Mbuga ya Wanyama ya Akagera walilikimbiza kundi la majangili kumi.

Kazi ya 14:

| Maneno | Kikundi cha shughuli za kijamii ambamo mashairi huweza kutungwa | Kikundi cha mambo mengine |
|---|---|---|
| Jando<br>Wanafasihi<br>Mshairi<br>Unyago<br>Msiba<br>Uyoga<br>harusi | Jando<br>Unyago<br>Msiba<br>Harusi | Wanafasihi<br>Mshairi<br>Uyoga |

Kazi ya 15:

1. Gonyau // Unyago
2. Ngimalija // Majangili
3. Kumiki // Mikuki
4. Omwekele // Mwelekeo

Kazi ya 16:

**Mfano:**

Elimu ndio ufunguo, katika maisha yetu,
Wenyewe si mshang'ao, kumbabaisha mtu,
Kama hukugusa bao, bado una thamani tu,
Lakini taabu kwako, zitakuwa haziishi.

Mambo mengi duniani, huongozwa na elimu,
Kama gogo asilani, nyenzo kwake yalazimu,
Kama uti mgongoni, elimu kitu muhimu,
Hewani hata majini, elimu kitu lazima.

Kurusha eropleni, mwanadamu ameweza,
Kavumbua na miwani, macho yake kugeuza,
Akiwemo mitamboni, sayari huqeza kuza,
Elimu hazina safi, mwizi hawezi kuiba.

(Benjamin Nashon Magawi)

Kazi ya 17:

Kila kundi lina kazi yake.

Kazi ya 18:

1. Mashairi huweza pia kuliwaza mtu wakati wa majonzi.
2. Tendo la kuhamasisha wanajamii hufanyika katika shughuli mbalimbali.
3. Ushairi simulizi wa Kiswahili kama utungo unaotumia lugha ya Kiswahili hueleza maisha ya Waswahili yaani wenyeji na watumiaji wa lugha hiyo

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 19:

Kutoa muhtasari kusisitizwe kwa kila mwanafunzi.

Kazi ya 20:

<table>
<tr><td>Kusaidia</td><td>kuelimisha</td><td>hadhira</td><td rowspan="5">ni mojawapo kati ya dhima za ushairi wa Kiswahili</td></tr>
<tr><td>Kusaidia</td><td>kukuza</td><td>kipawa</td></tr>
<tr><td>Kusaidia</td><td>kudumiasha</td><td>utamaduni</td></tr>
<tr><td>Kusaidia</td><td>kuburudisha</td><td>hadhira</td></tr>
<tr><td>Kusaidia</td><td>kuelimisha</td><td>jamii</td></tr>
</table>

Kazi ya 21:

Kueleza na kushughulikia msamiati uliotumiwa kalika beti husika kuzingatiwe.

Kazi ya 22:

| | |
|---|---|
| 1. Mashairi yaliyokuwa yakitungwa enzi hizo hayakuwa | kama haya ya kisasa |
| 2. Nyimbo | hugawanyika katika makundi mbalimbali |
| 3. Muundo maalumu ndio unaoletea shairi | mvuto usio wa kawaida |

**F. Mdahalo**

Kazi ya 23:

Kila kundi lina maoni yake

**G. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 24:

Klia mwanafunzi atoe kichekesho kingine.

**H. Kuandika**

Kila mwanafunzi atoe.

Kazi ya 25:

Kila mwanafunzi atunge shairi lake.

Kazi ya 26:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 27:

“Mti unaponyauka,
Nyasi nazo hukauka.
Nchi kavu huwa uchi,
Nyika huwa kame.
Ukame ukamatanapo,
Viumbe hustaajabustaajabu.

Hulia bila ufanisi,

Maskini,

Kufa ni lazima.

Kazi ya 28:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mashairi | ya | simango | ni | mojawapo kati ya vipera vya ushairi wa Kiswahili |
| Mashairi | ya | waadhi | ni | |
| | | majigambo | | |
| | | ......... | | |

Kazi ya 29:

Wazo kuu ni “kuwahamasisha wanawake kujikomboa.

# SOMO LA 9: AINA ZA SENTENSI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

**Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la tisa.**

| | | |
|---|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kubainisha aina za sentensi za Kiswahili | |
| Vipindi: | 7 | |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -sarufi na matumizi ya lugha; -Tathmini kuhusu sura | |
| Tathmini: | Tathmini endelezi na upimaji wa kiujumla | |
| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
| Kuzingatia aina za sentensi za Kiswahili | -Kufurahia kujua kuainisha sentensi za Kiswahili | -Kutunza mazingira<br>-Uzalishajimali |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Tunaona:

- Panya anayesema “Ng’ombe wangu,...”;
- Wachungaji ng’ombe na ng’ombe wao.

Kazi ya 2:

Picha inatuonyesha wachungaji ng’ombe na ng’ombe wao pamoja na panya. Na katika kifungu cha habari linalozungumziwa ni panya aliyefunga ng’ombe wa Mfalme na kukatalia wachungaji wake kuwarudisha kwa Mfalme.

### A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 3:

1. Habari hii ni hadithi simulizi ambayo ni ngano kwa sababu wahusika wake ni wanyama na binadamu.

2. Jambo lililosababisha mawasiliano kati ya MFALME na MBWA wake ni kitendo cha panya cha kuwafungia zizini kwake ng’ombe wa Mfalme walipoyavamia na kuyaharibu mashamba ya KABEBA.
3. Ili wachungaji na MFALME wasije wakawachukua ng’ombe wake, Mheshimiwa PANYA aliwafungia zizini na kutisha wachungaji kila mara walipojaribu kuja kuwachukua ng’ombe wa Mfalme. Maneno ya kuwatisha yalikuwa haya “Ni kweli kuwa ng’ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini siyo bila sababu. Ng’ombe hawa wanatoka kwa BUCYANA. Mheshimiwa huyu ni Bwana Mwenda-mbio na Mwenda-pole-na-taratibu, Bwana Mkubwa wa juu mbinguni ambaye anaweza kuwakata, bila kusita, vidole vyenu vidogo ambavyo vingetawanyika ardhini, Bwana ambaye angewapakulia ugali ambao kila anayekula kufumba na kufumbua ungemnenepesha”.

4. MBWA alipowarudisha ng’ombe wa Mfalme, MFALME alimfanyia sikukuu MBWA wake kwa kutimiza ahadi yake na kumchinjia ndama dume.

5. “Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu“. Kauli hii inamaanisha kuwa kuwa na uwezo wa kujilinda siyo kushinda. Ni kusema kwamba wachungaji wa ng’ombe wa Mfalme walikuwa na mikuki na silaha nyingine za kutumia ili kujilinda na kupigania ng’ombe wa Mfalme lakini PANYA hakuwa na kitu chochote. Walakini, walipokuja kuwachukua ng’ombe hao, PANYA aliwatisha kwa kutumia ulimi wake tu na kuweza kuwakimbiza. Jambo hili linaonyesha kwamba kuwa na silaha siyo kushinda.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza kwa makini na kuyazingatia mawazo makuu

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma habari mara nyingine kutamsaidia mwanafunzi kuifahamu zaidi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anasoma habari na kuifahamu.

Kazi ya 6:

Picha inatuonyesha mbwa anayezungumza na Mfalme. Ng’ombe wa Mfalme walipofungwa na panya na kukataliwa kurudishwa nyumbani, mbwa ndiye aliyekubalia Mfalme kuwarudisha ng’ombe wao kutoka kwa panya. Mbwa na Mfalme wanazungumzia jambo hilo.

Kazi ya 7:

| |
|---|
| 1. MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa PANYA ili aulize yaliyotokea. |
| 2. Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng’ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini. |
| 3. Wachungaji waliposikia hivyo, walighairi na kukimbia bila kuangalia nyuma |

| 4. Ni kweli kuwa ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini siyo bila sababu. |
|---|

Kazi ya 8:

| Nchi aliyoitawala | Jina la mfalme unalolijua |
|---|---|
| Rwanda | Kigeli IV Rwabugili<br>Yuhi III Musinga |
| Burundi | MwambutsaI<br>Ntare IV Rugamba<br>Mwezi IV Gisabo |
| Uganda | Kabaka Mwenga<br>Edward Mutesa II |
| Swazi | Mswati III<br>Sobhuza II<br>Dzeliwe<br>Dlamini IV<br>Ngwane V |

**D. Msamiati**

Kazi ya 9:

**Zizi:** Aina ya boma au ua lililojengwa maalumu kwa kufugia mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi, punda, na kadhalika

Kwenda shoti: Kwenda mbio

Fahali: Ng'ombe dume

Kazi ya 10:

Kila jozi ina sentensi zake / Mfano: Watu tunajua kwamba fahali wawili hawakai zizi moja.

Kazi ya 11:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake / Mfano: Kwa kutunza na kulinda mazingira, serikali imeanzisha mpango mpya wa kupanda miti pembeni mwa barabara zote za mji wa Huye

Kazi ya 12:

1.Mtu mwenye woga hawezi kumwua nyoka.
2.Nchini Rwanda, ng'ombe huchungiwa zizini ili kutimiza ombi la serikali.
3.Nilipopata shoti ya faranga elfu hamsini, ndipo niliamua kumwajiri wa kampuni.

Kazi ya 13:

1.Sahani, kikombe, gilasi, kijiko ni vyombo
2.Chungwa, papai, parachichi, fenesi ni matunda

Kazi ya 14:

-Kidole cha gumba ;
-Kidole cha shahada ;
-Kidole cha kati ;
-Idole cha pete ;
-Kidole cha mwisho

Kazi ya 15:

| Neno | Neno lenye maana sawa na lile | Kinyume cha neno lile |
|---|---|---|
| 1. Mbio<br>2. Kunenepa | Kasi<br>Kuwanda | Pole<br>Kukonda |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 16:

Kuwaambia yaliyomo katika matini kusisitizwe kwa kila mwanafunzi.

Kazi ya 17:

1. Mimi binafsi nitafanya jitihada ya kuwarudisha ng'ombe wako.
2. Lakini, badala ya Bwana MBWA kuogopa na kwenda zake, akafanya hatua moja mbele.
3. Kufuatana na jambo hilo, Mheshimiwa Panya alikuwa amewafungia nyumbani kwake.
4. Basi ndipo MBWA aliichukua fimbo ya wachungaji na kuwarejesha ng'ombe katika maskani ya MFALME.

Kazi ya 18:

| | |
|---|---|
| 1. MFALME kusikia hivyo | alifoka kwa hasira. |
| 2. Watumwa wa Mfalme | waliamua kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwake |
| 3. MBWA alipomwamkia mara ya tatu, | Mheshimiwa PANYA aliruka na kumkaba shingo. |

**F. Sarufi na matumizi ya lugha**

Kazi ya 19:

- Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya KABEBA. // Sentensi sahili
- Ng'ombe hawa ni mali ya BUCYANA. // Sentensi sahili
- MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. // Sentensi changamano

**Linganisha mifano hiyo ya kwanza na sentensi hizi zifuatazo:**

- Mimi ninaona ua. // Tungo tata
- Kalisa amekanyaga mtoto. // Tungo tata
- Mtoto anakuja hapa. // Tungo nyoofu

Kazi ya 20:

Mimi ninaona ua:

-"Ua" yaani sehemu ya mmea inayochanua, aghalabu huwa ndiyo sehemu ya uzazi ya mmea;

-"Ua" yaani mzunguko au boma lililofanywa kwa miti, mabati, makuti,... aghalabu huwa nyuma ya nyumba

**Kalisa amekanyaga mtoto:**

-"Mtoto" yaani kiumbe kinachozaliwa na mtu;

-"Mtoto" yaani kisanduku kidogo kinachoingizwa katika kabati (mtoto wa meza).

Ni kusema kuwa tungo hizi zinatatanisha kutokana na maana yake.

Kazi ya 21:

Katika jozi, wanafunzi watafute sentensi zao kisha wazisomee wenzao.

Kazi ya 22:

S=Sentensi sahili

ST=Sentensi tegemezi

Kazi ya 23:

Kwa kawaida, sentensi huwa na maana moja tu na wazi. Sentensi hiyo huitwa "sentensi / tungo nyoofu."

**Mfano:** Mama analima shamba.

Lakini, sentensi inaweza kuwa na maana zaidi ya moja (maana zisipo wazi kabisa). Sentensi hii inaweza kueleweka hivi na vile na kila maana ikawa sahihi katika mazingira yake. Kutokana na utata huo, inaitwa "sentensi / tungo tata".

**Mifano:**

[Hakuna maua!] Mfano huu unaweza kuwa na maana ya "maua" kama "sehemu ya mmea inayochanua" au "hakuna faida". Huo ndio utata unaojitokeza.

## Kazi ya 24:

1.Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya KABEBA.

S

2.Kalisa amekanyaga mtoto.

S

3.PANYA aliruka na kuingia ndani ya nyumba yake.

S U S

4.MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea.

S U ST

5.Tulikuwepo alipoingia hospitalini.

S ST

## Kazi ya 25:

1.Dada amemeza vidonge vingi sana.

N T N V E

2.Mwalimu anafundisha Kiswahili na wanafunzi wanaandika maelezo yake.

N T N U N T N V

## Kazi ya 26:

1.Sentensi isiyojitosheleza kimaana na kutegemea sentensi nyingine ili kuleta taarifa kamili huitwa sentensi tegemezi.

2.Sentensi ambayo inajengwa na kitenzi kimoja na kujitosheleza kimaana huitwa sentensi sahili.

3.Sentensi ambazo huwa na virejeshi vyenye dhana za masharti ambayo yamejikita katika mofimu za -nge, -ngeli- na -ngali- huitwa sentensi shurutia.

## Kazi ya 27:

Kulinganisha majibu na maelezo yaliyotolewa kuzingatiwe.

**G. Kuandika**

Kazi ya 28:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 29:

"Alikuwa na nia ya kuwauza ili kuboresha kazi zake za uzalishajimali". Kauli hii inalenga kuzalisha mali na kauli inayosomeka kwenye picha inaunga mkono hiyo ya kwanza kwani inasema, "Wekeza pesa yako, kuza mtaji na upate faida kubwa."

Kazi ya 30:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Wachungaji walijitahidi kuwatafuta ng'ombe hao | kama walivyokuwa wamefanya wengine |
| 2. Alipofika huko, alimwamkia | moja kwa moja hadi nyumbani kwa KABEBA |
| 3. Naye MFALME alimfanyia sikukuu MBWA wake | lakini hawakuwaona |
| 4. Wachungaji waliposikia habari hiyo, waliamua kwenda | kwa kutimiza ahadi yake |

**TATHMINI KUHUSU SURA YA KWANZA**

**Kusoma maswali na kutoa majibu:**

1. Fasihi simulizi ni hazina ya kazi za kubuni za sanaa inayotumia lugha yaani maneno kama njia ya kuwasilisha mambo yake.
2. "Nadharia ya msambao": Waasisi wa nadharia hii niJacob na Wilhem Grimm. Baadaye mawazo yao yaliendelezwa na Maxmuller na Mmarekani Stere Thomson. Licha ya tofauti ndogondogo, wataalamu wa nadharia hii wanaamini

kwamba chimbuko la fasihi simulizi ni moja lakini kutokana na maingiliano ya kijamii, fasihi simulizi ilisambaa hasa kutoka jamii zilizostaarabika (Ulaya) kuja katika jamii zisizostaarabika (Afrika). Baadhi yao walisema kuwa hadithi simulizi zilisambazwa na makundi ya wahamiaji kutoka India na kufika huko Magharibi kwa njia ya msambao.

3. Mdhamini ndiye anayeainisha nyanja za kufanyia utafiti, aula za utafiti na watafiti wenyewe. Ndiye anayetoa fedha na nyenzo za utafiti na kupokea matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, mtafiti analazimishwa kuwa karagosi wa mdhamini na matokeo ya utafiti yataathiriwa na mawazo ya mdhamini.
4. (Kila mwanafunzi atatunga shairi lake).
5. Toa maana ya semi fupi hizi:

   -Kuponda raha: Kuishi kwa furaha na amani

   -Kuona cha mtemakuni: Kupata mateso

   -Jogoo la shamba haliwiki mjini: Yeyote aliye ugenini inampasa kufanya mambo kwa tahadhari ili kulingana na mazingira ya hapo

   -Uchungu wa mwana aujuaye mzazi: Mwenye kuthamini kitu chochote kile ni yule mwenye kitu hicho kwani ndiye aliyetaabika katika kukitafuta na kukipata
6. Tegua vitendawili hivi:

   -Hazikauki umande // Pua za mbwa

   -Mtoto ana ndevu mzazi hana // Hindi

   Kuainisha sentensi:

1.Tungepata bomba za kutosha, tungekunywa maji safi. (Sentensi shurutia)

SSH

2.Wanyarwanda walifurahi waliposikia serikali yao imeunda mikakati thabiti ya kutunza

S ST S

mazingira. (Sentensi changamano)

S

3.Viongozi wote ulimwenguni ni watumwa wa raia. (Sentensi sahili)

s

4.Wanafunzi hawa wakisoma kwa bidii watafaulu mtihani wa taifa. (Sentensi shurutia)

SSH S

5.Walioshindwa si wanafunzi wa shule yetu. (Sentensi changamano)

ST S

6.Walimu wetu wasingalikuwa na muda wa kutosha wasingaliweza kutusaidia

SSH

katika kazi zetu. (Sentensi shurutia)

SSH

# SURA YA 2:

## FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI

Sura hii inaundwa na vipengele vinne vinavyohusiana na muhtasari, fani na maudhui. Kipengele cha kwanza kinahusu Muhtasari au ufupisho wa habari na mbinu mbalimbali zinazotumiwa ili uwe mzuri. Kipengele cha pili kinashughulikia maudhui katika uchambuzi wa hadithi yaani mambo mbalimbali ambayo yanatiliwa mkazo katika uchambuzi huo. Kipengele cha tatu kinatoa maelezo kuhusu fani katika uchambuzi wa hadithi na kutoa orodha ya mambo yanayoshughulikiwa katika uchambuzi huo. Kipengele cha mwisho kinaundwa na mfano wa uchambuzi uliotolewa kwa kuzingatia fani na maudhui yaani uchambuzi wa kina.

### MAANDALIO YA SOMO

Mfano wa maandalio ya masomo kuhusu sura hii ni huu ufuatao:

Jina la shule: **SHULE YA SEKONDARI YA KABAYA**

Jina la Mwalimu: **KAMALI Peter**

| MAANDALIO YA SOMO | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shule: | | | | Jina la mwalimu: | | | |
| Muhula wa | Tarehe | Somo | Kidato cha | Sura ya | Somo la | Muda | Idadi ya wanafunzi |
| Kwanza | 20/04/2016 | Kiswahili | Tano | pili | 1 kwa 10 | Dakika 80 | 30 |
| Makundi ya wanafunzi wenye matatizo ya kielimu na idadi yao:<br>1. Wanafunzi wenye matatizo ya kusikia: 2<br>2. Wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu: 4 | | | | | | | |
| Mada kuu: | Uhakiki na uwasilishaji katika fasihi simulizi | | | | | | |
| Mada ndogo: | Fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika mada: | Mwishoni mwa sura hii, mwanafunzi ataweza:<br>• Kusikiliza, kusoma, kwandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili. | | | | | | |
| Kichwa cha somo | Maana ya uhakiki na vipengele vyake katika fasihi simulizi | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika somo | Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi ataweza:<br>• Kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. | | | | | | |
| Mahali pa kufundishia | Darasani | | | | | | |

| | |
|---|---|
| Malengo ya kujifunza (Ni lazima yazingatiwe mahitaji ya wanafunzi) | Maarifa na ufahamu:<br>☐ Kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi ;<br>☐ Kuonyesha uwezo wa kuwasilisha mada inayohusiana na uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi;<br>☐ Kuelezea hadharani maoni yake kuhusu utanzu wa fasihi simulizi aliousoma au kuusikiliza darasani kwa kueleza alichofurahia, aichochukia, alichojifunza na kadhalika;<br>☐ Kukumbuka mambo muhimu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili.<br><br>Stadi:<br>☐ Kutumia vipengele vya fani na maudhui katika kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi simulizi.<br>☐ Kutathmini ubora wa utanzu wa fasihi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui;<br>☐ Kuwasilisha mbele ya darasa uchambuzi wa utanzu wowote wa fasihi simulizi;<br>☐ Kulinganisha utanzu mmoja na utanzu mwingine kwa kueleza kufanana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui;<br>☐ Kujadili matumizi ya lugha hususan tamathali za usemi zinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi kama vile masimulizi na mazungumzo;<br>☐ Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake.<br><br>Maadili na mwenendo:<br>☐ Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi;<br>☐ Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mwingine bila ugomvi wowote;<br>☐ Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika utanzu ulioshughulikiwa;<br>☐ Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. |
| Vifaa vitakavyotumiwa | Vitabu vya fasihi, magazeti, kazi za sanaa zilizorikodiwa, mtandao wa intaneti, ubao, chaki, kalamu na kifutio |
| Vitabu vitakavyotumiwa | Kitabu cha Mwanafunzi<br>Mwongozo wa Mwalimu<br>Vitabu vingine vinavyohusu uhakiki, utoaji wa maoni binafsi na utoaji wa mhadhara. |

| Muda na hatua | Mbinu za kufundishia na kujifunzia<br><br>Kwa kupitia kazi za kutafakari picha, kusikiliza, kusoma, kuzungumza, kujadili na kuandika katika makundi au jozi au kwa mwanafunzi peke yake au michezo, wanafunzi wataweza kuelewa vizuri fasihi ya Kiswahili, kusoma kazi mbalimbali za fasihi na kuwaambia wengine yale ambayo ameyasoma. | | Maarifa pamoja na Masuala mtambuka |
|---|---|---|---|
| | Wajibu wa mwalimu | Wajibu wa mwanafunzi | |
| Utangulizi<br><br>[Dakika 8=10%] | -Fuata maagizo yaliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi kama vile kuwaweka wanafunzi katika jozi au makundi mengine, kumpa mwanafunzi peke yake nafasi ya kujibu na kadhalika;<br>-Waache wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha iliyotumiwa;<br>-Wape wanafunzi dakika za kutosha za kuitafakari picha husika;<br>-Waulize wanafunzi wanachokiona kwenye picha iliyotumiwa.<br>-Waongoze katika kutoa maoni yao;<br>-Baada ya kutoa maoni yao, tambulisha somo husika la leo ambalo ni "Mazingira ya hospitali, vifaa na wafanyakazi". | -Wafuate maagizo yaliyotolewa katika Kitabu chao kama vile kujigawa katika jozi au makundi mengine, kila mwanafunzi kujibu maswali peke yake na kadhalika;<br>-Waitafakari picha kwa makini;<br>-Watoe maoni yao kwa sauti kuhusu picha iliyotumiwa. | Maarifa:<br>- Kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi ; Kuonyesha uwezo wa kuwasilisha mada inayohusiana na uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi; Kuelezea hadharani maoni yake kuhusu utanzu wa fasihi simulizi aliousoma au kuusikiliza darasani kwa kueleza alichofurahia, aichochukia, alichojifunza na kadhalika; Kukumbuka mambo muhimu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili<br><br>Stadi:<br><br>- Kutumia vipengele vya fani na maudhui katika kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi simulizi; Kutathmini ubora wa utanzu wa fasihi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui; Kuwasilisha mbele ya darasa uchambuzi wa utanzu wowote wa fasihi simulizi; Kulinganisha utanzu mmoja na utanzu mwingine kwa kueleza kufanana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui; Kujadili matumizi ya lugha hususan tamathali za usemi zinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi kama vile masimulizi na mazungumzo; Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Upeo<br><br>[Dakika 60=75%] | -Waambie wanafunzi wengine wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Baada ya kukisoma kifungu cha habari, wanafunzi wahusishe yaliyomo na ujumbe unaotolewa na picha ile;<br>-Mwambie mwanafunzi mmoja asimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzake yale ambayo ameyasoma.<br>-Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi yaliyopangwa na kutoa majibu yao;<br>-Jadiliana na wanafunzi kuhusu majibu yao au matokeo ya kazi wanazozifanya. | -Wasome kifungu cha habari kwa sauti;<br>-Wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Waige matamshi sahihi ya maneno mbalimbali na kiimbo kinachofaa;<br>-Wahusishe yaliyomo katika kifungu cha habari na ujumbe wa picha iliyotolewa;<br>-Wasimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzao yale ambayo wameyasoma;<br>-Wafanye kazi mbalimbali zilizopangwa;<br>-Wajadiliane na wenzao kuhusu majibu ambayo wameyapata au matokeo ya kazi ambazo wamefanya na kuyalinganisha majibu yote yaliyotolewa. | Maadili na mwenendo mwema:<br><br>- Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi; Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mwingine bila ugomvi wowote; Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika utanzu ulioshughulikiwa; Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika.<br><br>Masuala mtambuka yanayoshughulikiwa:<br><br>-Uzalishajimali,<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu,<br>- Mafunzo kuhusu mpango wa kuboresha uzazi<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI |
| Mwisho<br><br>[Dakika 12=15%] | -Waongoze wanafunzi katika kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Waachie wanafunzi kazi ya nyumbani | - Kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Washiriki katika zoezi ambalo limetolewa;<br>-Waandike katika daftari zao kazi ya nyumbani ambayo imetolewa na mwalimu. | |

| | |
|---|---|
| Tathmini ya mwalimu | Kutokana na maoni yake kuhusu jinsi wanafunzi walivyoshiriki katika somo lake, mwalimu achunguze jambo la kutilia mkazo hususan pale ambapo wanafunzi wamekutana na matatizo mbalimbali |

# SOMO LA 10:

# UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI NA VIPENGELE VYAKE

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuelewa na kuelezea uhakiki katika fasihi</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">6</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Mchezo</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
<tr><td>Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili.</td><td>-Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika.</td><td>-Uzalishajimali,<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu,<br>- Mafunzo kuhusu mpango wa kuboresha uzazi<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI</td></tr>
</table>

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Nadharia ni maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Uhakiki ni dhana ya kueleza na kuchunguza kwa makini kazi ya sanaa. Kwa hiyo, “nadharia ya uhakiki wa fasihi” ni maelezo yanayohusu kueleza na kuchunguza fasihi.

Kazi ya 2:

Kwenye picha kumeandikwa “Nadharia za uhakiki wa fasihi” na jambo hilo ndilo linaloshughulikiwa katika matini yetu.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.
2. Uhakiki wa kazi za fasihi ni mkongwe kwa sababu kuwepo kwake kulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine.
3. Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi vinavyoshughulikiwa ni maudhui na fani.
4. Maudhui hujumuisha vigezo kama vile kichwa cha habari, dhamira (kuu na ndogondogo), ujumbe, falsafa ya mtunzi, migogoro na muhtasari wa habari. Fani huundwa na wahusika, muundo, mtindo au matumizi ya lugha na mandhari.
5. Dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi katika maisha ya mwanafunzi ni:

-Kumwezesha kuielewa, kuieleza na kuifaidi kazi ipasavyo;
-Kumwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi;
-Kumwezesha kuchambua na kufafanua mifumo na picha za kisanaa zinazotumika katika kazi za fasihi ili kupevuka katika lugha;
-Kumwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi. Maonyo hayo tunaweza kuyatumia kwa kuwa kosoa wanajamii wengine.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kutega sikio na kuandika mawazo makuu
Mawazo makuu: (Uhakiki wa kazi za fasihi ni kongwe sana; Kuna vigezo mbalimbali vinavyozingatiwa katika kufanya uhakiki; Uhakiki una umuhimu fulani; Ukomavu, uwezo na mwenendo wa mhakiki ndizo nguzo za uhakiki)

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine kuzingatiwe.

Kazi ya 6:

Ninaogopa mnyama ambaye anaweza kuniua na kunila, siwezi kuogopa yale binadamu anayoyasema. Jambo hili linatokana na kuwa maneno hayawezi kuniua.

Kazi ya 7:

1. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.
2. Utunzi wa kazi ya fasihi si jambo la kubahatisha bali huongozwa na kaida maalum.
3. Uhakiki wa kazi ya fasihi huhitaji utafiti wa kutosha katika vitabu mbalimbali, kwenye mtandao wa intaneti na mahali pengi.

Kazi ya 8:

Kusoma kwa sauti na ufasaha kuzingatiwe.

**D. Msamiati**

Kazi ya 9:

**Ukongwe:** Hali ya kuzeeka

**Kutathmini**: Kutia kitu thamani; kuthamini
**Tajiriba:** Uzoefu mtu alio nao katika kutenda jambo
**Kuadhiri:** Kuvunjia heshima; kuaibisha
**Janga:** Balaa; hatari; tabu

Kazi ya 10:

Kila jozi ina sentensi zake /Mfano: Uzoefu mtu alionao katika kutenda jambo huitwa tajiriba.

Kazi ya 11:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake / Mfano: katika historia ya Wanyarwanda, tuna vitendo vingi vinavyolenga amani na maendeleo ya nchi.

Kazi ya 12:

1.Tajiriba
2.Anayoitamalaki
3.Vigezo

Kazi ya 13:

-Huitwa "wahusika."
-Hushughulikiwa katika kipengele kinachoitwa "fani"

Kazi ya 14:

| Maneno | Fani | Maudhui | Mengine |
|---|---|---|---|
| Dhamira<br>Mshairi<br>Udongo<br>Mandhari<br>Wahusika<br>Chandarua<br>Mtindo | Mshairi<br>Mandhari<br>Wahusika<br>Mtindo | Dhamira | Udongo<br>Chandarua |

Kazi ya 15:

"Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika." Ni kusema kwamba kuna vipengele viwili vya uhakiki lakini vigezo vinavyoainishwa katika vipengele hivyo si sawa kwa tanzu zote. Kuna tanzu zinazofanyiwa uhakiki kwa kupendelea vigezo fulani na kuacha vingine. Vilevile, mtu anaweza kuchagua vigezo mbalimbali atakavyopendelea katika uhakiki wake kutokana na lengo analotaka kufikia. Lengo hili ndilo linalochukuliwa kama wajibu unaohitajika kutekelezwa au kazi fulani.

## E. Kuzungumza

Kazi ya 16:

Kuwaambia yale ambayo amesoma kuzingatiwe.

Kazi ya 17:

| | |
|---|---|
| Ubora wa uhakiki hutegemea | mwenendo wa jamii husika |
| Ubora wa uhakiki hutegemea | ukomavu wa mhakiki |
| Ubora wa uhakiki hutegemea | uwezo wa mhakiki |

Kazi ya 18:

-Nini: Ni kusema linalozungumziwa;
-Nani: Ni kusema anayesema au anayefanya kazi fulani;
-Vipi: Ni kusema namna gani jambo fulani linavyofanyika

Kazi ya 19:

| | |
|---|---|
| 1. Ukosefu wa uwezo hasa wa kifedha kwa mhakiki huwa | ni tatizo kubwa linalotatuliwa na mdhamini. |
| 2. Iwapo udhamini umekosekana, | kazi ya mhakiki haitafaulu |
| 3. Uhakiki hupangwa vizuri ili kuwa | mzuri vya kutosha. |

## F. Mchezo

Kazi ya 20:

-Ukomavu;

-Uhakiki;

-Ukimwi;

-Tajiriba;

-Kaida.

## G. Kuandika

Kazi ya 21:

(Kila mwanafunzi ana sentensi zake)

Kazi ya 22:

| | |
|---|---|
| Kazi za fasihi simulizi zinazoweza kufanyiwa uhakiki ni kama | hadithi |
| | methali |
| | nahau na misemo |
| | Vitendawili |

Kazi ya 23:

| |
|---|
| 1. Umri na elimu ni baadhi ya mambo ambayo huchangia sana katika kuboresha uhakiki wa kazi ya fasihi. |
| 2. Kulinganisha kazi za fasihi ndiko kunakotuwezesha kumtambua mtunzi bingwa au yule ambaye kazi yake ni legevu. |
| 3. Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika. |

Kazi ya 24:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Lengo la somo hili ni kueleza na kuchunguza | kujibu maswali kama vile kwa nini, nani na vipi |
| 2. Uhakiki huanza katika kitendo cha kujaribu kuielewa kazi ya fasihi na | kwa makini kazi ya fasihi |
| 3. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha tano, fanya mazoezi mengi | ili kupevuka katika kazi hiyo |

# SOMO LA 11: KUHAKIKI HADITHI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na moja.

| | | |
|---|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa hadithi simulizi za Kiswahili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususan tamathali za usemi | |
| Vipindi: | 8 | |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki | |
| Tathmini: | Tathmini endelezi | |
| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
| Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika hadithi simulizi za Kiswahili | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI (magonjwa mengi ya zinaa kama vile UKIMWI)<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza mali yako ili uweze kupata faida) |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Picha hii inaonyesha Nyambere na Mariya katika safari yao kuelekea kwa mumewe Mariya baada ya kufunga ndoa. Wanaambatana na viumbe vingine ambavyo ni mazimwi.

Kazi ya 2:

Picha hii inaonyesha Nyambere na Mariya katika safari yao kuelekea kwa mumewe Mariya baada ya kufunga ndoa. Wanaambatana na viumbe vingine ambavyo ni mazimwi. Na katika habari mambo yanayozungumziwa ni hayo hayo.

### A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 3:

1. Hadithi hii ni ngano kwa sababu wahusika wake ni binadamu wanaochanganywa na mazimwi.
2. "Mariya alikuwa msichana asiye na makini." Jambo linalodhihirisha kauli hii ni kwamba Mariya alipoelezewa habari hii, aliipuuza na kusema kwamba ni uvumi.
3. Watu walioambatana na mumewe Mariya katika safari yake kwenda kumchukua mchumba wake walikuwa vichaka. Vichaka hivyo vilikuwa vimegeuzwa na zimwi hilo kuwa watu.
4. Maajabu yaliyofanywa na mumewe Mariya ni kama vile:

-kujigeuza kuwa zimwi;

-kumkatakata Mariya vipande vipande wakati wa usiku na ilipofika asubuhi, kuviunga vipande hivyo tena na kumtengeneza Mariya;

-Kuning'inia kwenye paa;

-Kula mijusi kafiri ambayo haikupikwa;

-Kujigeuza kuwa kware na kadhalika.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza na kuzingatia mawazo makuu kuzingatiwe.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine mara nyingine kusisitizwe.

Kazi ya 6:

Kusoma kwa sauti na ufasaha kusisitizwe.

Kazi ya 7:

Jambo linalozungumziwa ni “Fanyeni uhakiki wa hadithi”. Uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.

**D. Msamiati**

Kazi ya 8:

**Dondoo:** Tabia ya uzinifu; uzinzi

**Uchumba:** Makubaliano ya pande mbili baina ya mwanamke na mwanamume wanaotaka kuoana

**Mkwe:** Jina la heshima aitwalo baba, mama, au ndugu wa mzazi ambaye mtoto wake ameoa au kuolewa na mtu fulani wa mtoto huyo; mcheja

**Kichaka:** Mahali penye miti mifupimifupi na nyasi, miiba na kadhalika; kituka

Kazi ya 9:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake / Mfano: katika utamaduni wa Wanyarwanda, mama mkwe hawezi kuchangia chakula na mkwe wake.

Kazi ya 10:

1.Fuata njia nyembamba ili kufika kwenye kituo cha kuboresha uzazi. [Maana yake ni "njia finyu"]
2.Mchanga mwembamba hutumiwa katika kujenga nyumba za kisasa. [Maana yake ni "mchanga wenye ulaini"]
3.Watoto wanapaswa kunywa uji mwembamba ili wasije wakakumbana na maumivu ya tumboni. [Maana yake ni "uji mwepesi"]
4.Nyakati za sasa, watanashati wanapenda sana nguo nyembamba. [Maana yake ni "nguo zenye wororo"]

Kazi ya 11:

| |
|---|
| 1. Kumbe ilikuwa sauti ya kasuku aliyekuwa akiyarudia maneno ya Nyambere kabla ya kutoroka. |
| 2. Katika nchi ya mumewe kulikuwako na wanawake wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko. |
| 3. Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza kupaa juu akiwafuata Mariya na nduguye. |

Kazi ya 12:

| Maajabu yaliyofanywa na mumewe Mariya | Maajabu yaliyofanywa na Nyambere |
|---|---|
| -kujigeuza kuwa zimwi;<br>-kumkatakata Mariya vipande vipande wakati wa usiku na ilipofika asubuhi, kuviunga vipande hivyo tena na kumtengeneza Mariya;<br>-Kuning'inia kwenye paa;<br>-Kula mijusi kafiri ambayo haikupikwa;<br>-Kujigeuza kuwa kware na kadhalika. | -Kwa kutumia vijiti na nguvu zake za kichawi za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo;<br>-kunya mavi halafu mlima mrefu sana karibu kugusa mbingu ukatokea;<br>-kukojoa mkojo mkali na ikatokea bahari pana na yenye kina kirefu sana. |

Kazi ya 13:

"Damu nzito kuliko maji": Ni kusema kwamba ndugu ni ndugu tu hata kama wakigombana watapatana hawataweza kutengana kamwe.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 14:

Kuwaambia yale ambayo kila mwanafunzi amesoma kuzingatiwe.

Kazi ya 15:

"Zimwi likujualo halikuli likakwisha" [Maana yake ni kuwa watu wa jamii au ukoo mmoja hawadhuriani kabisa. Endapo wakifanya hivyo, basi huitwa wachawi lakini huendelea kuhesabika kuwa ni wa jamii au ukoo huo]

Kazi ya 16:

| | |
|---|---|
| Mkwe | ni jina la heshima aitwalo baba, mama au ndugu wa mzazi ambaye mtoto wake ameoa au kuolewa na mtu fulani wa mtoto huyo |
| Kilembwekeza | ni mtoto aliyezaliwa na kilembwe |
| Binamu | ni mtoto wa ndugu wa kiume wa baba |
| Ami | ni ndugu wa kiume wa baba |

Kazi ya 17:

| | |
|---|---|
| 1. Mariya na Nyambere waliendelea na safari yao | wakiambatana na watu wa jamii yao. |
| 2. Kuning'inia kwenye paa | kulimfanya aonekane kama popo. |
| 3. Walikwenda na gari la abiria | na kufika mahali walikozaliwa |

**F. Utafiti**

Kazi ya 18:

Kutafuta hadithi simulizi ya Kinyarwanda na kuitafsiri

***Inkware n'inzoka***

Kera Inkware n'Inzoka zari incuti ebyiri z'akadasohoka zigakunda gusangira igicuma cy'urwagwa.

Umunsi umwe Inzoka yabwiye Inkware iti "hari icyo nabonye iyo tuganira kandi ndumva nshaka kukikubwira".

Inkware yarayisubije iti "Ngaho mbwira ncuti yanjye.

Inzoka irayibwira iti "Birangora cyane kumenya icyo utekereza ni ukuvuga ikikuri ku mutima. Ngaho fungura akanwa kawe ndebe ikirimo!"

Inkware yahise ifungura akanwa itazuyaje ariko nta kintu cyarimo.

Inkware na yo yakurikiyeho maze Inzoka ifungura akanwa Inkware irareba ibonamo akumba hirya ahagana mu nkanka.

Muri ako kanya umuriro uba uradutse mu ishyamba hanyuma inzoka ibwira Inkware iti "Urabona biriya birimi by'umuriro? Reka tugurukane utatugeraho." Igitekerezo k'Inzoka cyaremewe maze yizunguriza ku ijosi ryayo irayigurukana.

Zigeze aho zitekanye zarahagaze ariko inzoka yanga kujya hasi ahubwo itangira kuyiniga. Abantu ni bo baje kuyitabara maze bica ya nzoka.

Si jye wahera hahera umugani!

***Kware na nyoka***

Hapo zamani, Bwana Kware na Bwana Nyoka walikuwa majirani wawili wazuri sana na mara kwa mara walikutana mbele ya mtungi wa pombe.

Siku moja Bwana Nyoka akaeleza jirani yake Kware, "Kuna kitu ambacho nimekiona katika mazungumzo yetu ya kila siku na nimeona ni heri nikuelezee".

"Naam, nielezee tu rafiki yangu", akajibu Bwana Kware.

“Ninaona vigumu sana kujua undani wako yaani kilichoko rohoni mwako. Kwa hiyo, fungua kinywa chako ili niangalie kilichomo”, akasema Bwana Nyoka.

Kware alifungua kinywa bila kusita lakini hapakuwa na kitu chochote.

Sasa zamu ikawa yake Kware. Nyoka naye alifungua kinywa chake kisha Kware akachunguza vizuri na kuona kijumba kidogo katika sehemu ya ndani ya koo.

Punde si punde ukazuka moto humo msituni. Nyoka akamtahadharisha Kware, « Unaziona ndimi zile za moto ? Hebu turuke pamoja ili tuukwepe moto ule ». Nyoka alikubaliwa akajiviringisha shingoni mwa Kware wakaruka pamoja.

Mara baada ya kutua salama, Nyoka alikataa kuteremka chini na kuanza kulikaba shingo la Kware. Watu ndio waliokuja kumnusuru Kware kwa kumuua Bwana Nyoka.

Huu ndio mwisho wa hadithi !

**G. Kuandika**

Kazi ya 19:

Kubuni hadithi kuhimizwe kwa kila kundi.

Kazi ya 20

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

Kazi ya 21:

| | |
|---|---|
| Nyambere | yu miongoni mwa wahusika wakuu katika hadithi ya “Kasoroka” |
| Mariya | |
| Mumewe Mariya | |

Kazi ya 22:

1. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na kutetemeka ovyo.

| |
|---|
| 2. Basi Nyambere , kwa kutumia vijiti na nguvu zake za kichawi za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. |
| 3. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama angeweza kuolewa naye, alikubali bila kusita. |

Kazi ya 23:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Mariya alimwomba msamaha Nyambere | bali zimwi lililokuwa limejigeuza na kuwa binadamu |
| 2. "Mangera" ilipokuwa tayari wakati wa jioni, Mariya na Nyambere | waliingia ndani na kupaa juu kuelekea nchini mwao |
| 3. Mwanamume huyu alikuwa si mwanamume hasa, | kwa chuki aliyokuwa amemfanyia |

H. Uhakiki au uchambuzi wa hadithi "Nyambere"

(Kujikumbusha uhakiki wa hadithi)

Kazi ya 24:

Kuchagua hadithi simulizi ya Kiswahili na kuifanyia uhakiki kuzingatiwe.

Kazi ya 25:

Kuwasomea wenzao uhakiki na kujibu maswali kusisitizwe.

Kazi ya 26:

Kubadilishana hadithi na kuzifanyia uhakiki kusisitizwe.

# SOMO LA 12: KUHAKIKI METHALI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

**Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na mbili.**

| | | |
|---|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa methali za Kiswahili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi | |
| Vipindi: | 6 | |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki; -Utafiti; - Kucheka | |
| Tathmini: | Tathmini endelezi | |
| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
| Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika methali za Kiswahili | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | -Amani na maendeleo,<br>-Usawa wa jinsia,<br>-Uzalishajimali<br>-Mafunzo kuhusu maendeleo ya kudumu |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kumeandikwa “Fahali wawili wakipigana, nyasi huumia.”

Kazi ya 2:

Ni methali ya Kiswahili.

Kazi ya 3:

Kwenye picha kumeandikwa “Fahali wawili wakipigana, nyasi huumia”. Hii ni methali na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu “uhakiki wa methali”.

## A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 4:

1. “Methali huwa na maana ya nje na maana ya ndani au maana yenyewe”. Hebu tutoe mfano wa methali “Kidole kimoja hakivunji chawa”. Chawa ni kidudu kinachokaa kwenye mwili wa binadamu hasa katika nywele na nguo chafu na hunyonya damu yake. Ufafanuzi wake au maana yake ya nje ni kuwa mtu hawezi kumwua chawa kwa kidole kimoja. Ni lazima ambanie katikati ya vidole viwili. Maana yake ya ndani ni kuwa “mtu mmoja hawezi kufanya kazi inayohitaji watu wengi.”
2. “Methali huwa na mazingira yake”. Kila methali huelezea uwanja fulani wa maisha ya mtu kama vile ukulima, amani na maendeleo, usawa wa jinsia, uzalishajimali, burudani, uimbaji na kadhalika.
3. Methali hutambuliwa haraka kutokana na muundo na lugha yake.
4. Methali hizi huzungumzia uwanja (mazingira) gani ya maisha?
   - Mpanda farasi wawili hupasuka msamba // Ufugaji
   - Mchovya asali hachovyi mara moja // Chakula
   - Mbuzi wa maskini hazai mapacha // Ufugaji

## B. Kusikiliza

Kazi ya 5:

Wanafunzi wapewe fursa ya kusoma kifungu cha habari wenzao wakiwatega masikio kwa makini.

## C. Kusoma

Kazi ya 6:

Kusoma kwa makini kusisitizwe.

Kazi ya 7:

Hakuna jibu sahihi.

Kazi ya 8:

1. Ujumbe wa methali unapofafanuliwa kutokana na mazingira yake ndipo tunapata ufafanuzi wake na maana yenyewe ya methali.
2. Methali hutumia mbinu maalumu za lugha au za kishairi zinazochangia katika kukumbukika kwake.
3. Methali yetu hiyo inatufundisha kuwa “Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”..

**D. Msamiati**

Kazi ya 9:

**Mkizi:** Aina ya samaki wa baharini ambaye anaweza kuruka sana
**Utengano:** Hali ya kuweka mtu kando
**Udhaifu:** Hali ya kudhoofika au kutokuwa na nguvu au kuwa mnyonge
**Ukinzani:** Hali ya ukaidi; upinzani
**Ndwele (uwele):** Maumivu mwilini; ugonjwa
Kuganga: Kufanyia mgonjwa matibabu; kutengeneza kilichovunjika au kuharibika

Kazi ya 10:

Dunia ni mti mkavu wenye maajabu mengi. Linaloshangaza ni kuwa watu wake wengi hawapendi kushirikiana na wenzao. Wao husahau kwamba hawana budi kuutupilia mbali utengano ili waishi katika utengamano. Hawajui kwamba hali hii ni udhaifu kabisa! Unapowahamasisha kuhusu jambo hilo, wao hupinga na kuruka kama mkizi baharini. Ni kweli kuwa ukinzani huo ni kizuizi cha maendeleo yao binafsi na ya nchi zao. Kuepukana na jambo hili kunawezekana kwani dawa ya kuponya uwele huo haijakosekana. Ni lazima kila mtu arekebishe mwenendo wake na kufanya bidii ili kuganga yajayo.

Kazi ya 11:

1. Tembo hashindwi na mkonga wake.
2. Aisifuye mvua, imemnyeshea.
3. Bendera hufuata upepo.
4. Teke la kuku halimwumizi mwanawe

Kazi ya 12:

1.Angurumapo simba, mchezaji nani;
Usitukane wakunga na uzazi ungalipo;
Mwezi na mtembezi, giza na mwizi;
Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya13:

Kuwaelezea wenzake yale ambayo amesoma kupewe nafasi ya kutosha.

Kazi ya 14:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Shukrani | za | punda | ni | mashuzi |
| Fadhila | za | punda | ni | mateke |
| Fadhila | za | nyuki | ni | Moto |

Kazi ya 15:

| |
|---|
| 1. Methali hii inatumiwa kwa kuwaonya watu wafanye kulihali ili kuboresha maisha yao ya mbeleni |
| 2. Kuna methali za kale zinazotumia lugha ya kale na methali za kisasa zinazotumia lugha ya kisasa |
| 3. Methali, kama semi zenye busara, hutoa maadili mbalimbali katika maisha ya binadamu |

**F. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 16:

Kuwaambia wengine kichekesho kutiliwe maanani.

**G. Uhakiki**

Kazi ya 17:

**1.Cheche huzaa moto;**

**Mazingira:** Moto.
**Maana:** Kitu kidogo huweza kuleta madhara makubwa.
**Matumizi:** Methali hii hutumika kuwatahadharisha wale wanaodharau mambo madogo kwani huweza kusababisha madhara makubwa yasiyotegemewa.
**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (cheche) na (huzaa moto).
**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa.

**2.Chururu si ndo ndo ndo;**

**Mazingira:** Mvujo.
**Maana:** Jambo kubwa si sawa na jambo dogo.
**Matumizi:** Methali hii inahamasisha watu ambao wana juhudi katika kufanya kazi ndani ya jamii kuwa waongeze juhudi.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Chururu) na (si ndo ndo ndo).
**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni tanakali za sauti.

**3.Maskini na mwanawe, tajiri na mali yake;**

**Mazingira:** Mali.
**Maana:** Methali inamaanisha kuwa matumaini ya mtu maskini ni wa toto wake lakini matumaini ya mtu tajiri ni pesa zake.

**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote (awe tajiri au fukara) kuwa kila mtu ana matumaini yake yanayotokana na maisha aliyo nayo.
**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Maskini na mwa nawe) na (tajiri na mali yake).
**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni sitiari.

**4.Maneno mema humtoa nyoka pangoni;**

**Mazingira:** Usemi.
**Maana:** Utumiaji wa usemi mzuri humfanya mtu apate chochote anachohitaji.
**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote kuwa ni vizuri kuchagua maneno ya kutumia kabla ya kusema kwani uta mu wa maneno unamsaidia mtu kulifikia lengo lake.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Maneno mema) na (humtoa nyoka pangoni).

**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni tashhisi.

**5.Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia.**

**Mazingira:** Elimu.

**Maana:** Mzazi ndiye mwalimu wa kwanza wa mtoto. Ikiwa mtoto hakufunzwa na mama yake, dunia yenyewe itamfunza. Ni kusema kwamba ikiwa mtu anapuuza mashauri ya wa zazi wake, matatizo mbalimbali ambayo yatamfikia ndiyo yatakayomfunza.

**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote kuwa kupuuza ush auri wa wazazi wake huleta madhara mengi. Kwa hiyo, ni lazima kuzingatia mafunzo ya wazazi.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Asiyefunzwa na mamaye) na (hufunzwa na dunia).

**Lugha iliyotumiwa:**Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni sitiari.

### H. Utafiti

Kazi ya 18:

Kutafuta methali na kuzifanyia uhakiki kusisitizwe.

Kazi ya 19:

Wanafunzi watoe maoni yao wakijibu maswali yaliyoulizwa.

### I. Kuandika

Kazi ya 20:

| | |
|---|---|
| Chovya chovya | humaliza buyu la asali |
| Haraka haraka | haina baraka |
| Bandu bandu | huisha gogo |
| Bandu bandu | humaliza gogo |

Kazi ya 21:

| | |
|---|---|
| Methali hutambuliwa haraka kutokana na | muundo wake |
| | lugha yake |

Kazi ya 22:

| |
|---|
| 1. Ibilisi ni shetani, kiumbe kinachodhaniwa kutendea mabaya binadamu. |
| 2. Methali hutungwa kwa umbo maalumu kutokana na ufundi wa msanii. |
| 3. Uhakiki wa methali huzingatia vipengele vya maudhui na fani lakini kwa njia inayotofautiana na ile ya uhakiki wa hadithi. |

Kazi ya 23:

| **Kikundi cha A** | **Kikundi cha B** |
|---|---|
| 1. Kuganga ni kufanyia | bali ni binadamu mwenzako. |
| 2. Methali inamaanisha kuwa si kiumbe mwingine anayeweza kukufanyia mabaya | na kutokasirika kwani ujinga ndio chanzo cha yote. |
| 3. Methali hii inatumiwa kwa kumkumbusha mtu kutoshtushwa na maovu anayoweza kutendewa na yule aliyemfanyia hisani | mgonjwa matibabu au kutibu. |

# SOMO LA 13:

# KUHAKIKI VITENDAWILI VYA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo ambao unahusu somo hili la kumi na tatu.

| | |
|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa vitendawili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Vipindi: | 6 | | |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki; -Utafiti; - Kucheka | | |
| Tathmini: | Tathmini endelezi | | |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
|---|---|---|
| Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Amani na maendeleo ya kudumu |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kitanda

Kazi ya 2:

Habari inahusu uhakiki wa vitendawili na picha yenyewe inaonyesha bikizee anayekaa na watoto wakitega na kutegua vitendawili.

### A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 3:

1.Vitu vitatu vinavyorejelewa na fumbo la vitendawili:

Vyombo vya jikoni;
Matunda mbalimbali;
Aina za nguo;
Magonjwa;
Mimea;
Mashine na mitambo mbalimbali;
Sehemu za mwili na kadhalika.

2.Kwa kawaida, muundo wa vitendawili unajitokeza namna hii:

Hupitishwa baina ya pande mbili: upande unaotega kitendawili na upande unaokitegua.
Huwa na muundo maalumu wa kuendelezwa yaani utangulizi, swali (au jaribio) na jibu.

**Mtegaji** : Kitendawili!
**Mteguaji** : Tega!
**Mtegaji** : (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").
**Mfano** : Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
**Mteguaji** : (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").
**Jibu** : Nyota

Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huomba apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

3.Mbinu mbili za lugha zinazoweza kutumiwa katika vitendawili ni:

**Tanakali za sauti:** Ni matumizi ya neno linaloiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika yaani milio yake.
**Mfano:** Drrrrrrrrrrh mpaka ngambo" / [Buibui]";
**Sitiari:** Ni tamathali ya usemi inayolinganisha moja kwa moja vitu viwili bila kutumia viunganishi

4.Tegua vitendawili hivi:
Mchicha mzuri umechumwa na watu wa nje // Dada yangu
Anajipiga kisha analia // Jogoo
Nimpigapo mwanangu watu hucheza // Ngoma

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi wanafunzi wanavyosoma kifungu cha habari na kueleza yanayozungumziwa kuzingatiwe.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa sauti na makini na kuheshimu alama za uakifishaji kusisitizwe.

Kazi ya 6:

Konokono kaacha alama.

Kazi ya 7:

1. Vitendawili hutumia mbinu mbalimbali za lugha (au tamathali za usemi) ili fumbo lake liweze kuwa tamu.
2. Walakini, uhakiki wa vitendawili huwa tofauti kidogo na ule unaofanywa kwa habari mbalimbali zinazoingia katika kundi la masimulizi kama hadithi.
3. Vitendawili ni utanzu wa fasihi simulizi unaoweza kufanyiwa uhakiki.

**D. Msamiati**

Kazi ya 8:

**Mkungu wa ndizi:** Tawi la mgomba lenye ndizi (sehemu yote yenye ndizi)

**Mtemi:** Mtawala wa kienyeji katika sehemu fulani za nchi mbalimbali

**Buibui:** Mdudu anayetandaza utando wa kukamatia nzi na wadudu wengine

Kazi ya 9:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 10:

1. Kuku wangu katagia miibani
2. Babu anakojoa

Kazi ya 11:

1. Yeye anasuka mikeka lakini hulala chini / (Boga);
2. Saa yangu kila siku hutembea, ikisimama haitengenezeki tena / (Moyo).

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 12:

Kuelezea aliyoyasoma (mwanafunzi) kutiliwe maanani.

Kazi ya 13:

| | | |
|---|---|---|
| Konokono | kaacha | alama |
| Hazikauki | umande | |
| Chapanda mti | bila | mguu |

Kazi ya 14:

| |
|---|
| 1. Nikisimama anasimama, nikiketi anaketi, nikiondoka anaondoka |
| 2. Vitendawili kama fumbo la kuvutia la kisanii huwa na muundo wake, lugha yake na wakati wake |

**F. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 15:

Kuwaambia wanafunzi kichekesho kingine kusisitizwe kwa kila mwanafunzi.

**G. Uhakiki**

Kazi ya 16:

1.Mifugo ya babu imetafuna ukuta / Panya

**Kitendawili chenyewe:** [Mifugo ya babu imetafuna ukuta]
**Jibu:** [Panya
**Mazingira:** Ufugaji
**Lugha iliyotumiwa:** sitiari
**Aina yake:** Kitendawili sahili

2.Ng’ombe wangu huchungiwa mlimani / Chawa

**Kitendawili chenyewe:** [Ng’ombe wangu huchungiwa mlimani]
**Jibu:** [Chawa]
**Mazingira:** Ufugaji
**Lugha iliyotumiwa:** sitiari
**Aina yake:** Kitendawili sahili

**H. Utafiti**

Kazi ya 17:

Kutafuta vitendawili na kuvifanyia uhakiki kusisitizwe.

Kazi ya 18:

Wanafunzi washirikishwe kutoa maoni kuhusu kazi hiyo.

**I. Kuandika**

Kazi ya 19:

| | |
|---|---|
| Drrrrrrrrrrrrr | mpaka ngambo |
| Parrrrrrr | mpaka Maka |

Kazi ya 20:

| | |
|---|---|
| Vitendawili vya tanakali za sauti | ni vile ambavyo vinatumia tanakali za sauti |
| Vitendawili sahili | vitendawili vifupi vyenye muundo mwepesi kueleweka |
| Vitendawili mkufu | Huwa na vipande vinavyofuatana. Kila kipande huwa na uhusiano na kipande kilichotangulia |

Kazi ya 21:

| |
|---|
| 1. Mgeni wangu anapoingia humkaribisha vizuri sana lakini anapoondoka sipendi kumwangalia. |
| 2. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huomba apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. |
| 3. Vitendawili huwa na fumbo lililofumbwa na msanii na ambalo linapaswa kufumbuliwa. |

Kazi ya 22:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Urefu wa kitendawili, muundo wake na mbinu za lugha zinazotumiwa | lakini kulipopambazuka sikuuona |
| 2. Nimeanika mpunga wangu juani | mazingira ya mwanadamu na vinavyojulikana sana |
| 3. Fumbo hilo hurejelea vitu vinavyopatikana katika | ndiyo mambo yanayotuwezesha kuainisha vitendawili |

# MUHULA WA PILI

# SOMO LA 14: UHAKIKI WA NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na nne.

| | |
|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa nahau na misemo ya Kiswahili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi |
| Vipindi: | 6 |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki; -Utafiti |
| Tathmini: | Tathmini endelezi |

| | | |
|---|---|---|
| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |

| | | |
|---|---|---|
| Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika nahau na misemo ya Kiswahili | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | -Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (kuboresha maisha na mazingira ya binadamu)<br>-Elimu isiyo na ubaguzi |

**B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI**

Kazi ya 1:

Kwenye picha kumeandikwa “Misemo mipya” na “Nahau”.

Kazi ya 2:

Habari inahusu uhakiki wa nahau na misemo. Picha nayo inahusu mambo hayo yaani “nahau na misemo.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Nahau mbili zinazorejelea vitu vinavyopatikana katika mazingira ya mitambo mbalimbali na maana yake:

    -Kutia jeki = Kuinua au kusaidia mtu
    -Kupiga darubini = Kufanya uchunguzi

2. Vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa nahau na misemo kifani:

    -Muundo;
    -Lugha.

3. Toa maana ya nahau na misemo hii:
    -Kugonga mwamba = Kutofanikiwa
    -Kuwa na damu ya kunguni = Kuwa na bahati mbaya
    -Kuchapa maneno = Kubuni maneno ya uongo juu ya mtu
    -Kulea mtoto kwa hali na mali = Kulea mtoto vizuri uwezavyo
    -Mtu mwenye domo kaya = Mpayukaji ambaye hawezi kutunza siri

## B. Kusikiliza

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma (mwanafunzi) akifuata matumizi ya alama za uakifishaji kusisitizwe.

## C. Kusoma

Kazi ya 5:

Kusoma kwa sauti, ufasaha na makini kusisitizwe.

Kazi ya 6:

Kauli ile "Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika" ni methali.

Kazi ya 7:

1. Nahau huwa na kitenzi chake halisi (au maalumu) kinachotumiwa na kisichobadilika ilhali misemo haina kitenzi maalumu kwani huweza kutumiwa bila kitenzi au pamoja na kitenzi chochote anachokipendelea msemaji.
2. Fulani alikubali kuambatana naye shingo upande.

## D. Msamiati

Kazi ya 8:

**Mrija:** Chombo chenye uwazi ndani kinachotumika kufyonzea vitu viowevu au kutengenezea filimbi au kiko cha tumbaku; njia yoyote ya kujipatia faida ya binafsi kwa kuwanyonya wengine

**Kukonda:** Kuwa na wembamba wa mwili; kudhoofu

**Mtema kuni:** Mtu akataye kuni

Kazi ya 9:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 10:

1.Nahau;

2.Birika.

Kazi ya 11:

1.Kuwa pete na kidole = Kuwa marafiki sana
2.Kuvaa miwani = Kulewa sana

Kazi ya 12:

1.Kalisa alimtilia guu Yohana katika mapenzi yake na Nyiramana. Ni kusema kuwa alimchafulia mambo.
2.Kazi ile ya kuinua mitambo Ilimvunja kiuno / ilimvunja mgongo Ni kusema kuwa ilikuwa kazi ngumu ya kuchosha.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 13:

Kuwaelezea wanafunzi yale ambayo mwanafunzi mmoja amesoma kusisitizwe.

Kazi ya 14:

| | |
|---|---|
| Kubugia mchanga | ni kuanguka |
| Kupiga umaridadi | ni kuvaa vizuri |
| Kula chumvi nyingi | ni kuishi maisha marefu |

Kazi ya 15:

| |
|---|
| 1. Mazingira hayo ya mwanadamu ndiyo mazingira ya nahau na misemo |
| 2. John amepigwa kalamu kutokana na ulevi wake na kuchelewa kazi |

**F. Uhakiki**

Kazi ya 16:

1.Kupiga umaridadi

**Nahau yenyewe:** [Kupiga umaridadi]
**Maana yake**: [Kuvaa vizuri]
**Mazingira:** Mavazi
**Lugha iliyotumiwa:** kuongeza ukali wa maneno

2.Amekula chumvi nyingi

**Nahau yenyewe:** [Amekula chumvi nyingi
**Maana yake:** [Ameishi maisha marefu]
**Mazingira:** Chakula
**Lugha iliyotumiwa:** Sitiari

3.Kumwaga unga

**Nahau yenyewe:** [Kumwaga unga]
**Maana yake:** [Kufukuzwa kazi]
**Mazingira:** Chakula
**Lugha iliyotumiwa:** kupunguza ukali wa maneno na sitiari

**G. Utafiti**

Kazi ya 17:

Kutafuta nahau na misemo na kuifanyia uhakiki kusisitizwe.

Kazi ya 18:

Wanafunzi wahamasishwe kutoa maoni yao binafsi.

**H. Kuandika**

Kazi ya 19:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake.

Kazi ya 20:

| | |
|---|---|
| Unapomwona mtu akianguka , unaweza kusema kuwa | amebugia mchanga |
| Unapomwona mtu akifukuzwa kazi, unaweza kusema kuwa | amepigwa kalamu |

| | |
|---|---|
| Unapomwona mtu akiwa na mimba, unaweza kusema kuwa | ni mja mzito |

Kazi ya 21:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Vitu hivyo vyote ndivyo vinavyotumiwa ili kuleta maana nyingine | na kiguu na njia |
| 2. Nahau na misemo ni semi zinazoweza kutumia mbinu | badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika |
| 3. Maishani mwangu, siwezi kuandamana | 3. Maishani mwangu, siwezi kuambatana |

# SOMO LA 15: UHAKIKI WA NYIMBO ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na tano.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa nyimbo za Kiswahili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">8</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki; -Utafiti</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
<tr><td>Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika nyimbo za Kiswahili</td><td>-Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika.</td><td>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (Umoja na maridhiano)</td></tr>
</table>

# B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Tunaona Bwana na Bibi Harusi pamoja na waimbaji. Wanaimba wimbo uitwao "Kasha langu"

Kazi ya 2:

Picha inaonyesha waimbaji na matini inazungumza kuhusu nyimbo yaani kazi za sanaa za waimbaji

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Wazo kuu katika habari hii ni uhakiki wa nyimbo
2. Sifa mbalimbali zinazopewa kasha lile ni kama vile:

Ni la zamani;

Lina muundo wa kale (si wa kisasa);

Lina thamani kubwa kwani lilipatikana baada ya kulipa pesa nyingi;

Linapofunguliwa hutoa harufu nzuri ya waridi na karafuu;

Lina kifua kizuri kama zabibu tosa na tini;

Lina matiti mviringo kama ndimu;

Lina macho mazuri kama johari.

3. "Mviringo ndimu, zalowanda mwake kifuwani". Mtunzi anataka kusema kwamba matiti ya mpenzi wake ni mazuri tena mviringo kama "ndimu mviringo".
4. Licha ya umbile, sehemu nyingine za kasha anazozisifu msemaji ni kama vile kifua kizuri, matiti mviringo na macho mazuri kama johari.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi mwanafunzi anavyosoma kifungu cha habari kwa kuheshimu alama za uakifishaji kuzingatiwe.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingi kifungu cha habari kusisitizwe kwa wanafunzi wote.

Kazi ya 6:

Huu ni ubeti mmoja wa wimbo “kasha langu” ambao ulitolewa katika kifungu cha habari:

Kifuwa cha kasha hilo, zabibu tosa na tini, (X2)
Mviringo ndimu zalo,-wanda mwake kifuwani,
Mato johari (i)yalo,-umbiwa mwake usoni.

Katika ubeti huu, mtunzi anasema kuwa matiti ya mpenzi wake ni kama “ndimu mviringo”. Ndimu hizo “ziliwanda kifuani mwake”. Picha yetu inaonyesha “ndimu” yaani matunda yaliyozungumziwa na mtunzi wa ubeti.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7:

**Kasha:** Aina ya sanduku kubwa hasa hutumiwa kuwekea nguo au vitu vya thamani

**Tumbuu:** Chombo cha chuma kinachowekwa kwenye mhimili wa mlango na kutumiwa kwa kufungia

**Kitasa:** Chombo mfano wa kisanduku kidogo chenye komeo ndani kitumiwacho kwa kufungia mlango, sanduku, kabati na kadhalika

**Mkafuu:** Aina ya mti

**Kuwanda:** Kuwa nene; kunenepa

Kazi ya 8:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake / Mfano: Wanyarwanda wengi hutumia kitasa ili kujilinda dhidi ya majambazi wanaoweza kuzivamia nyumba zao.

Kazi ya 9:

| Maneno | Mimea au matunda | Vyombo |
|---|---|---|
| Ufunguo<br>tumbuu<br>Kasha<br>Waridi<br>Zabibu<br>Tini<br>Fuu<br>Ndimu | Waridi<br>Zabibu<br>Tini<br>Fuu<br>Ndimu | Ufunguo<br>tumbuu<br>Kasha |

Kazi ya 10:

| |
|---|
| 1. Embe tosa ni lile ambalo lingali gumu lakini linalokaribia kuiva. |
| 2. Kitasa ni kifaa mfano wa kisanduku kidogo chenye komeo ndani ambacho kinatumiwa kwa kufungia kama vile mlango au sanduku. |
| 3. Ndege huyo mkubwa kuliko tetere na mwenye rangi ya kijivu, weupe usiokoza na ambaye hula nafaka anaitwa njiwa. |

Kazi ya 11:

**Haradali (nyeupe au nyeusi):** Ni kali sana na hutiwa katika vyakula.

**Karafuu:** Hutiwa katika chakula au katika sigara au hufanyiza dawa.

**Jira**: ni bizari inayotumika katika upishi hasa wa pilau.

**Zafarani:** Ni majani ambayo huungia chakula kama vile biriani, halua,... lakini huweza kutumika katika kutengeneza wino.

**Uwatu:** Hutumiwa katika mkate au kama dawa ya tumbo la mwanamke.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 12

Wanafunzi wahamasishwe kuwaambia wenzao yale ambayo wamesoma bila ya kupotosha maana.

Kazi ya 13:

1.Kasha // (wingi wake ni “makasha”)
2.Waridi // (wingi wake ni “mawaridi”)
3.Njiwa // (wingi wake ni “njiwa”)

Kazi ya 14:

1. Mkafuu;
2. Kuwanda.

Kazi ya 15:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kasha muundo wa | kale | si muundo wa | kisasa |
| Kasha muundo wa | zamani | si muundo wa | leo |

**F. Uchambuzi au uhakiki wa wimbo ”Kasha langu“**

(Kuhakiki wimbo “Kasha langu”)

**G. Utafiti na uhakiki**

Kazi ya 16:

**Wimbo “Starehe” ni huu**

| | |
|---|---|
| 1<br>Hapa nilipo mimi, nipo kitandani<br>Starehe zimeniweka matatani<br>Kupona tena mimi haiwezekani<br>“Masela” wangu, ndugu zangu buriani<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>“Sua Side Scott Jenta” kwaherini<br>“Bongo Record” na Majani kwaherini<br>Hamtaniona tena duniani.<br>Sasa najuta, mwenzenu yamenikuta<br>Ibilisi amefanikiwa kunivuta<br>Sasa sijui wa kumlaumu nani<br>Kati ya nafsi yangu ama shetani!<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>Makongo na Jiteute, kwaherini<br>Mohaa na Azinia, kwaherini<br>Aaan haa, haaa, haaa<br><br>2<br>Saa saba juu ya alama saa nikiitazama<br>Nimeisha achana na jacky sasa namfuata Salama<br>Saa kumi na mbili nina “appointment” na “mademu” wawili<br>Achana na Lily ambaye tutakutana saa mbili<br>Jenny wa Mikocheni ambaye sasa hayupo tena duniani<br>Aliyekuwa akinisubiria pale Vatican kijiweni<br>Amina na Semeni tunakutana kwa Macheni<br>Na kila siku nawabadilisha tena kwa foleni<br>Huo ndio uliokuwa mwenendo wa maisha yangu<br>Mimi viwanja kujivinjari na machangu oh ooh | 3<br>Hapa nilipo mimi, nipo kitandani<br>Starehe zimeniweka matatani<br>Kupona tena mimi haiwezekani<br>“Masela” wangu, ndugu zangu buriani<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>Afande Sele Morogoro, kwaherini<br>Arusha wanaApollo, kwaherini<br>Hamtaniona tena duniani.<br>Sasa najuta, mwenzenu yamenikuta<br>Ibilisi amefanikiwa kunivuta<br>Sasa sijui wa kumlaumu nani<br>Kati ya nafsi yangu ama shetani!<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>“discipline Camp” na Wakushi, kwaherini<br>Sinza Star na Choka mbaya, kwaherini<br>Aaan haa, haaa, haaa<br><br>4<br>Kijana vipi, mbona hujagonga mlango<br>Jipange kwenye foleni mmoja mmoja ndio mpango<br>Ondoa mashaka, tiba bora haihitaji haraka<br>Subiri watibiwe wenzako nawe utafuata<br><br>5<br>Dokta mi nimekuja kufanya hitimisho<br>Naamini hii ndiyo itakuwa ngwe yangu ya mwisho<br>Dalili zinaonyesha nimeathirika<br>Ila nimekuja pima tu nipate uhakika |

| | |
|---|---|
| Niliona fahari ii yeah<br>Starehe mi nilizinyaia papara<br>Nilibadili “mademu’ kama vidaladala<br>Nikienda nimepanda hili, nikirudi lile<br>Nilitamani starehe zote nizitawale<br>Hata kumkumbuka Mola wangu ilikuwa ndoto<br>Nilitekwa na ulimwengu kumbe naukimbilia moto<br>Katika kubadili wasichana nilikubuhu<br>Nilitembea na watoto wa geti, machangu na masista duu<br>Ubaya kwamba kondomu sikuitambua<br>Kwa kujua kwamba ladha ya mapenzi itapungua<br>Kumbe nilikuwa ninapotea njia<br>Niliyoshauriwa mimi niliyapuuzia<br>Idadi ya wanawake ikawa lukuki<br>Ikafika kipindi wengine nikawa siwakumbuki<br>Ona, ona aa<br>Ona sasa yaliyonibusu kwa dada yake Bashiri<br>Nilisha msahau kama tulisha kutana kimwili<br>Nilivyomwona, nikamtongoza tena<br>Tena kwa mara ya pili<br>Ona sasa aa aah | Hebu cheki dokta nilivyokonda<br>Nimebakia mifupa, mwili umetapakaa vodonda<br>Vipele usiseme hii dalili ya umeme<br>Dalili ya umeme eeh<br><br>6<br>Oh acha woga hata malaria iko namna hii<br>Unaweza ukakonda kwa “typhoid” au “TB”<br>Ukinificha unahatarisha maisha<br>Ni bora kubainisha kipi kinakutisha, eeh<br><br>7<br>Homa za mara kwa mara kwangu hazikatiki<br>Kuharisha, kutapika mara sitini na mbili kwa wiki<br>Eh angalia hata nywele zilivyonyonyoka<br>Mabega yamepanda juu utasema yanachomoka<br>Ninao, ninao<br>(Subiri vipimo)<br>Ninao, ninao<br>(Usikate tamaa)<br>Ninao, ninao<br>Dokta usinipe moyo<br>Ni sawa unampa mfupa autafune kibogoyo<br>Duniani mimi sina umuhimu<br>Kuaga dunia napaswa inanilazimu<br>Ni bora nijue tu nielekee kuzimu |

| | |
|---|---|
| 8<br>“No, no”, hayo maamuzi ya ajabu<br>Nani ulimbukeni kujiua pasipo sababu<br>Maradhi ni kawaida kwa binadamu hilo ufahamu<br>Ni vema ungetulia upate majibu ya damu<br><br>9<br>Sasa kumbe we unaona mi nasubiri nini?<br>Ni bora tu niwahi kupumzika kaburini<br><br>10<br>Starehe mnazipenda ila mwisho wake mbaya<br>Wengi wameteketea kwa kuendekeza umalaya<br>Vipimo vinaonyesha ni kweli umeathirika<br>“i’m very sorry” kupoteza nguvu ya taifa<br>Ni vema kufanya ibada na kumrudia Mwumba wako<br>Kula vizuri, fanya mazoezi, pumzisha mwili wako<br>Ukizingatia haya utaishi kwa matumaini<br>“by the way”, unayo nafasi hebu jiamini | 11<br>Mbona aliyeniumba sasa nilisha mkosea<br>Hata ardhi na mbingu vyote vinanizomea<br>Malaika wa adhabu kwa hamu wananingojea<br>(Koh koh koh)<br>Nikifika huko nani atanipokea aah aa<br><br>12<br>Hapa nilipo mimi, nipo kitandani<br>Starehe zimeniweka matatani<br>Kupona tena mimi haiwezekani<br>“Masela” wangu, ndugu zangu buriani<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>Wa bara na visiwani, kwaherini<br>TMK, Kino Graid, kwaherini<br>Hamtaniona tena duniani.<br>Sasa najuta, mwenzenu yamenikuta<br>Ibilisi amefanikiwa kunivuta<br>Sasa sijui wa kumlaumu nani<br>Kati ya nafsi yangu ama shetani!<br>Kwaherini, kwaherini, kwaherini<br>Kikosi cha Mizinga, kwaherini<br>Migo Migo, Sinza, kwaherini<br>Aaan haa, haaa, haaa |

Kazi ya 17:

Kuwasomea wanafunzi wengine na kujibu maswali yahusuyo uhakiki ambao umefanywa kuzingatiwe.

Kazi ya 18:

Kutafuta nyimbo, kuziandika na kuzisomea darasa kusisitizwe.

**H. Kuandika na kuhakiki**

Kazi ya 19:

Kufanya uhakiki na kusoma matokeo ya kazi kuzingatiwe.

Kazi ya 20:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake.

Kazi ya 21:

Kubuni wimbo, kuufanyia uhakiki na kuutolea thathmini kusisitizwe.

# SOMO LA 16:

# KUHAKIKI MASHAIRI SIMULIZI YA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo ambao unahusu somo hili la kumi na sita.

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kufafanua vipengele vya fani na maudhui katika uhakiki wa mashairi ya Kiswahili<br>- kujadili matumizi ya lugha hususani tamathali za usemi</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">6</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Uhakiki; -Utafiti</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| Kuwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika mashairi simulizi ya Kiswahili | -Kuwa na utaratibu wa kuongozwa na tafakuri tunduizi.<br>-Kujivunia na kuutetea utamaduni wa mwafrika. | -Mafunzo kuhusu kuboresha uzazi<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza mali na kutegemea benki ili kuboresha maisha ya mtu) |

Kazi ya 1:

Kwenye picha, mwalimu anafundisha mashairi ya Kiswahili na, katika matini, linaloshughulikiwa ni uhakiki wa mashairi ya Kiswahili.

Kazi ya 2:

Mwalimu anafundisha mashairi na matini inahusu ushairi simulizi.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1.Mambo mbalimbali yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kimaudhui ni:

-Maisha ya mtunzi;
-Kichwa cha shairi;
-Aina ya shairi;
-Dhamira;
-Ujumbe au maadili;
-Falsafa au msimamo wa mshairi;
-Muhtasari kwa njia ya nathari.

2. Mambo hayo yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kimaudhui si sawa na yale yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kifani. Fani ya shairi inahusu mambo yafuatayo:

-Wahusika (ikiwa shairi linahusisha wahusika);
-Mtindo;
-Muundo au umbo la shairi;
-Uhuru wa mshairi.

3. Mambo yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa umbo la shairi ni:

-Idadi ya beti;
-Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
-Idadi ya vipande vya mstari;
-Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
-Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;
-Bahari ama mstari wa mwisho.Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa “kibwagizo” au “kiitikio”. Kama hakuna mstari wa mwisho unaorudiarudia, basi mstari huo utaitwa “kimalizio” au “kiishio”.

4. “Kuboronga sarufi” kunaleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi kila mwanafunzi anavyosoma kifungu cha habari akiheshimu alama za uakifishaji kuzingatiwe.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine kifungu cha habari kupendekezwe kwa wanafunzi wote.

Kazi ya 6:

Sawa na picha ya kwanza, picha hii inatuonyesha ukurasa wa kwanza wa kitabu ambako kumeandikwa “Ushairi: Nadharia ya Tahakiki”. Ni kusema kwamba linalozungumziwa ni sawa na lile linalozungumziwa katika kifungu cha habari yaani “mashairi ya Kiswahili”.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7

**Kuwekaza:** Kutia kitu mahali fulani kwa ajili ya manufaa ya baadaye.
**Ubeti:** Kifungu cha mishororo katika shairi.
**Mshororo:** Mstari katika shairi.
**Kina:** Silabi zenye sauti za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadha hususa katikati na mwisho wa kila mstari wa ubeti wa shairi.

**Kuboronga:** Kuharibu; kuvuruga.

Kazi ya 8:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake / Serikali ya Rwanda inahimiza wananchi kuweza mali yao na kutegemea benki ili kuweza kuwa na maisha bora.

Kazi ya 9:

Fani: Vina; Mishororo; Idadi ya beti
Maudhui: Dhamira; Ujumbe wa mtunzi; Muhtasari wa shairi

Kazi ya 10:

| |
|---|
| 1. Kuhakiki shairi kimaudhui ni kulichambua na kuweka wazi mawazo na mafunzo yote anayoyazungumzia mtunzi pamoja na mtazamo wake juu ya mawazo hayo. |
| 2. Ni vigumu kuwajua watunzi wa mashairi similizi ya Kiswahili kwani ni utanzu mkongwe sana. |
| 3. Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika kazi yake. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lake liwe na umbo fulani. |

Kazi ya 11:

1.Kuboronga sarufi ni njia moja msanii anayoitumia ili kuifanya sentensi yake iwe tamu.
2.Ni vigumu kuwajua watunzi wa mashairi ya fasihi simulizi.
3."Titi la mama li tamu" ni mojawapo kati ya mashairi ya kimapokeo.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 12:

Kuwaambia wengine yale ambayo kila mwanafunzi ameyasoma kusisitizwe.

Kazi ya 13:

| | |
|---|---|
| Kibwagizo | mstari wa mwisho unaojirudiarudia kwa kila ubeti |
| Kifungu cha maneno katika shairi | huitwa ubeti |
| Kifungu cha maneno katika shairi | mistari katika shairi |

| | |
|---|---|
| Sauti zinazofanana mwishoni mwa kila nusu-mstari | huitwa vina vya kati |

Kazi ya 14:

| | |
|---|---|
| 1. Falsafa au msimamo wa mshairi au mtazamo wa mshairi | ni mambo anayokubali mshairi kuwa ni ya kweli |
| 2. Mmshairi anapopambanisha wema na ubaya katika kazi yake, falsafa inaweza kuwa | “mnyonge hushinda mtundu”. |

**F. Uchambuzi au uhakiki**

Kazi ya 15:

Mwalimu awaelekeze wanafunzi jinsi ya kufanya habari iliyotolewa.

**G. Utafiti na uhakiki**

Kazi ya 16:

Kutafuta shairi na kulifanyia uhakiki kusisitizwe.

Kazi ya 17:

Kusoma uhakiki na kujibu maswali mbalimbali kuhamasishwe.

Kazi ya 18:

Kutafuta, kuandika na kusoma mashairi.

**H. Kuandika**

Kazi ya 19:

| | |
|---|---|
| Iwapo mstari wa mwisho unaojirudiarudia mwishoni mwa kila ubeti unaitwa | kibwagizo |
| Iwapo mstari wa mwisho haukururuduliwa mwishoni mwa kila ubeti unaitwa | Kimalizio |

Kazi ya 20:

Kubuni shairi, kulifanyia uhakiki na kulitolea tathmini kuzingatiwe.

Kazi ya 21:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. “Kuboronga sarufi” ni kupangua mpangilio wa maneno ili | akubalike na wanajamii wote |
| 2. Si lazima kila wakati mshairi | mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa kama vile tamathali za usemi na kadhalika |
| 3. Ni lazima kuonyesha iwapo shairi ni la kimapokeo au la kisasa na | kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi |

Kazi ya 22:

Kutunga shairi, kulifanyia uhakiki na kulitolea tathmini kuzingatiwe.

# SOMO LA 17: UTOAJI WA MAONI BINAFSI JUU YA KAZI YA FASIHI SIMULIZI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na saba.

| | |
|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuelezea hadharani maoni yao kuhusu utanzu wa fasihi simulizi ambao wameusoma au kuusikiliza darasani kwa kueleza walichofurahia, walichochukia, walichijifunza na kadhalika |
| Vipindi: | 6 |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti |
| Tathmini: | Tathmini endelezi |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili | -Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mtu mwingine bila ugomvi wowote.<br>-Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika tanzu inayoshughulikiwa. | -Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (kuwahudumia maskini hohehahe kwa kuwapa ng'ombe)<br>-Elimu isiyo na ubaguzi (elimu kwa wote na wanawake kuwa warithi) |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Mtu mmoja mwenye bango. Kwenye bango kumeandikwa "Utoaji wa maoni binafsi."

Kazi ya 2:

Kwenye bango kumeandikwa "Utoaji wa maoni bianafsi". Na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu jambo hilo la "Utoaji wa maoni binafsi."

### A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 3:

1. Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi ni kitendo cha kutoa msimamo wake au maneno yanayoonyesha fikra zake juu ya kazi ya fasihi.
2. Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi ni muhimu kwa sababu:

- -humwezesha mtu kumudu na kuboresha stadi za mazungumzo na kujieleza hadharani bila woga wala wasiwasi;
- -humfanya mtu aongezewe ujuzi wake wa kihistoria kuhusu utanzu na kipera fulani cha fasihi simulizi;
- -humfanya mtu azingatie ipaswavyo mbinu za kushawishi wengine ili waunge mkono msimamo wake;
- -humfanya mtu aongezewe uwezo wake wa kufafanua suala na kutatua tatizo haraka bila kukawia;

-humfanya mtu awe na adabu na uvumilivu katika kuyasikia maoni ya wengine na kutoa msimamo wake;
-humwezesha mtu hasa hasa mwanafunzi kuelewa maswali katika mtihani na kuyajibu ipaswavyo.

Mbinu zinazofuatiliwa katika kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi ni:

•Kuelewa suala yaani:

-Kuelewa kwanza maana ya maneno yaliyotumiwa;
-Kujua na kuelewa wakati na mahali husika yaani wakati gani jambo hilo lilitokea au lilifanyika na mahali lilipofanyiwa;
-Kujua maana ya viunganishi.

•Kusoma kazi ya fasihi na kuandika mambo yatakayojadiliwa;
•Kutayarisha mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi;
•Kueleza kazi ya fasihi husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

-Kutoa maelezo kuhusu maisha ya mtunzi (yanapojulikana);
-Kueleza chimbuko au asili ya kazi ya fasihi;
-Kuzitoa dhamira (kuu);
-Kutoa suala husika;
-Kutaja muhtasari wa mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi.

•Kufafanua au kuchambua kazi ya fasihi husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

-Kuzungumzia mawazo (dhamira) yanayozungumziwa katika kila aya: Mawazo hayo huelezwa kufuatana na jinsi mtunzi anavyoyaona mambo na msamiati aliotumia;
-Sentensi chache za kunukuu ni muhimu;
-Kuepukana na maelezo yasiyo na umuhimu.

•Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi kutokana na uhuru wa mchambuzi wa:

-Kusema kwamba msimamo wa mtunzi haukubaliwi na watu wote na kwamba kuna misimamo mingine;
-Kupinga maoni ya mtunzi na kutoa maelezo yanayotetea upinzani huo;
-Kukamilisha maoni ya mtunzi.

•Kukata shauri kuhusu suala yaani mchambuzi:

-Kutoa muhtasari wa mambo yaliyosemwa katika kazi hii;

-Kuzungumzia kidogo faida ya kazi hii ya utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi ambayo ameifanya

4.Katika kipengele chenyewe cha utoaji wa maoni binafsi, mchambuzi anaruhusiwa:

- -Kusema kwamba msimamo wa mtunzi haukubaliwi na watu wote na kwamba kuna misimamo mingine;
- -Kupinga maoni ya mtunzi na kutoa maelezo yanayotetea upinzani huo;
- -Kukamilisha maoni ya mtunzi.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kila mwanafunzi apewe fursa ya kusikiliza jinsi mwenzake au mwalimu anavyosoma habari hii kisha aandike mawazo makuu.

**B. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine kuzingatiwe.

Kazi ya 6:

Picha hii inaonyesha mtu anayesimama mbele ya kundi la watu na kutoa maoni yake binafsi kuhusu jambo fulani. Na habari yetu inahusu “utoaji wa maoni binafsi”.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7:

**Ovyo(ovyo):** Bila ya kufuata utaratibu; bila ya mpango
**Kufeli:** Kushindwa katika mtihani
**Hohehahe:** Mtu ambaye hali yake ya maisha si nzuri; mtu asiye na mbele wala nyuma; maskini sana

Kazi ya 8:

Kutunga kifungu cha habari kwa kila pea kuhimizwe.

Kazi ya 9:

1.Kufeli

2.Suala

Kazi ya 10:

| Kueleza kazi ya fasihi husika | Kufafanua kazi ya fasihi husika |
|---|---|
| - Kutoa maelezo kuhusu maisha ya mtunzi (yanapojulikana);<br>- Kueleza chimbuko au asili ya kazi ya fasihi;<br>- Kuzitoa dhamira (kuu);<br>- Kutoa suala husika;<br>- Kutaja muhtasari wa mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi. | - Kuzungumzia mawazo (dhamira) yanayozungumziwa katika kila aya: Mawazo hayo huelezwa kufuatana na jinsi mtunzi anavyoyaona mambo na msamiati aliotumia;<br>- Sentensi chache za kunukuu ni muhimu;<br>- Kuepukana na maelezo yasiyo na umuhimu. |
| | |

Kazi ya 11:

| |
|---|
| 1. Kila mtu ana uwezo wa kutoa maoni yake binafsi yake kuhusu kazi yoyote ya fasihi simulizi |
| 2. Si vizuri kutupilia mbali maoni ya mtu wakati hajamaliza kutoa nia yake. |
| 3. Ni lazima kuonyesha mambo mengine unayoyajua ambayo yatakusaidia katika kueleza suala na kutoa maoni binafsi juu ya kazi hiyo |

## E. Kuzungumza

Kazi ya 12:

Kuwaambia wengine yale ambayo yamesomwa kusisitizwe.

Kazi ya 13:

| | |
|---|---|
| Hapa ndipo mchambuzi ana uhuru wa | kukamilisha maoni ya mtunzi |
| | Kupinga maoni ya mtunzi na kutoa maelezo yanayotetea upinzani huo |
| | Kusema kwamba msimamo wa mtunzi haukubaliwi na watu wote na kwamba kuna misimamo mingine |

**F. Utafiti**

Kazi ya 14:

Kutafuta kazi ya fasihi simulizi, kuisoma na kujibu maswali husika kuzingatiwe.

**G. Kuandika**

Kazi ya 15:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Hata | wakongwe | wanapaswa | kulifanya | wanapojieleza | hadharani |
| Hata | wanafunzi | wanapaswa | kujihadhari | wanapoingia | darasani |
| Hata | waalikwa | wanalazimishwa | kunyamaza | wanapokusanyika | kumbini |

Kazi ya 16:

| |
|---|
| 1. Ni lazima na wewe utoe msimamo wako juu ya maoni yake na maelezo ya kutosha ili mawasiliano kati yenu yafanyike na kumshawishi akubaliane na wewe. |
| 2. Anapohitimu masomo yake, mwanafunzi anatahiniwa ili kufaulu na kupewa cheti chake. |
| 3. Kuna watu ambao huwa na hofu au kutetemeka ovyo wanapoambiwa kutoa maoni yao mbele ya umati au hadharani. |

Kazi ya 17:

1.Kufafanua suala ni kazi isiyo rahisi, kazi ambayo inahitaji makini.
2.Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi ni zoezi ambalo linahitaji ujuzi na uzoefu wa kiwango fulani katika taaluma ya elimu.
3.Utoaji wa maoni binafsi ni kama nguzo ya mawasiliano baina ya watu.

# SOMO LA 18: UTOAJI WA UWASILISHAJI KUHUSU KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

**Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na nane.**

| | |
|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuwasilisha mada inayohusiana na uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi<br>- kulinganisha tanzu moja na nyingine kwa kueleza kufanana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui |
| Vipindi: | 7 |
| Shughuli: | -Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Utafiti |
| Tathmini: | Tathmini endelezi |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
|---|---|---|
| Kumwezesha mwanafunzi kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza hadharani akichambua na kufafanua vipengele vya fani na maudhui vinavyojitokeza katika tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili | -Uhuru wa kutoa hoja au maoni tofauti na ya mtu mwingine bila ugomvi wowote.<br>-Mabadiliko au athari chanya za kiakili na kitabia kutokana na ujumbe unaozingatiwa katika tanzu inayoshughulikiwa. | -Mafunzo kuhusu kuzalisha kwa kiwango (bidhaa za kweli yaani zisizo za bandia)<br>-Amani na maendeleo<br>-Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Tunaona watu ambao wanawasilisha kazi yao kwa wengine. Kuna bango ambako kumeandikwa “Utoaji wa uwasilishaji”.

Kazi ya 2:

Kifungu cha habari kinahusu “kuwasilisha kazi za fasihi simulizi” na kwenye picha watu wanafanya kitendo cha kuwasilisha kazi yao kwa wenzao.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. “Utoaji wa uwasilishaji” au “utoaji wa mhadhara” ni utoaji wa maelezo mbele ya watu kwa ajili ya kufundisha.
2.Utoaji wa uwasilishaji kwa ujumla ni muhimu kwa sababu:

-Hukuza utu wa mtu;
-Humfanya mhadhiri azingatie na kumiliki stadi za kuzungumza hadharani na kushawishi hadhira yake;

-Humwongezea ujuzi mhadhiri;
-Humfanya mhadhiri aheshimiwe na hadhira kutokana na ujuzi wake wa kiwango cha juu alioutoa hadharani;
-Huweza kumfanya mhadhiri ajiongezee mali.

3.Nyinyi wanafunzi, mnatakiwa kufuata taratibu zifuatazo ili kuweza kufaulu katika kutoa mhadhara:

•Kutilia mkazo maandalizi ya utoaji wa uwasilishaji yaani:

-kufanya utafiti wa kutosha ili kuyapata maelezo yatakayozitetea nia zako;
-kuzingatia sehemu za kazi yako na yaliyomo ndani yake;
-kujiweka katika hali ya utulivu na kujiamini;
-kuwaza kuhusu namna ya utangulizi unaovuta hisia za hadhira.

•Kuwa tayari wakati wa kutoa mhadhara: Ingekuwa vizuri kujiandaa ipasavyo na kuwa tayari kuhusu mhadhara siku mbili kabla ya utoaji wa uwasilishaji. Ni kusema kuwa ni lazima kazi yako iwe tayari siku mbili kabla ya mhadhara na uwe umeizingatia vya kutosha. Kumbuka kuwa unapaswa kuweka 90% ya kazi yako kichwani mwako kwani kufaulu kwako katika mhadhara hakutategemea zaidi maandishi yako. Isitoshe, fika mapema mahali patakapofanyiwa mhadhara.

•Kuonyesha mwenendo wa kisomi yaani:

-Kuelewa na kumudu vizuri wazo kuu la kazi yako;
-Kuwaza vizuri kabla ya kusema;
-Kukuza msamiati wako;

-Kutumia maneno na sentensi kamili na sahihi.
-Kutii kanuni za sarufi;
-Kutumia maneno yanayoonyesha heshima;
-Kuonyesha kuwa unafahamu na kumudu vizuri yale unayoyasema;
-Kuzungumza bila kutazama sana maandishi;
-Kuwa na maoni mazuri juu ya hadhira;
-Kuvaa vizuri;
-Kudhibiti mwenendo wako mbele ya hadhira...

• Kuzingatia na kumudu stadi za kuzungumza: Mhadhiri hulazimishwa :

-Kutumia maneno machache lakini yanayoeleza vizuri mawazo yake;
-Kutositasita katika mazungumzo;
-Kusema polepole;
-Kutumia ishara za mikono;
-Kutochezacheza na vitu mbalimbali.

•Kuchambua kazi na kuingia katika undani wake: Kuhusu jambo hili, mhadhiri anatakiwa:

-Kukuza au kuongeza ujuzi alio nao kuhusu kazi ya fasihi simulizi husika;
-Kuijua athari ya kazi ya fasihi simulizi husika kwa hadhira yake.

•Kutoa mhadhara ipasavyo kwa kuzingatia sehemu mbalimbali zinazotakiwa.

4.“Mhadhara huwa na sehemu muhimu ambazo huzingatiwa katika utayarishaji wake”. Sehemu hizo ni hizi zifuatazo:

a.Utangulizi: Ni sehemu ya kwanza ya mhadhara. Mhadhiri hutakiwa:

-Kuanzisha jambo au hadithi au msemo mwingine unaoweza kuifanya hadhira itoe maoni yanayoelekeza kwenye mada itakayozungumziwa;
-Kutaja mada ya kazi yake;
-Kukumbusha mambo inayoyafahamu hadhira kuhusu mada yenyewe;
-Kutaja shabaha ya kazi yake;
-Kutaja mawazo makuu yanayopatikana katika kazi yake na jinsi mhadhara unavyotarajiwa kuendelezwa.

b.Upeo: Mambo ya kuzingatia ni haya yafuatayo:

-Urefu wa mhadhara: urefu wa sehemu hii hutokana na muda wa mhadhara (kuanzishwa na kufungwa kwake);
-Kujihadhari ili kutoenda mbali na mada husika;
-Ujuzi wa hadhira: Si vizuri kutegemea ujuzi wa hadhira;

-Kutumia sentensi fupi;
-Kueleza istilahi muhimu na maneno magumu yatakayotumiwa katika mhadhara;
-Kunukuu ni muhimu.

c.Mkaguo: Hii ni sehemu ya mwisho ya mhadhara. Mhadhiri hutakiwa:

-Kutumia mkagua unaosisimua hadhira;
-Kutoa muhtasari wa yale ambayo yamezungumziwa katika mhadhara;
-Kukumbusha kidogo wazo lake kuu;
-Kuipa hadhira fursa ya kuuliza maswali na kuyajibu;
-Kutoa shukrani kwa hadhira kwa kuhudhuria mhadhara.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza na kuandika mawazo makuu kutiliwe maanani kwa kila mwanafunzi.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma habari kwa mara nyingine kwa kuheshimu alama za uakifishaji kuzingatiwe.

Kazi ya 6:

-Wanazungumzia kuhusu “mhadhara”;
-Mhadhara ni maelezo yanayotolewa mbele ya watu juu ya mada fulani kwa ajili ya kufundisha.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7:

**Stadi:** Mbinu zinazotumiwa katika kutenda jambo fulani kiufundi
**Msimu:** Majira; kipindi kirefu cha wakati ambapo jambo fulani (kama vile mvua, jua,...) hutokea
**Taasisi:** Sehemu au idara inayoshughulika na uchunguzi wa fani mbalimbali
**Mapato**: Kitu kinachopatikana hasa baada ya kazi au biashara

Kazi ya 8:

Kila jozi ina sentensi zake.

Kazi ya 9:

1.Utulivu
2.Mihadhara

Kazi ya 10:

| Kuonyesha mwenendo wa kisomi | Kuzingatia na kumudu stadi za kuzungumza |
|---|---|
| -Kuelewa na kumudu vizuri wazo kuu la kazi yako;<br>-Kuwaza vizuri kabla ya kusema;<br>-Kukuza msamiati wako;<br>-Kutumia maneno na sentensi kamili na sahihi.<br>-Kutii kanuni za sarufi;<br>-Kutumia maneno yanayoonyesha heshima;<br>-Kuonyesha kuwa unafahamu na kumudu vizuri yale unayoyasema;<br>-Kuzungumza bila kutazama sana maandishi;<br>-Kuwa na maoni mazuri juu ya hadhira;<br>-Kuvaa vizuri;<br>-Kudhibiti mwenendo wako mbele ya hadhira;... | -Kutumia maneno machache lakini yanayoeleza vizuri mawazo yake;<br>-Kutositasita katika mazungumzo;<br>-Kusema polepole;<br>-Kutumia ishara za mikono;<br>-Kutochezacheza na vitu mbalimbali. |

Kazi ya 11:

| |
|---|
| 1. Darasani, mwanafunzi anayetoa mhadhara kwa wenzake anapaswa kuiheshimu hadhira yake ili kuweza kuwashawishi kukubali hoja zake. |
| 2. Mhadhiri akifaulu katika utoaji wa uwasilishaji, hadhira itamwona kama msomi mwenye ujuzi mkubwa na kumheshimu vilevile. |

| |
|---|
| 3. Epuka maneno yanayovunja kanuni za sarufi au yanayotumiwa na wahuni na watoto wa mtaani yaani lugha chafu. |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 12:

Kuwaambia yale ambayo kila mwanafunzi amesoma kuzingatiwe.

Kazi ya 13:

| | |
|---|---|
| Katika utangulizi wa mhadhara, mhadhiri hutakiwa | kutaja mada ya kazi yake |
| | Kuanzisha jambo au hadithi au msemo mwingine unaoweza kuifanya hadhira itoe maoni yanayoelekeza kwenye mada itakayozungumziwa |
| | Kutaja mada ya kazi yake |
| | Kukumbusha mambo inayoyafahamu hadhira kuhusu mada yenyewe |
| | Kutaja shabaha ya kazi yake |
| | Kutaja mawazo makuu yanayopatikana katika kazi yake na jinsi mhadhara unavyotarajiwa kuendelezwa |

**F. Utafiti**

Kazi ya 14:

Kutafuta hadithi yoyote ya fasihi simulizi ya Kiswahili na kutayarisha mhadhara juu yake.

**G. Kuandika**

Kazi ya 15:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Utoaji | wa | mhadhara | huongeza | ujuzi | wa | mhadhiri |
| Utoaji | wa | mhadhara | hukuza | utu | wa | mhadhiri |
| Utoaji | wa | mhadhara | huongeza | mali | ya | mhadhiri |

Kazi ya 16:

| |
|---|
| 1. Ni lazima mwenendo wako uonyeshe kwamba wewe ni msomi mwenye ujuzi wa kiwango cha juu. |
| 2. Mbinu hii inakusaidia katika kuepukana na matumizi ya maneno yasiyo na maana au ukosefu wa jambo la kusema. |
| 3. Kuna kazi za fasihi simulizi zinazoweza kuwa na athari mbaya kwa hadhira. |

Kazi ya 17:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Mhadhara wako utavuta hisia za watu kutokana na maneno unayoyatumia hasa maneno yenye | matokeo ya kazi tuliyoifanya au kazi ya wengine |
| 2. Kumbuka kuwa unapaswa kuweka 90% ya kazi yako kichwani mwako kwani | maana sawa na yale magumu ambayo yalitumiwa katika kazi ya fasihi husika |
| 3. Maishani mwetu, tunaweza kutakiwa kuwasilisha kwa hadhira | kufaulu kwako katika mhadhara hakutategemea zaidi maandishi yako |

# SOMO LA 19: MUUNDO WA SENTENSI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la kumi na tisa

<table>
<tr><td>Shabaha:</td><td colspan="2">Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kukumbuka mambo muhimu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake</td></tr>
<tr><td>Vipindi:</td><td colspan="2">6</td></tr>
<tr><td>Shughuli:</td><td colspan="2">-Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; sarufi na matumizi ya lugha; -Tathmini kuhusu sura</td></tr>
<tr><td>Tathmini:</td><td colspan="2">Tathmini endelezi na upimaji wa kiujumla</td></tr>
<tr><td>Uwezo wa kuendelezwa</td><td>Mwenendo na maadili mema</td><td>Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| Kuzingatia muundo wa sentensi za Kiswahili | -Kufurahia kujua kuchambua sentensi ya Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake | -Mafunzo kuhusu maendeleo ya haraka ya uchumi<br>-Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (sigara huharibu afya ya mtu) |

**B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI**

Kazi ya 1:

Tunaona kiwanda cha UTEXRWA kinachotengeneza nguo.

Kazi ya 2:

Picha inatuonyesha kiwanda cha UTEXRWA kinachotengeneza nguo na habari yetu inahusu viwanda barani Afrika.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. "Nchi nyingi za kiafrika zinakitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yake." Ni kusema kwamba serikali za nchi nyingi za kiafrika hutilia mkazo kilimo na kukiona kama nguzo ya maendeleo yake. Idadi kubwa ya wananchi ni wakulima.
2. Ni vizuri katika nchi kuwa na sekta ya kilimo na sekta ya viwanda kwa sababu ni vitu.
3. Matatizo yanayovikabili viwanda vingi barani Afrika ni kama vile:

   -kukosa vipuli na kubadilika kwa miundo ya mitambo;
   -kukosa wataalamu;
   -aina nyingine ya malighafi ambayo huagizwa kutoka nchi za ng'ambo.

4. Licha ya majembe na matrekta, kuna zana nyingine za kilimo kama vile sepetu, sururu, reki, tridenti, pipa la kumwagilia na kadhalika
5. Katika kurutubisha mashamba yako, unaweza kutumia mbolea ya samadi au ya chumvi chumvi.

## B. Kusikiliza

Kazi ya 4:

Kusikiliza na kuzingatia mawazo makuu kusisitizwe.

## C. Kusoma

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine kusisitizwe.

Kazi ya 6:

Picha hizi zinaonyesha noti za dola za Marekani na za faranga za Rwanda. Kwenye soko la kimataifa, fedha yenye nguvu ni dola za kimarekani. Ile ya Rwanda haina thamani kubwa.

Kazi ya 7:

| |
|---|
| 1. Mara nyingi imelazimu kupata wataalamu wa kuendesha viwanda kutoka nchi zilizoendelea. |
| 2. Tatizo kubwa kwa viwanda vingi ni lile la kukosa vipuli na kubadilika kwa miundo ya mitambo |
| 3. Nchi zinapokuwa katika matatizo ya kifedha, hushindwa kuagiza malighafi hizo na husababisha viwanda kufungwa |

Kazi ya 8:

| Bidhaa | Kiwanda |
|---|---|
| Sharubati | INYANGE INDUSTRIES Ltd |
| Pombe | BRALIRWA Ltd; MBC Ltd |
| Saruji | CIMERWA Ltd |
| Nguo | UTEXRWA Ltd |

## D. Msamiati

Kazi ya 9:

**Kutoma:** Kuingia ghafla au kwa nguvu

**Pembejeo:** Vitu mbalimbali (kama vile mbolea, madawa,...) vinavyotiwa katika mashamba ili kuweza kupata mazao mengi tena mazuri
**Malighafi:** Mali ambayo haijasafishwa kama vile madini (dhahabu, lulu,...)

Kazi ya 10:

Kutunga sentensi / Mfano: Viwanda vyote hufanya kazi kwa kutumia malighafi.

Kazi ya 11:

Kila mwanafunzi ana sentensi zake / Mfano: Kuvuta sigara huharibu afya ya mtu na hakuwezi kamwe kuboresha afya yake.

Kazi ya 12:

1. Wataalamu hao wamezigharimu serikali au mashirika yanayoendesha viwanda kiasi kikubwa cha fedha.
2. Nchini Rwanda, mbolea ya samadi huchanganywa na ile ya chumvi chumvi ili kurutubisha mashamba.
3. Badala ya kuuza malighafi katika nchi za Ulaya na Marekani, bidhaa zilitengenezewa nyumbani ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi ambao wengi wao walikuwa wakulima.

Kazi ya 13:

1. Jembe, trekta, panga, mkokoteni ni zana.
2. BRALIRWA, BMC, UTEXRWA, TOLIRWA ni viwanda.

Kazi ya 14:

| Neno | Neno lenye maana sawa na lile | Kinyume cha neno lile |
|---|---|---|
| 1. Kufaulu<br>2. Kuharibu | Kushinda<br>Kuangamiza | Kufeli<br>Kulinda / Kuokoa |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 15:

Kuwaambia yale ambayo kila mwanafunzi amesoma kusisitizwe.

Kazi ya 16:

1. Ingawa nchi nyingi hulisha viwanda vyake kwa malighafi ambayo imezalishwa humo humo nchini, kuna aina nyingine ya malighafi ambayo huagizwa kutoka nchi za ng’ambo.
2. Hivi sasa, nchi zinazouza vipuli zimeathiriwa na matatizo ya kiuchumi na, kwa hiyo, bei yake imepanda.
3. Viwanda navyo kwa upande mwingine huhitaji malighafi kama vile kahawa, pamba, mkonge, tumbaku na kadhalika.
4. Mitambo ya viwanda vingi barani Afrika iliagizwa kutoka Ulaya, Marekani au sehemu nyingine zenye viwanda-mama.

**F. Sarufi na matumizi ya lugha**

Kazi ya 17:

Muundo wa sentensi hizi si sawa unapozingatia aina ya maneno yanayoziunda lakini zote zina kiima na kiarifu.

Kazi ya 18:

1. Viwanda huhitaji malighafi na vipuli.
   N T N U N

2. Nchi zetu hukitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yetu.
   N V T N U N V N V N V

3. Vitu vyote hivi ni matokeo ya kazi za viwanda.
   N V V t N V N V N

4. Nchi nyingi hushindwa kuagiza malighafi muhimu na hupata hasara viwandani.
   N V Ts T N V U T N E

Kazi ya 19:

Katika jozi wanafunzi watafute muundo wa sentensi na kuwasomea wenzao matokeo ya utafiti wao.

Kazi ya 20:

a) “Kiima”: ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
b) “kiarifu”: ni sehemu ya sentensi yenye kitenzi, shamirisho na chagizo.

c) “shamirisho”: ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo. Ni mtendwa au mtendewa katika sentensi. Ni sehemu inayojibu swali “alitenda.

d) nini?”, “alitenda nani?”
“chagizo”: hutueleza zaidi kuhusu kiima na shamirisho. Aghalabu, chagizo ni kielezi.
“kipashio”: kipande cha tungo ambacho kinaweza kujengwa na neno moja au zaidi.

Kazi ya 21:

1. Serikali ya Rwanda iliunda mikakati thabiti ya kuboresha uzazi.

| Kiima (K) | | | Kiarifu (A) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | V | N | T | SH (Shamirisho) | | | | |
| | | | | N | V | CH (Chagizo) | | |
| | | | | | | V | T | V |
| Serika | ya | Rwanda | iliunda | mikakati | thabiti | ya | Kuboresha | Uzazi |

2. Umoja wa wananchi ni nguzo muhimu ya Amani na maendeleo

| Kiima (K) | | | Kiarifu (A) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | V | N | t | j (Kijalizo) | | | | | |
| | | | | N | V | CH (Chagizo) | | | |
| | | | | | | V | N | U | N |
| Umoja | wa | wananchi | ni | nguzo | muhimu | ya | amani | na | maendeleo |

3. Nchi yake huagiza malighafi kutoka Rwanda.

| Kiima (K) | | Kiarifu (A) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| N | V | T | SH (Shamirisho) | | |
| | | | | CH( Chagizo) | |
| | | | N | H | N |
| Nchi | yake | huagiza | malighafi | kutoka | Rwanda |

Kazi ya 22:

1.Kiima ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
2.Kiarifu ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.

3.Shamirisho ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

Kazi ya 23:

Kulinganisha majibu na maelezo

G. Kuandika

Kazi ya 24:

| **Majembe, matrekta,...** | **ni** | **zana** | **za** | **kilimo** |
|---|---|---|---|---|
| Bastola, kifaru, bunduki, manowari, mzinga, nyambizi,... | ni | zana | za | vita |
| Basi, baisikeli, gari la ngombe, mkokoteni, motokaa, mtumbwi, pikipiki, garimoshi,... | ni | zana | za | usafirishaji |
| Simu, faksi, teleksi, redio,... | ni | zana | za | mawasiliano |

Kazi ya 25:

1.Katika uzalishaji, ingekuwa rahisi zaidi kama sekta hizi mbili zingekamilishana.
2.Hata hivyo, imethibitika kwamba ili nchi zipate kuendelea, ni lazima viwanda vitiliwe mkazo.
3.Matatizo haya pamoja na mengine mengi yamevifanya viwanda mbalimbali vijikute katika matatizo makubwa.
4.Labda tatizo hili litapunguzwa kwa kuwaandaa wataalamu wananchi katika nchi zenye teknolojia sadifu ya juu.

TATHMINI KUHUSU SURA YA PILI

Kujibu maswali:
1.“Uhakiki wa kazi za fasihi si jambo la hivi karibuni”. Kuwepo kwa uhakiki ulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine. Yeyote yule anayelinganisha kazi za fasihi na tajiriba yake maishani au na kazi nyingine huwa ameanza kufanya uhakiki. Uhakiki huanza katika kitendo cha kujaribu kuielewa kazi ya fasihi na kujibu maswali kama vile kwa nini, nani na vipi.

2.Mwanafunzi huhitaji kufanya mazoezi kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi kwa sababu:

-humwezesha kuielewa, kuieleza na kuifaidi kazi ipaswavyo;
-humwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi;
-humwezesha kuchambua na kufafanua mifumo na picha za kisanaa zinazotumika katika kazi za fasihi ili kupevuka katika lugha;
-humwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi. Maonyo hayo tunaweza kuyatumia kwa kuwakosoa wanajamii wengine.

3.Kuchagua hadithi na kuifanyia uhakiki.

4.Kutafuta methali na kuzifanyia uhakiki.

5.Kutafuta vitendawili na kuvifanyia uhakiki.

6.Toa maana ya nahau hizi:
-Kumwaga unga= Kufukuzwa kazi
-Kugonga mwamba= Kutofanikiwa

7.Vipengele ambavyo hushughulikiwa katika kuhakiki shairi ni:

Uhakiki wa shairi kimaudhui:

-Maisha ya mtunzi (iwapo yanajulikana);
-Kichwa cha shairi;
-Aina (au kipera) ya shairi;
-Dhamira au wazo kuu;
-Ujumbe au fundisho au maadili au onyo;
-Falsafa au msimamo wa mshairi au mtazamo wa mshairi;
-Muhtasari (kwa nathari).

Uhakiki wa shairi kifani:

•Wahusika: Ikiwa shairi limehusisha wahusika;
•Mtindo;
•Muundo au umbo la shairi: Mambo yatakayozungumziwa hapa ni:

-Idadi ya beti;
-Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
-Idadi ya vipande vya mstari;
-Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
-Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;
-Bahari ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa “kibwagizo” au “kiitikio”. Kama hakuna mstari wa mwisho unaojirudiarudia, basi mstari huo utaitwa “kimalizio” au “kituo.”

•Uhuru wa mshairi.

8.Mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi:

•Kuelewa suala yaani:

-Kuelewa kwanza maana ya maneno yaliyotumiwa;
-Kujua na kuelewa wakati na mahali husika yaani wakati gani jambo hilo lilitokea au lilifanyika na mahali lilipofanyiwa;
-Kujua maana ya viunganishi.

•Kusoma kazi ya fasihi na kuandika mambo yatakayojadiliwa;
•Kutayarisha mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi;
•Kueleza kazi ya fasihi husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

-Kutoa maelezo kuhusu maisha ya mtunzi (yanapojulikana);
-Kueleza chimbuko au asili ya kazi ya fasihi;
-Kuzitoa dhamira (kuu);
-Kutoa suala husika;
-Kutaja muhtasari wa mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi.

•Kufafanua au kuchambua kazi ya fasihi husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

-Kuzungumzia mawazo (dhamira) yanayozungumziwa katika kila aya: Mawazo hayo huelezwa kufuatana na jinsi mtunzi anavyoyaona mambo na msamiati aliotumia;
-Sentensi chache za kunukuu ni muhimu;
-Kuepukana na maelezo yasiyo na umuhimu.

•Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi kutokana na uhuru wa mchambuzi wa:

-Kusema kwamba msimamo wa mtunzi haukubaliwi na watu wote na kwamba kuna misimamo mingine;
-Kupinga maoni ya mtunzi na kutoa maelezo yanayotetea upinzani huo;
-Kukamilisha maoni ya mtunzi.

•Kukata shauri kuhusu suala yaani mchambuzi:

-Kutoa muhtasari wa mambo yaliyosemwa katika kazi hii;
-Kuzungumzia kidogo faida ya kazi hii ya utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi ambayo ameifanya
9.Shirikiana na mwenzako na kutunga sentensi tatu zinazohusu “amali na tamaduni na kuzalisha kwa kiwango”. Mtakapomaliza, mwonyeshe muundo wa sentensi hizo.

Kila kundi lina sentennsi zake

# SURA YA 3: UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO

Sura hii inashughulikia vipengele viwili. Kipengele cha kwanza kinahusu fasili ya barua rasmi na kipengele cha pili kinahusu simu na matangazo.

## MAANDALIO YA SOMO

Mfano wa maandalio ya masomo kuhusu sura hii ni huu ufuatao:

<table>
<tr><td colspan="8">MAANDALIO YA SOMO</td></tr>
<tr><td colspan="4">Shule:</td><td colspan="4">Jina la mwalimu:</td></tr>
<tr><td>Muhula wa</td><td>Tarehe</td><td>Somo</td><td>Kidato cha</td><td>Sura ya</td><td>Somo la</td><td>Muda</td><td>Idadi ya wanafunzi</td></tr>
<tr><td>Kwanza</td><td>20/06/2016</td><td>Kiswahili</td><td>Tano</td><td>tatu</td><td>1 kwa 4</td><td>Dakika 80</td><td>32</td></tr>
<tr><td colspan="8">Makundi ya wanafunzi wenye matatizo ya kielimu na idadi yao:<br>1. Wanafunzi wenye matatizo ya kusikia: 2<br>2. Wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu: 4</td></tr>
<tr><td>Mada kuu:</td><td colspan="7">Mawasiliano rasmi</td></tr>
<tr><td>Mada ndogo:</td><td colspan="7">Utungaji wa barua rasmi, simu na matangazo</td></tr>
<tr><td>Uwezo unaohitajiwa katika mada:</td><td colspan="7">Mwishoni mwa sura hii, mwanafunzi ataweza:<br>• Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi akitumia Kiswahili sanifu.</td></tr>
<tr><td>Kichwa cha somo</td><td colspan="7">Utungaji wa barua rasmi au ya kikazi</td></tr>
<tr><td>Uwezo unaohitajiwa katika somo</td><td colspan="7">Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi ataweza:<br>• Kutunga barua ya kikazi kutokana na kisa kinachojitokeza.</td></tr>
<tr><td>Mahali pa kufundishia</td><td colspan="7">Darasani</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| Malengo ya kujifunza (Ni lazima yazingatiwe mahitaji ya wanafunzi) | Maarifa na ufahamu:<br>• Kueleza tofauti iliyopo kati ya barua ya kirafiki na barua rasmi ;<br>• Kukumbuka sehemu za barua rasmi;<br>• Kutoa mfano wa mazingira ya barua za kikazi, simu pamoja na tangazo lililotumiwa;<br>• Kutambua mtindo wa simu na wa tangazo;<br>• Kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili.<br><br>Stadi:<br>• Kutunga barua ya kikazi kutokana na kisa kinachojitokeza;<br>• Kuonyesha kwa mchoro sehemu kuu za barua rasmi;<br>• Kuandika simu kwa kuzingatia taratibu au mtindo unaojidhihirisha;<br>• Kutayarisha tangazo maalumu kulingana na mazingira yanayotolewa.<br><br>Maadili na mwenendo:<br>• Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao;<br>• Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano;<br>• Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. |
| Vifaa vitakavyotumiwa | Matini zenye mitindo mbalimbali ya uandishi wa barua, magazeti, mtandao wa intaneti, vitabu, simu ya mkononi, ubao, chaki, kalamu na kifutio |
| Vitabu vitakavyotumiwa | Kitabu cha Mwanafunzi<br>Mwongozo wa Mwalimu<br>Vitabu vingine vinavyohusu utungaji wa barua katika Kiswahili, simu ya maneno na matangazo |

| | |
|---|---|
| Tathmini ya mwalimu | Kutokana na maoni yake kuhusu jinsi wanafunzi walivyoshiriki katika somo lake, mwalimu achunguze jambo la kutilia mkazo hususan pale ambapo wanafunzi wamekutana na matatizo mbalimbali. |

# SOMO LA 20: BARUA RASMI NA UTUNGAJI WAKE

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la ishirini.

| | | |
|---|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kueleza tofauti iliyopo baina ya barua ya kirafiki na barua rasmi<br>- kutunga barua ya kikazi kutokana na kisa kinachojitokeza<br>- kukumbuka sehemu muhimu za barua rasmi<br>- kutoa mfano wa barua za kikazi | |
| **Vipindi:** | 18 | |
| **Shughuli:** | - Kutafakari picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika | |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi | |
| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
| Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | -Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (umoja na maridhiano baina ya Wanyarwanda) |

### KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kinachoonekana ni:

- Mkono ambao unachukua barua;
- Kwenye bahasha kumeandikwa jina “Kalisa.”

Kazi ya 2:

Picha inaonyesha mtu ambaye anaandika barua na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu jinsi ya kuandika barua hasa ya kikazi.

**A. Maswali ya Ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Barua au waraka ni maandishi kwa mtindo wa kinathari yanayopelekwa kwa mtu kutoka mtu mwingine kwa madhumuni ya:

   - Kuarifu kwa haraka;
   - Kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa,...;
   - Kuagiza bidhaa na kadhalika.

2. Sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi ni kama vile kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, kuandikia meneja wa gazeti na kadhalika
3. “Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo”. Anapoipokea mtu aliyetungiwa barua, anamwona mwandishi katika picha ya barua hiyo. Mawazo yanayopatikana ndani yake ni yale ya mwandishi. Ni kusema kuwa barua yenyewe inamwakilisha mwandishi wake na kumpelekea mwandikiwa ujumbe kutoka kwa mwandishi.
4. “Barua ni nusu ya kuonana.” Unapoipokea barua kutoka kwa mtu fulani, ni kama kumwona mtu huyo lakini si ana kwa ana bali kuna kitu yaani barua kinachomwakilisha. Ni kusema kuwa mwandikiwa amemwona mwandishi katika barua yake au amemwona kwa nusu tu.
5. Kwa maoni yangu, barua huandikwa kwa mtindo wa nathari.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza na kuandika mawazo makuu.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma habari mara nyingine

Kazi ya 6:

Picha inaonyesha kalamu. Kalamu ni chombo kinachotumiwa katika kuandika barua.

Kazi ya 7:

| |
|---|
| 1. Mwanafunzi anapohitimu masomo yake huhitaji kuandika barua ili kuomba kazi. |
| 2. Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo. |

**D. Msamiati**

Kazi ya 8:

Risala: Taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani aghalabu inayoeleza haja inayotakiwa
Kuadhimisha: Kusherehekea jambo au siku kwa kuitukuza au kuisifu
Nadra: Hali ya kutopatikana mara kwa mara
Saini: Sahihi; maandishi ya jina la mtu ya kuthibitisha au kuidhinisha kutendeka au kupatikana kwa kitu au jambo fulani kwa kuandika jina lako
Nakala: Kitu chochote kilichonukuliwa kama vile maandishi, mchoro, picha,...

Kazi ya 9:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake

Kazi ya 10:

| Ujumbe | Sehemu |
|---|---|
| | Mwisho au hitimisho |
| | Saini ya mwandishi na jina lake |
| | (Nakala kwa) |

Kazi ya 11:

| |
|---|
| 1. Samahani mwalimu, tuseme kuwa mimi ni daktari wa meno. |
| 2. Barua hii haitakuwa ya kirafiki kwa kuwa katikiro si kiongozi! |
| 3. Sehemu hii inatumiwa mara kwa mara kwa madhumuni fulani. |

Kazi ya 12:

Kutoa maelezo ya kutosha.

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 13:

-Kumbukumbu namba (ikiwa unayo)
-Anwani ya mwandishi na tarehe:
-Anwani ya mwandikiwa
-(Kupitia kwa na anwani ya mwenye kusaini na kutia muhuri)
-Salaam
-Yahusu / Kuhusu / Yah. / Kuh.
-Mwanzo au utangulizi
-Ujumbe
-Mwisho au hitimisho

Kazi ya 14:

| | |
|---|---|
| Barua ni | nusu ya kuonana |
| | risala au ujumbe mwepesi |
| | kumbukumbu ya kudumu |
| | shahidi wa nafsi |

**F. Utaratibu wa barua rasmi**

Utaratibu wa barua rasmi

Kazi ya 15:

Kutunga barua.

**G. Kuandika**

Kazi ya 16:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Si | kusahau | Mtoto | wangu |
| Si | kualika | Rafiki | yangu |
| Si | kupenda | Dada | zangu |
| Si | kusamehe | Kaka | yangu |

Kazi ya 17:

Kutunga barua na kutoa jibu.

KUMB: GA/103/03/2016

Kijiji cha Gihaya
Kata ya Mubali
Tarafa ya Rubero
Wilaya ya Giti
Namba ya Simu: 0788521366
SLP 25 Rwamagana
JIMBO LA MASHARIKI

25/06/2016

Mkuu wa Shule ya Giti
SLP 48 Rwamagana
JIMBO LA MASHARIKI

Mkuu wa Shule,

YAH: Kufunga shule

Kichwa cha hapo juu chahusika.

Rejea barua yangu ya tarehe 20/0/2016 iliyokuwa ikiwataka kufunga shule kwa sababu ya ugonjwa wa kipindupindu uliojitokeza ghafla katika wilaya yetu.
Ni matumaini yangu kwamba barua hiyo uliipokea na hivyo, utekelezaji wake usingechelewa.
Ninapenda kukutumia barua hii tena kukuomba kufunga shule. Jambo hili ni la kuzingatia kwani likiendelea linaweza kusababisha madhara makubwa kwa wanafunzi na umma mzima.

Asante.

Wako mtiifu,

(Saini)

Mkuu wa Wilaya

Kazi ya 18:

Kuandika barua.

# SOMO LA 21: UTUNGAJI WA SIMU

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo ambao unahusu somo hili la ishirini na moja

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua mtindo wa simu<br>- kutunga simu ya maneno kutokana na kisa kinachojitokeza<br>- kuelewa sehemu muhimu za simu ya maneno<br>- kutoa mfano wa simu ya maneno |
| **Vipindi:** | 18 |
| **Shughuli:** | -Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; - Kucheka |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
|---|---|---|
| Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | -Usawa wa jinsia<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Simu ya kawaida ya waya na simu ya mkononi

Kazi ya 2:

Hizi ni simu. Simu ni vyombo vinavyotumiwa katika kuwasiliana kwa njia mbalimbali kama vile kupashana habari, kutuma ujumbe wa maandiko na kadhalika.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Simu ni chombo kinachotumia umeme na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana. Chombo hicho hupelekea na kupokelea mawimbi ya sauti baina ya mtu na mtu papo kwa papo. Simu huweza pia kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia chombo hicho au kwa kutumia mtambo mwingine (kama vile faksi, teleksi,...) na kuandikwa baadaye.
2. Simu ya maneno huwa fupi sana kwa sababu mtu hana fursa ya kueleza mengi au kuzungumza moja kwa moja na yule anayempelekea taarifa.
3. Sifa za simu ya maneno ni:

    - Kuwa fupi sana;
    - Kwenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida;
    - Kuwa na maneno machache;
    - Kuandikwa kwa kutumia herufi kubwa.

4. “Simu ni mjumbe mwepesi sana”. Kwa kusafirishwa na mitambo mbalimbali, simu ya maneno humfikia mtu baada ya muda mfupi sana (sekunde chache sana).

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma na kuandika mawazo makuu.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma kwa mara nyingine.

Kazi ya 6:

Picha hii inaonyesha kampuni tatu zinazoshughulikia mawasiliano nchini Rwanda hasa kwa kupitia njia ya simu ya mkononi. Na katika kifungu cha habari kuna aya zinazohusu mawasiliano hayo.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7:

Waya: Uzi wa madini ya chuma unaotumiwa katika kusafirisha umeme, mawimbi ya sauti na kadhalika
Umeme: Miali ya moto inayoonekana kabla ya radi; nguvu zinazotoa cheche
Wimbi: Mtutumko wa sauti au nuru zinazosafiri hewani au wa maji baharini au ziwani...

Kazi ya 8:

Kila jozi imetunga aya yake.

Kazi ya 9:

| Sehemu zake | Mitambo inayotumiwa ili kutuma ujumbe |
|---|---|
| -Anwani kamili ya mwandikiwa;<br>-Ujumbe wenyewe;<br>-Jina la mwandikaji. | -faksi;<br>-teleksi |

Kazi ya 10:

| |
|---|
| 1. Simu ni chombo kinachotumia umeme na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana. |
| 2. Kwa kusafirishwa na mitambo mbalimbali, simu ya maneno humfikia mtu baada ya muda mfupi sana (sekunde chache sana). |
| 3. Awali, simu ilihitaji iunganishwe na nyaya, lakini leo hii kuna siwaya au simu bila waya. |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 11:

Kuwaambia wengine yale ambayo ameyasoma

Kazi ya 12:

Huu ni mnara wa mawasiliano. Mitambo mbalimbali ambayo inachangia katika kurahisisha mawasiliano inafungwa kwenye mnara huu. Na simu ya maneno inasafirishwa kupitia mitambo hiyo.

Kazi ya 13:

| | |
|---|---|
| Simu inaweza kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia chombo hicho au kwa kutumia mtambo mwingine kama vile | faksi |
| | teleksi |

**F. Cheka uongeze siku za kuishi**

Kazi ya 14:

Kutafuta kichekesho kingine.

**G. Kuandika**

Kazi ya 15:

| | |
|---|---|
| Simu ya maneno | huwa fupi sana |
| | huenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida |
| | huwa na maneno machache |
| | huandikwa kwa kutumia herufi kubwa |

Kazi ya 16:

Kupeleka ujumbe.

Kazi ya 17:

Kutunga simu ya maneno.

# SOMO LA 22: UTUNGAJI WA MATANGAZO

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Huu ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la ishirini na mbili.

| | |
|---|---|
| Shabaha: | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kutambua mtindo wa tangazo<br>- kutunga tangazo kutokana na kisa kinachojitokeza<br>- kuelewa sehemu muhimu za tangazo<br>- kutoa mfano wa tangazo |
| Vipindi: | 18 |
| Shughuli: | -Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika |
| Tathmini: | Tathmini endelezi |

| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
|---|---|---|
| Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandiko rasmi kwa kutumia Kiswahili sanifu | -Adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowasiliana nao.<br>-Ari ya kupenda kuwasiliana na watu kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano.<br>-Moyo wa kujenga urafiki na ushirikiano na watu mbalimbali kwa njia ya mawasiliano. | -Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kuwekeza pesa na kuwasiliana na benki ili kukuza mtaji)<br>-Mafunzo kuhusu amani (mkataba wa amani)<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI<br>-Mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu (kuepukana na kuvuta sigara) |

B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kwenye picha kumeandikwa tangazo hili la Polisi “Kutumia njia za pembeni ni kuvunja sheria, kuharibu barabara na mazingira. AMRI: Fuata barabara kuu”

Kazi ya 2:

Picha inaonyesha tangazo la polisi na kifungu cha habari chetu kinazungumzia utungaji wa matangazo.

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Tangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani.
2. “Lengo la matangazo huwa na uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa”. Matangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani na huainishwa kufuatana na shughuli au jambo linalozungumziwa. Kwa hiyo, tutakuwa na matangazo ya serikali, matangazo ya biashara, matangazo ya kazi, matangazo ya kifo na kadhalika.
3. Matangazo huandikwa kwa muhtasari kwa sababu hutumia maneno machache ili kutomchosha mlengwa.
4. Katika matangazo ya biashara, lugha ya mvuto hutumiwa kwa sababu huwa nyepesi kukumbukwa na huwa inaeleweka kirahisi.
5. Mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo:

   - Kuandika kichwa cha tangazo;
   - Kutaja mtu au shirika linalotangaza;
   - Kutaja watu ambao wanalengwa;
   - Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo;
   - Kuandika masharti ya tangazo;
   - Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;
   - Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma na kuandika mawazo makuu.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma habari kwa mara nyingine

Kazi ya 6:

Mtu kama huyu huonekana kijijini kwetu. Ni mtu anayeupelekea raia ujumbe wa viongozi wa ngazi mbalimbali hasa ujumbe kuhusu utekelezaji wa sera

za serikali kama vile kazi za harambee yaani “Umuganda”, kupiga kura na kadhalika. Ni kiunganishi kati ya ngazi za uongozi na raia.

**D. Msamiati**

Kazi ya 7:

Mkataba: Makubaliano yanayofikiwa kwa kuandikiana baina ya watu au vikundi viwili au zaidi ili kufanya jambo au kazi fulani
Tukio: Jambo lililofanywa au lililotokea
Mtaji: Mali inayotumika kuanzishia biashara au kazi nyingine yoyote ya kuzalisha mali
Maarufu: Kinachojulikana mahali kote
Wadhifa (nyadhifa): Cheo ambacho mtu anakuwa nacho kazini; madaraka

Kazi ya 8:

Kutunga sentensi

Kazi ya 9:

Kutunga sentensi.

Kazi ya 10:

| Lengo la matangazo | Mambo ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo |
|---|---|
| Matangazo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani. | - Kuandika kichwa cha tangazo;<br>- Kutaja mtu au shirika linalotangaza;<br>- Kutaja watu ambao wanalengwa;<br>- Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo;<br>- Kuandika masharti ya tangazo;<br>- Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;<br>- Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo. |

## E. Kuzungumza

Kazi ya 11:

Kuwaambia wengine yale ambayo anayafahamu.

Kazi ya 12:

Kila mwanafunzi ana maoni yake

Kazi ya 13:

| | |
|---|---|
| Matangazo ni maandishi yanayoweza kutoa habari juu ya | mkutano |
| | kifo cha mtu |
| | wizi |
| | mkataba wa amani |

Kazi ya 14:

| |
|---|
| 1. Matangazo mengi ya biashara huwatumia watu maarufu ili kuwashawishi walengwa |
| 2. Maneno ya kisanii katika matangazo hasa ya biashara huwa mepesi kukumbukwa na huwa yanaeleweka kirahisi |

F. Kuandika

Kazi ya 15:

Kuandika tangazo.

Kazi ya 16:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Tunazoea kusikia matangazo yakitolewa na kupitishwa | ili kutomchosha mlengwa |
| 2. Matangazo mengi ya biashara huwa | kwenye redio na runinga, makanisani, darasani na kwengineko |
| 3. Matangazo hutumia maneno machache | lina uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa |
| 4. Matangazo huweza kuwa na lengo la kutoa taarifa, kuonya na kushawishi lakini lengo hilo | yanaambatana na picha |

Kazi ya 17:

Kutayarisha tangazo.

Kazi ya 18:

Kutayarisha tangazo.

# MUHULA WA TATU

# SOMO LA 23: UCHANGANUZI WA SENTENSI ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo ambao unahusu somo hili la ishirini na tatu.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili |
| **Vipindi:** | 18 |
| **Shughuli:** | -Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Sarufi na matumizi ya lugha; -tathmini kuhusu sura |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi na upimaji wa kiujumla |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
|---|---|---|
| Kutambua na kuchanganua sentensi za Kiswahili | - Kufurahia kuainisha na kuchanganua sentensi za Kiswahili | -Mafunzo kuhusu amani<br>-Mafunzo kuhusu ugonjwa wa kuambukiza UKIMWI |

**B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI**

Kazi ya 1:

Kinachoonekana ni mchoro wa sentensi ya Kiswahili ambayo umefanyiwa uchanganuzi

Kazi ya 2:

Picha inaonyesha mchoro wa sentensi ya Kiswahili ambayo umefanyiwa uchanganuzi. Na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 4:

1. Uchanganuzi au upambanuzi wa sentensi ni ufafanuzi wa sentensi unaofanywa katika kujifunza lugha mbalimbali na ambao humwezesha mwanafunzi kuchanganua vipashio vyote vinavyoiunda sentensi kuanzia kwa neno.
2. Ili kufanya uchanganuzi wa sentensi ipaswavyo, unalazimishwa kufuata hatua hizi:
   - Kutaja aina ya sentensi husika. Sentensi inaweza kuwa:

     - Sentensi sahili;
     - Sentensi changamano;
     - Sentensi ambatano;
     - Sentensi shurutia.

   - Kutaja sehemu zake kuu. Sehemu hizo ni kama vile:

     - Kiima;
     - Kiarifu.

Ni lazima kutaja pia sehemu kuu za kiima na kiarifu ambazo ni:
- Kundi la nomino;
- Kundi la kitenzi.

- Kutaja sehemu zote za maneno yaliyotumika katika sentensi husika.

3. Namna mbalimbali za kuipambanua sentensi ya Kiswahili ni kama vile:

   - Njia ya maneno;
   - Njia ya mishale au mistari;
   - Njia ya visanduku au ya jedwali;
   - Njia ya matawi.

4. Katika kuchanganua sentensi, sehemu kuu za kiarifu ni:

   - Kundi la kitenzi;
   - Kundi la nomino.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma habari mara nyingine

**D. Msamiati**

Kazi ya 6:

1. Kiholela: Ovyo(ovyo); bila ya mipango
2. Kuchanganua: Kuchambua dhana, fikira au maandishi
3. Kupambanua: Kuonyesha tofauti waziwazi; kufafanua

Kazi ya 7:

| Aina za sentensi | Njia za uchanganuzi wa sentensi |
|---|---|
| - Sentensi sahili;<br>- Sentensi changamano;<br>- Sentensi ambatano;<br>- Sentensi shurutia. | - Njia ya mishale au mistari;<br>- Njia ya visanduku au ya jedwali;<br>- Njia ya matawi. |

Kazi ya 8:

Katika sentensi zake, anaweza kutumia maneno kama vile “nanasi” au “sharubati”

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 9:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Dada | angekuwa | na | pesa, | mdogo wake asingekosa matibabu |
| Mtoto | angekuwa | na | kalamu, | mwalimu wake asingempa adhabu |
| Bibi | angepigwa | na | bumbuazi, | mume wake asingetunza siri |

**F. Kuandika**

Kazi ya 10:

| | | |
|---|---|---|
| Aliposikia | amewasili | alifoka kwa hasira |
| Alipokumbuka | amekufa | alilia kwa kwikwi |
| Waliposikia | ameondoka | waliingia kwa vigelegele |

Kazi ya 11:

1. UKIMWI huo unaaangamiza watu wengi. (Sentensi sahili)
2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini yeye hataki kwenda shuleni. (Sentensi changamano)

Kazi ya 12:

Uchanganuzi kwa njia ya visanduku

UKIMWI huo unaangamiza watu wengi

- ❖ Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni

| SS | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | V | T | KN | |
| | | | N | V |
| **UKIMWI** | **huo** | **unaangamiza** | **watu** | **wengi** |

| SA | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | | U | S2 | | | |
| KN | | KT | | | KN | KT | | |
| N | V | T | N | | N | Ts | T | E |
| | | | | | | | | |
| Wanafunzi | wote | wameshinda | mtihani | lakini | Sifa | hataki | kwenda | shuleni |

Kazi ya 13:

- ❖ UKIMWI huo unaangamiza watu wengi

- ❖ SS → KN + KT
- ❖ KN → N+V
- ❖ N → UKIMWI
- ❖ V → huo
- ❖ KT → T+KN
- ❖ T → unaangamiza
- ❖ KN → N+V
- ❖ N → watu
- ❖ V → wengi


- ❖ Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini sifa hataki kwenda shuleni


- ❖ SA → S1 + S2
- ❖ S1 → KN+KT
- ❖ KN → N+V
- ❖ N → Wanafunzi

- ❖ V → wote
- ❖ KT → T+N
- ❖ T → wameshinda
- ❖ N → mtihani
- ❖ U → lakini
- ❖ S2 → KN+KT
- ❖ KN → N
- ❖ N → Sifa
- ❖ KT → Ts+T+E
- ❖ Ts → hataki
- ❖ T → kwenda
- ❖ E → shuleni

Kazi ya 14:

- ❖ UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.






Kazi ya 15:

- ❖ Kulinganisha majibu na maelezo
- ❖ TATHMINI KUHUSU SURA YA TATU

Kazi ya 16:

1. Kuandika barua
2. Kutuma simu
3. Kutunga tangazo

# SURA YA 4: UFAHAMU NA UFUPISHO

Sura hii inashughulikia vipengele viwili. Kipengele cha kwanza kinahusu fasili ya ufahamu na kipengele cha pili kinahusu ufupisho. Katika sura hii, muhtasari wa matumizi ya nyakati kuu za kiswahili utashughulikiwa.

## MAANDALIO YA SOMO

Mfano wa maandalio ya masomo kuhusu sura hii ni huu ufuatao:

| MAANDALIO YA SOMO | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shule: | | | | Jina la mwalimu: | | | |
| Muhula wa | Tarehe | Somo | Kidato cha | Sura ya | Somo la | Muda | Idadi ya wanafunzi |
| Kwanza | 20/08/2016 | Kiswahili | Tano | Nne | 1 kwa 3 | Dakika 80 | 32 |
| Makundi ya wanafunzi wenye matatizo ya kielimu na idadi yao:<br>1. Wanafunzi wenye matatizo ya kusikia: 2<br>2. Wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu: 4 | | | | | | | |
| Mada kuu: | Kusoma na ufahamu | | | | | | |
| Mada ndogo: | Ufahamu na ufupisho | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika mada: | Mwishoni mwa sura hii, mwanafunzi ataweza:<br>• Kusoma vifungu vya habari, kuvitafsiri na kuvitolea ufupisho. | | | | | | |
| Kichwa cha somo | Ufahamu | | | | | | |
| Uwezo unaohitajiwa katika somo | Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi ataweza:<br>• Kusoma habari, na kueleza mawazo yaliyomo,<br>• Kujibu maswali ya ufahamu kuhusu kifungu cha habari chochote. | | | | | | |
| Mahali pa kufundishia | Darasani | | | | | | |

| | |
|---|---|
| Malengo ya kujifunza<br>(Ni lazima yazingatiwe mahitaji ya wanafunzi) | Maarifa na ufahamu:<br>• Kueleza mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani ;<br>• Kutoa maana inayopatikana katika aya za kifungu cha habari bila kuyapotosha;<br>• Kukumbuka na kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza katika matumizi ya nyakati za Kiswahili katika hali yakinishi na hali kanushi.<br><br>Stadi:<br>• Kujibu kwa ufasaha maswali yanayojitokeza katika kifungu cha habari husika;<br>• Kuonyesha dhamira kuu au kiini cha habari kinachozungumziwa;<br>• Kuonyesha sehemu kuu za kifungu cha habari na dhamira zake;<br><br>Maadili na mwenendo:<br>• Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine; |
| Vifaa vitakavyotumiwa | Matini zenye habari mbalimbali, taarifa, kanda na vinasa sauti, ubao, chaki, kalamu na kifutio |
| Vitabu vitakavyotumiwa | Kitabu cha Mwanafunzi<br>Mwongozo wa Mwalimu<br>Vitabu vingine vinavyohusu ufahamu na ufupisho |

| Muda na hatua | Mbinu za kufundishia na kujifunzia<br><br>Kwa kupitia kazi za kutafakari picha, kusikiliza, kusoma, kuzungumza, kujadili na kuandika katika makundi au jozi au kwa mwanafunzi peke yake au michezo, wanafunzi wataweza kuelewa vizuri fasihi ya Kiswahili, kusoma kazi mbalimbali za fasihi na kuwaambia wengine yale ambayo ameyasoma. | | Maarifa pamoja na Masuala mtambuka |
|---|---|---|---|
| | Wajibu wa mwalimu | Wajibu wa mwanafunzi | |
| Utangulizi<br><br>[Dakika 8=10%] | -Fuata maagizo yaliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi kama vile kuwaweka wanafunzi katika jozi au makundi mengine, kumpa mwanafunzi peke yake nafasi ya kujibu na kadhalika;<br>-Waache wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha iliyotumiwa;<br>-Wape wanafunzi dakika za kutosha za kuitafakari picha husika;<br>-Waulize wanafunzi wanachokiona kwenye picha iliyotumiwa.<br>-Waongoze katika kutoa maoni yao;<br>-Baada ya kutoa maoni yao, tambulisha somo husika la leo ambalo ni “Mazingira ya hospitali, vifaa na wafanyakazi”. | -Wafuate maagizo yaliyotolewa katika Kitabu chao kama vile kujigawa katika jozi au makundi mengine, kila mwanafunzi kujibu maswali peke yake na kadhalika;<br>-Waitafakari picha kwa makini;<br>-Watoe maoni yao kwa sauti kuhusu picha iliyotumiwa. | Maarifa:<br>- Kueleza mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani ; Kutaja sifa za ufupisho mzuri; Kujadili kanuni za ufupisho wa habari fulani; Kutoa maana inayopatikana katika aya za kifungu cha habari bila kuyapotosha; Kukumbuka na kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza katika matumizi ya nyakati za Kiswahili katika hali yakinishi na hali kanushi<br><br>Stadi:<br><br>- Kujibu kwa ufasaha maswali yanayojitokeza katika kifungu cha habari husika; Kuonyesha dhamira kuu au kiini cha habari kinachozungumziwa; Kuonyesha sehemu kuu za kifungu cha habari na dhamira zake; Kufupisha vifungu vya habari kwa kufuata mwongozo wa ufupisho |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Upeo<br><br>[Dakika 60=75%] | -Waambie wanafunzi wengine wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Baada ya kukisoma kifungu cha habari, wanafunzi wahusishe yaliyomo na ujumbe unaotolewa na picha ile;<br>-Mwambie mwanafunzi mmoja asimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzake yale ambayo ameyasoma.<br>-Waongoze wanafunzi katika kufanya mazoezi yaliyopangwa na kutoa majibu yao;<br>-Jadiliana na wanafunzi kuhusu majibu yao au matokeo ya kazi wanazozifanya. | -Wasome kifungu cha habari kwa sauti;<br>-Wasikilize jinsi mwenzao au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari;<br>-Waige matamshi sahihi ya maneno mbalimbali na kiimbo kinachofaa;<br>-Wahusishe yaliyomo katika kifungu cha habari na ujumbe wa picha iliyotolewa;<br>-Wasimame mbele ya darasa na kuwaambia wenzao yale ambayo wameyasoma;<br>-Wafanye kazi mbalimbali zilizopangwa;<br>-Wajadiliane na wenzao kuhusu majibu ambayo wameyapata au matokeo ya kazi ambazo wamefanya na kuyalinganisha majibu yote yaliyotolewa. | Maadili na mwenendo mwema:<br><br>- Ukuzaji wa tafakuri tunduizi; Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine; Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani<br><br>Masuala mtambuka yanayoshughulikiwa:<br><br>-Mila na desturi na kuzalisha kwa kiwango<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu |
| Mwisho<br><br>[Dakika 12=15%] | -Waongoze wanafunzi katika kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Waachie wanafunzi kazi ya nyumbani | - Kutoa muhtasari wa kazi zao;<br>-Washiriki katika zoezi ambalo limetolewa;<br>-Waandike katika daftari zao kazi ya nyumbani ambayo imetolewa na mwalimu. | |

| | |
|---|---|
| Tathmini ya mwalimu | Kutokana na maoni yake kuhusu jinsi wanafunzi walivyoshiriki katika somo lake, mwalimu achunguze jambo la kutilia mkazo hususan pale ambapo wanafunzi wamekutana na matatizo mbalimbali |

# SOMO LA 24: UFAHAMU WA HABARI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la ishirini na nne.

| | | |
|---|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kuelezea mbinu za kufahamu kifungu cha habari fulani<br>- kujibu kwa ufasaha maswali yanayoulizwa kuhusu kifungu cha habari husika | |
| **Vipindi:** | 24 | |
| **Shughuli:** | -Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika | |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi | |
| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
| Kumwezesha mwanafunzi kusoma vifungu vya habari na kuvitafsiri | -Ukuzaji wa tafakari tunduizi.<br>-Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine.<br>-Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani. | -Mila na desturi na kuzalisha kwa kiwango<br>-Mafunzo kuhusu uzalishajimali<br>-Mazingira na maendeleo ya kudumu |

### B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Tunaona mwalimu ambaye anafundisha somo la “Ufahamu wa habari.”

Kazi ya 2:

Kwenye picha, tunaona mwalimu ambaye anafundisha somo la “Ufahamu wa habari”. Kifungu cha habari nacho kinazungumzia kuhusu “ufahamu wa habari”.

### A. Maswali ya ufahamu

Kazi ya 3:

1. Ufahamu wa habari ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi.

2. Ili kufahamu habari anapoisoma, mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kufanya hivi:

   - Kubaini mawazo makuu;
   - Kutilia mkazo alama za vituo;
   - Kubaini maana ya maneno na misemo tofauti;
   - Kumakinikia kila kipengele anachokisoma.

3. Ili kuifahamu habari anapoisimuliwa, mwanafunzi huyo atafanya hivi:

   Kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji ili asikie vizuri kinachosemwa;
   Kuzingatia vidokezo vya maana ili kujua iwapo msemaji anafafanua au anaongeza jambo jipya;
   Kuandika baadhi ya mambo muhimu ili yamsaidie katika kukumbuka hapo baadaye;
   - Kumakinikia ishara mbalimbali za mwili (kama vile kunyosha mkono, kutingisha kichwa, kupepesa macho na kadhalika).

4. Ni muhimu kubaini maana ya maneno na misemo tofauti katika kuisoma habari ili kuifahamu zaidi kwani ndipo tunaelewa vema maana ya maneno aliyoyatumia mwandishi.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma vizuri mara nyingine

**D. Msamiati**

Kazi ya 6:

Kupotosha: Kitu kuharibika kwa kupoteza sifa kilichokuwa nayo
Kubaini: Kueleza waziwazi; kufafanua
Kurekodi: Kuhifadhi mambo kama vile kwa maandishi au kwa kuyanasa katika kinasasauti au sahani za santuri kwa ajili ya matumizi ya baadaye
Kupepesa: Kuchezesha kope kwa kuzipeleka juu na chini kwa haraka; kukopesa

Kazi ya 7:

Kila mwanafunzi atunge sentensi zake / Mfano: Kalisa angali anarekodi nyimbo zake kwani ni msanii.

Kazi ya 8:

| **Aina za ufahamu wa habari** | **Kutaja alama za vituo** |
|---|---|
| - Ufahamu wa kusoma<br>- Ufahamu wa kusikiliza | - Nukta .<br>- Nukta mbili :<br>- Mkato ,<br>- Nukta mkato ;<br>- Alama za mtajo "..."<br>- Alama ya mshang'ao !<br>- Alama ya kuuliza ?<br>- Alama za mabano (...),<br>na kadhalika |

Kazi ya 9:

| |
|---|
| 1. Anapokuwa na makini kuhusu kipengele anachokisoma, ndipo msomaji anaelewa vizuri jambo analolisoma. |
| 2. Ufahamu wa kusoma ni ule mtu anaoupata katika njia ya kusoma habari, majarida, magazeti na makala mbalimbali. |
| 3. Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi. |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 10

Kutoa muhtasari.

Kazi ya 11:

| | |
|---|---|
| Katika ufahamu wa habari wa kusikiliza, | msikilizaji anatakiwa kumakinikia ishara za mwili |
| | kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji |
| | kuzingatia vidokezo vya maana |
| | kuandika baadhi ya mambo muhimu |

Kazi ya 12:

Kusoma habari na kuulizwa maswali

**F. Kujizatiti na ufahamu wa habari**

Kazi ya 13:

Kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu

Kazi ya 14:

1. Mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi:

    - Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba);
    - Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni);
    - Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno);
    - Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala);
    - Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.

2. Kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni jambo muhimu kwa sababu ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi.
3. “Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili”. Kauli hii ni ya uongo kwani kila mtu (awe mtoto au mkubwa, mtu mzima au mlemavu,... anahusika na usafi wa mwili.
4. “Shule za chekechea”: Ni shule za wale watoto wachanga ambao hawajafikia umri wa kuanza shule za msingi; “Shule za msingi” ni shule zinazotoa mafunzo ya kwanza ambayo ni kama nguzo ya elimu maishani mwetu.
5. Usafi wa kinywa ni muhimu sana kwa sababu madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika.
6. Tunatakiwa kusugua meno mara kwa mara hasa hasa:

    Asubuhi tunapoamka kabla ya kifunguakinywa;
    - Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari;
    - Usiku kabla ya kulala.

7. Tunalazimishwa kunawa mikono yetu kwa ukawaida yaani:

    - Baada ya kutoka chooni;

- Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula;
- Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi;
- Baada ya kutupa takataka;
- Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa;
- Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama;
- Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo;
- Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.

8. Kitendo cha kuosha mikono kinafanyika namna hii:

   - Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni;
   - Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako;
   - Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi;
   - Safisha mikono yako katika maji safi;
   - Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.

9. Ni lazima nguo za ndani za mtu ziwe safi kwa sababu zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya na hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yake.

Kazi ya 15:

1 

2 

3 

**G. Kuandika**

Kazi ya 16:

Kila mwanafunzi ametunga sentensi zake

Kazi ya 17:

1. Uchafu wa mikono unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, kipindupindu, kuhara damu, nimonia, ebola na mengineyo.
2. Upigaji mswaki wa mara kwa mara unashauriwa kwa watu wote.
3. Misingi sahihi ya usafi anayofundishwa na watu hao ndiyo inayomwezesha kutilia mkazo usafi wa mwili wake katika maisha yake ya baadaye.
4. Kuhusu usafi wa nywele, zinaweza kukatwa au kusukwa mara kwa mara na kusafishwa vizuri kwa kutumia maji na sabuni.

Kazi ya 18:

Kila kundi lina hadithi yake

# SOMO LA 25: UFUPISHO WA HABARI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la ishirini na tano.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- Kutaja sifa za ufupisho mzuri<br>- kujadili kanuni za ufupisho wa habari fulani<br>- kutoa maana inayopatikana katika aya za kifungu cha habari bila kuyapotosha |
| **Vipindi:** | 24 |
| **Shughuli:** | - Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Kucheka |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| **Uwezo wa kuendelezwa** | **Mwenendo na maadili mema** | **Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| Kumwezesha mwanafunzi kusoma vifungu vya habari, kuvitafsiri na kuvitolea ufupisho | - Ukuzaji wa tafakari tunduizi.<br>- Ukomavu wa akili kwa kuyatafsiri maoni ya wengine.<br>- Utimizaji wa wajibu katika mbinu za kulitatua tatizo fulani. | - Usawa wa Jinsia<br>- Elimu isiyo na ubaguzi |

**B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI**

Kazi ya 1:

Mwalimu na wanafunzi wake wanaongea kuhusu "sifa za ufupisho wa habari"

Kazi ya 2:

Kifungu cha habari kinazungumzia "ufupisho wa habari" na picha inaonyesha mwalimu na wanafunzi wake wakiongea kuhusu "ufupisho wa habari huo".

**A. Maswali ya ufahamu**

Kazi ya 3:

1. Ufupisho wa habari ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma. Ufundi huo hulenga kuisoma habari, kuielewa vizuri (yaani kuifahamu) na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali.
2. Umuhimu wa somo la ufupisho wa habari kwa mwanafunzi ni kuwawezesha kupima ufahamu wao na uwezo wao wa kujieleza kwa maneno machache.
3. Ni lazima kutumia "ubahiri wa maneno" katika zoezi la kufupisha habari kwa sababu ufupisho huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo. Hivyo, ni lazima kutumia maneno machache iwezekanavyo ili kuyaeleza mambo mengi iwezekanavyo.
4. Mfupishaji hufanikisha shughuli au kazi yake ikiwa wazo kuu au dhamira kuu iliyozungumziwa katika habari imeelezwa kwa kifupi na ikiwa maelezo yanayotolewa yanajitegemea, yaani ikiwa yametolewa bila kuirudia habari asilia.

**B. Kusikiliza**

Kazi ya 4:

Kusikiliza jinsi anavyosoma.

**C. Kusoma**

Kazi ya 5:

Kusoma mara nyingine.

**D. Msamiati**

Kazi ya 6:

Kulenga: Kutuliza macho mahali kwa kusudi la kupata shabaha
Ligi: Mkusanyiko wa timu za michezo kama vile klabu za mpira wa miguu zinazopambanishwa ili kupata mshindi au bingwa
Radhi: Hali ya nafsi kuridhika au kutosheka na matendo ya mtu
Niwie radhi: Ninakuomba msamaha

Kazi ya 7:

Kila kikundi kina sentensi zake / Mfano: Siku hizi watu wanafurahia michezo ya ligi kuu ya Ulaya

Kazi ya 8:

| Sifa za ufupisho wa habari | Hatua zinazofuatiliwa katika kufupisha habari |
|---|---|
| • Huwa ni mfupi kuliko habari ya mwanzo. Kwa hiyo, ni lazima "ubahiri wa maneno" utumiwe;<br>• Huwa na ujumbe ule ule uliokuwa katika habari ya mwanzo;<br>• Hujumuisha mawazo makuu yaliyodondolewa kutoka habari ya mwanzo;<br>• Mawazo haya makuu sharti yapangwe katika mtiririko wenye mantiki. | • Kuisoma au kuisikiliza habari kwa makini na mara nyingi ili kuielewa vizuri. Hatua hii ndiyo iitwayo "ufahamu wa habari";<br>• Kutambua na kubaini mawazo makuu yanayojitokeza katika kila aya;<br>• Kuyaunganisha mawazo makuu na kuandika au kuelezea ufupisho wa habari hiyo kwa maneno yako mwenyewe bila kupotosha maana ya habari ya kwanza; |

| | |
|---|---|
| | • Kuhesabu idadi ya maneno ya ufupisho ili kuyapunguza ikiwa yanazidi idadi iliyotakiwa;<br>• Pitia tena habari ya mwanzo kisha upitie tena ufupisho ili kujiridhisha kuwa hujaacha taarifa yoyote ya muhimu. |

Kazi ya 9:

| |
|---|
| 1. Haya ni matunda ya somo la ufahamu. |
| 2. Ingekuwa vizuri kutukumbusha kwani wengi kati yetu wameisha sahau mengi kuhusu ufupisho au muhtasari. |
| 3. Kumbukeni nyote kuwa ufupisho wa habari ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma. |

**E. Kuzungumza**

Kazi ya 10:

Kutoa muhtasari wa yaliyosomwa

Kazi ya 11:

| | |
|---|---|
| Ufupisho wa habari | huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo |
| | na ujumbe ule ule uliokuwa katika habari ya mwanzo |
| | hujumuisha mawazo makuu yaliyodondolewa kutoka habari ya mwanzo |
| | huwa na mawazo makuu yaliyopangwa katika mtiririko wenye mantiki |

**F. Cheka kidogo**

Kazi ya 12:

Kichekesho.

**G. Mfano wa ufupisho wa kifungu cha habari "Usafi wa mwili"**

Kazi ya 13:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ni | lazima | nguo | nazo | ziwe | safi |
| Ni | vizuri | meno | nayo | yawe | meupe |
| Ni | lazima | kinywa | nacho | kiwe | safi |
| Ni | vizuri | mikono | nayo | iwe | safi |

Kazi ya 14:

Kusoma kwa sauti na kimoyomoyo.

Kazi ya 15:

Kuandika ufupisho wa hadithi.

Kazi ya 16:

Kutoa ufupisho

# SOMO LA 26: MUHTASARI WA MATUMIZI YA NYAKATI KUU ZA KISWAHILI

## A. MPANGILIO WA SOMO LENYEWE

Ufuatao ni mwongozo wenyewe ambao unahusu somo hili la ishirini na sita.

| | |
|---|---|
| **Shabaha:** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- kukumbuka na kuzingatiamabadiliko yanayojitokeza katika matumizi ya nyakati za Kiswahili katika hali yakinishi na hali kanushi |
| **Vipindi:** | 24 |
| **Shughuli:** | -Kuchunguza picha; -Kusikiliza; -Kusoma; -Msamiati; -Maswali ya ufahamu; -Kuzungumza; -Kuandika; -Kucheka |
| **Tathmini:** | Tathmini endelezi |

| Uwezo wa kuendelezwa | Mwenendo na maadili mema | Masuala mtambuka yatakayoshughulikiwa |
| --- | --- | --- |
| Kumwezesha mwanafunzi kuzingatia matumizi ya nyakati kuu za Kiswahili | - Kufurahia kujua kutumia ipaswavyo nyakati kuu za Kiswahili | - Mafunzo kuhusu uzalishajimali (kurutubisha shamba ili kupata mavuno mengi)<br>- Mafunzo kuhusu amani na maendeleo (kutetea haki za watoto na kupiga marufuku ubakaji wa watoto) |

## B. KUSAHIHISHA KAZI MBALIMBALI

Kazi ya 1:

Kuna maandishi yafuatayo “Zinabadilika nyakati.”

Kazi ya 2:

- Wakati uliopo;
- Wakati uliopita;
- Wakati ujao;
- Wakati uliotimilika;
- Wakati wa mazoea;

Kazi ya 3:

Hali yakinishi, wakati uliopita
1. Kabanda alirutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu alisamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali yakinishi, wakati ujao
1. Kabanda atarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu atasamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali yakinishi, wakati uliotimilika
1. Kabanda amerutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu amesamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali yakinishi, wakati wa mazoea
1. Kabanda hurutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu husamehe watu wote waliopora mali yake.

Kazi ya 4:

Hali kanushi, wakati uliopita
1. Kabanda hakurutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu hakusamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali kanushi, wakati ujao
1. Kabanda hatarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu hatasamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali kanushi, wakati uliotimilika
1. Kabanda hajarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu hajasamehe watu wote waliopora mali yake.

Hali kanushi, wakati wa mazoea
1. Kabanda harutubishi shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu hasamehe watu wote waliopora mali yake.

Kazi ya 5:

“Maana ya sentensi hutegemea sana matumizi ya nyakati”. Nyakati ndizo zinazoonyesha iwapo kitendo kilitendeka wakati uliopita, kinatendeka wakati huu ama kitatendeka wakati ujao. Na sentensi inafuata maana hiyo.

Kazi ya 6:

1. Kabanda anarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliopo, hali yakinishi)
2. Kabanda alirutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliopita, hali yakinishi)
3. Kabanda amerutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliotimilika, hali yakinishi)
4. Kabanda atarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati ujao, hali yakinishi)
5. Kabanda harutubishi shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliopo, hali kanushi)
6. Kabanda hakurutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliopita, hali kanushi)
7. Kabanda hajarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati uliotimilika, hali kanushi)
8. Kabanda hatarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati ujao, hali kanushi)

Kazi ya 7:

1. Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, wangenipa kazi ile.
2. Barabara zote zingekuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda lingekuwa safi.
3. Kituo chetu kisingalilenga kutetea haki za watoto, kisingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu.
4. Ukimwadhibu mtoto, atakuwa na nidhamu na mwenendo bora.

Kazi ya 8:

1. Wasingejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, wasingenipa kazi ile.
2. Barabara zote zisingekuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda lisingekuwa safi.
3. Kituo chetu kisingalilenga kutetea haki za watoto, kisingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu.
4. Usipomwadhibu mtoto, hatakuwa na nidhamu wala mwenendo bora.

**TATHMINI KUHUSU SURA YA NNE**

1. Kuchagua hadithi na kutayarisha maswali

2. Kutoa ufupisho wa hadithi

3. Kutunga sentensi

## MAREJEO


1. ABDILAHI Nassir, Tamrini za Kiswahili: Kitabu cha pili, Nairobi, Oxford University Press, 1974
2. Co-Publishing Committee, Hadithi za kwetu, Nairobi, Co-Publishing Committee, 1987
3. INTANETI, Tovuti mbalimbali, Julai 2015
4. INTANETI, Tovuti mbalimbali, Julai 2015
5. MBUNDA Msokile, Misingi ya uhakiki wa fasihi, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi, 1993
6. MINEPRISEC, Ikinyarwanda: Gusoma no gusesengura imyandiko, Kigali, Nzeri 1982
7. Mohamed, M.A. & Saidi, A.M, Kamusi ya Visawe, Nairobi, East African Educational Publishers Ltd, 2002
8. Mohamed, A.M., Sarufi Mpya, Dar-es-salaam, Press and Publicity Centre, 1986
9. Mulokozi, M.M., Fasihi ya Kiswahili, Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, 1996
10. Mulokozi, M.M., Tenzi Tatu za Kale, Dar-es-Salaam, TUKI, 1999
11. NICKY STANTON, Mastering Communication, Hampshire, Macmillan Master Series, 1996
12. NKWERA, F.M., Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo, Dar-es-salaam, TPH, 1978
13. OXFORD University Press, Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi, Kenya, 2007
14. Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, Kitabu cha Kiswahili III B, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Agosti 1987
15. Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, Kitabu cha Kiswahili IV-VA, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Novemba 1987
16. Wamitila, K.W., Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia, Nairobi, Focus Publications Ltd, 2003